Kikao cha Ishirini na Nne - Tarehe 17 Julai, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika: (Ali Abdalla Ali) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi na Ushirika kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Mlinde Mabouk Juma(Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari) : Mhe. Naibu Spika, kwa heshima yako na taadhima kubwa naomba kuwasilisha hati mezani ya Hotuba ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa mwaka 2013/2014. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*).

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 54

Kuhusu Uteuzi wa Viongozi Wakuu wa Jeshi la Polisi (*TPDF*)

(Mhe. Mwakilishi aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 22

Juhudi za Kuwawezesha kuwa Wavuvi Wadogo wadogo

Mhe. Hassan Hamad Omar – Aliuliza**:**

Serikali imeonesha juhudi na dhamira njema kwa wananchi wake kwa kuweka mikakati ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Suala hilo Wizara ya Mifugo na Uvuvi ililipokea vyema na kuahidi kuwaboresha wavuvi wadogo wadogo na kuanda mipango mizuri ya kufikia uvuvi wa bahari kuu.

(a) Je, ni juhudi gani zilizochukuliwa na Wizara katika kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo ili waweze kibiashara zaidi.

(b) Je, Wizara yako imefikia hatua gani katika kuelekea uvuvi wa bahari kuu.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 22 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu katika kuwafanya wavuvi wadogo wadogo waende kibiashara, imefanya juhudi mbali mbali ikiwa pamoja na kujenga masoko katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba na kuyatia majokofu kwa ajili ya kuhifadhia samaki wakati wavuvi wamechelewa kurudi baharini au wamekosa wanunuzi ili waweze kuwauza siku za mbele na kupata bei ya tija zaidi. Aidha Wizara yangu kupitia Mradi wa *MACEMP* ilitoa vyombo na vifaa vya kufanyia kazi kwa vikundi mbali mbali vya uvuvi kama boti za uvuvi, nyavu na mashine. Hatua hii alianza katika mwaka 2005 mpaka mwaka 2011 ili kuwawezesha wavuvi kwenda kuvua masafa ya mbali zaidi na kupata mapato mengi ya ziada.

Kuhusu suala la bahari kuu mpaka sasa wizara yangu inaendelea na utaratibu wa kupata vyombo vya uvuvi kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa vijana na kujenga uwezo wa watakaopewa mafunzo hayo ili waweze kujua aina ya uvuvi watakaoshughulika nao na pia kupata ujuzi wa kuendesha vyombo kwa kufuata sheria za kimataifa. Hii itatoa uzoefu wa kufanya kazi katika maji ya kina kirefu ambapo itapelekea wavuvi hao kuwa baharini zaidi ya masaa 24 mpaka wiki moja, badala ya mazoea ya kwenda na kurudi kwa masaa machache.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Spika, aliyonieleza. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wizara yako inachukua watu kuwapeleka China kwenda kujifunza ufugaji wa samaki.

(a) Je, kuna mafanikio gani katika watu waliopelekwa kule kuwafundisha wenzao ili kufanikisha jambo la ufugaji wa samaki ili kuweza kuepukana na watu wengi kwenda baharini na kupata njia mbadala ya ufugaji wa samaki, kuna mafanikio gani.

(b) Kwa sababu Idara ya Uvuvi imepangiwa shilingi milioni mia moja na wewe unasema kwamba wavuvi wadogo watapata fursa ya kujifundisha

kila kitu ili waweze kufika sehemu ya mbali katika mavuvi yao. Je, shilingi milioni mia moja hii kweli itawasaidia wavuvi wadogo kufanyakazi zao kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:

(a) Mhe. Naibu Spika, wizara yangu imechukua hatua nzuri sana ya kuwapeleka wafugaji wa samaki katika nchi cha China pamoja na India. Lakini vile vile tumefanya utaratibu kwa kushirikiana na wataalamu wetu kuwapitia kila mara na kuweza kuwapa utaalamu wa kudumu pamoja na kutenga mabwawa yenye hadhi yanayoweza kudumu katika kina cha maji ili wasiweze kujenga mabwawa ambayo yana kina kidogo na hatimae samaki wale hufa wakati wanapopata *temperature* tofauti.

(b) Nadhani hii isikupe wasi wasi hivi sasa tayari tumeshaanza mchakato na sheria ile tumeipeleka kwa Mwanasheria Mkuu tayari bodi ya tenda imekaa na kutoa bodi, na mpaka sasa tumepata bodi moja kwa sasa na tumepata vijana 30 kwa kuanzia, na hii isikupe tabu baada ya milioni moja nadhani tukiona hatua inafaa Serikali itaongeza pesa nyengine pale ili kuweza kuendelea na kupata bodi nyengine ili tupate ufanisi.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wavuvi si wanaume tu lakini wapo na wavuvi wanawake ambao wamejipanga na shughuli hizi za uvuvi hasa katika Shehia yangu ya Kangani wapo wanawake ambao wanavua katika bahari. Je, Mhe. Naibu Waziri umejipanga vipi kwenda kuwaona wanawake hao ili kuwapatia taaluma na kuwapatia msaada. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe Naibu Spika, hilo tunataka tupate ushirikiano mkubwa kati ya wizara yangu na wewe Mhe. Mwakilishi ili tukawatembelee hasa kwa kuzingatia *gender* ambao wanawake hawa wanavua kwa umakini zaidi ili tujue njia gani za kuwasaidia.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wananchi wangu wa Paje waliambiwa wajisalimishe wazirejeshe nyavu zao na hadi leo nyavu zile hawajapelekewa nyengine ni lini Mhe. Naibu Waziri ataniahidi kwamba atawapelekea nyavu zile.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, mradi wa *MACEMP* ambao ulikuwa ukitoa nyavu na vifaa mbali mbali sasa tayari umekufa tarehe 15/2. Lakini vile vile wizara yangu inafanya jitihada kubwa ya kupata mradi mwengine na pindipo tukipata na tutashirikiana na wewe Mhe. Mwakilishi ili twende bega kwa bega kule na tuweze kuwapa nyavu

zenye ubora zaidi ili waondokane na zile nyavu haramu ambazo tayari tunazipiga vita serikali.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa Fedha 2013/2014.

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe wachangiaji waliobaki jana ni 15 tungelishauri na kuomba kwamba wale waliokuwa hawajachangia wasitoke toke kwa sababu inabidi unataka kumwita mtu lakini hayupo. Sasa wale wote walioleta majina yao wanaotaka kuchangia wasitoke nje kama wanataka kutoka wana dharura wanijuilishe ili tupate kwenda uzuri kwenye michangio yetu. Kwa hivyo, naanza na Mhe. Ibrahim Hassan Makungu umebakisha jana dakika 10.

Mhe. Ibrahim Hussein Makungu: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi kumalizia mchangio wangu.

Kwanza nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii asubuhi hii ya leo nikiwa mtu wa mwanzo kabisa kuchangia hii bajeti ya Wizara ya Elimu.

Mhe. Naibu Spika, nije hapa kwenye hawa walimu wetu wanaopata posho kwa shilingi elfu tano kwa watu wenye ulemavu. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, hizi fedha ni kidogo sana kwa mahitaji ya wananchi wetu hasa kwa sasa kimaisha. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri atakapokuja anifafanulie zaidi kajipanga vipi kuwaongezea posho hawa walimu wetu au mpango wa baadae uko vipi ili kuwasaidia wananchi hawa.

Mhe. Naibu Spika, hawa walimu wetu wanaowasomesha watu wenye ulemavu kwa kweli wana kazi kubwa mno kwa sababu mimi mwenyewe binafsi yangu nimeshakwenda kuwaona watoto hawa hata ufahamu wao unakuwa mdogo sana. Lakini kwa walimu wetu wanavyojitahidi kwa kweli nawapongeza sana na wazidi juhudi hizo kuziongeza kwa watoto wetu wenye ulemavu ili na wao kuwatoa katika kuwapa elimu bora na kuwaelimisha zaidi.

Mhe. Naibu Spika, pia katika skuli zetu nyingi za Unguja na Pemba kwa kweli Maktaba hakuna. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri atakapokuja kidogo anifafanulie kajipanga vipi kuhusu Maktaba kuziboresha zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nikitazama suala la usafiri kama nilivyosema jana nilipata bahati kutembelea Kengeja kwenye Skuli moja nikaona wanafunzi wanavyotembea masafa marefu na nikawauliza wakajibu wanatembea masafa marefu. Kwa kweli, hali ambayo wanafunzi hawa wanaipata hata ile elimu yao inakuwa shida na unafahamu wao unakuwa mdogo kwa ule umbali wa masafa wanayotaka kufika maskulini kwao.

Lakini nitoe mfano mdogo tu katika Jimbo langu la Bububu kwa kuliona hili ni jambo ni muhimu sana basi tukakaa na wananchi na viongozi kuona kuna umuhimu kuwatafutia usafiri hawa wanafunzi wetu wa Jimbo la Bububu. Lakini ukiangalia hawa wanafunzi kwa kweli hata nauli hawana pesa yao ya kula ukitizama haikidhi kwa ajili ya hali yao duni watoto wetu, tukafanya juhudi ya kutafuta usafiri wa kwenda na kurudi kilomita saba bila ya kutoa nauli yoyote kwa kuwasaidia ili wapate ufahamu mzuri na kuendelea kimaisha. Kama tunavyojua elimu ni kitu muhimu sana katika maisha ya binadamu hasa elimu ya msingi mpaka sekondari.

Lakini pia niseme Mhe. Naibu Spika, je Mhe. Waziri kajipanga vipi katika kuwaweka sawa hawa wanafunzi, kwa kweli hawa wanafunzi wetu hawana mabuku, penseli, peni, kwa kweli vitendea kazi vyote vya kusomea hawana tofauti na sisi tulipokuwa tunasoma enzi zetu tunapata mabuku kila baada ya muda, penseli bure bila ya malipo yoyote. Sijui Serikali kupitia waziri wamejipanga vipi kuwasaidia hawa wanafunzi wetu kama kuwapa motisha ili kuwapa ufahamu mzuri na kuwapa moyo kupitia Serikali yao na kupitia viongozi wao.

Suala hili la kuwasaidia wanafunzi si suala la mtu mmoja, kama Mwakilishi au Mbunge au Wazee au walimu ni suala la jamii nzima kusaidiana kwa pamoja ili kuwasaidia hawa wanafunzi wetu kwa kile kilichokuwa kigumu kuwasaidia kama usafiri, mabuku, penseli kwa sababu hawafanyi kazi hawa wanategemea kupewa na wazee na wazee hali zao ni duni kabisa. Kwa hivyo hili si suala la mtu mmoja ni suala la watu sote viongozi wakuu wote wa kisiasa wote tushirikiane sote kuwasaidia hawa watoto ili tupate watu bora kwenye taifa la kesho ambao watakuja kuliongoza taifa hili wapate elimu nzuri kabisa.

Kwanza niishukuru sana hii *NGO's* ya *Aga Khan Foundation* kwa kujenga madarasa 84, pia ikiwemo kwenye Jimbo langu la Bububu. Kwa hivyo, nawashukuru sana kuona umuhimu wa elimu kwa sababu elimu ni muhimu kwa duniani na kesho akhera. Lakini nataka pia niseme Mhe. Naibu Spika, hawa walimu wetu wa vyuo vya madrassa, pia nilikuwa naomba kupitia Wizara yako ya Elimu uwaangalie vizuri hawa walimu kwa sababu maisha yao yako kwenye hali ngumu sana ya kimaisha. Kwa hivyo, ikiwezekana

naomba sana uangalie japo posho uwapatie kila baada ya muda fulani ya mwezi ili wapate posho, kwa sababu tukisema wana siasa tuwasaidie, kwa kweli hali zetu zinakuwa ngumu saa nyengine hata kuwasaidia hawa walimu wa vyuo vya madrassa kwa sababu wanahitaji mambo mengi na wao na ukitizama hali zao ni duni kabisa.

Lakini nataka niseme Mhe. Naibu Spika, na hawa walimu tuwaangalie hali zao. Tukiangalia sasa hivi walimu wengi wanaacha kazi wanakwenda kwenye sekta nyengine ambayo sio fani zao, wanakwenda kwenye sekta nyengine kufanyakazi kwa kukimbilia maslahi mazuri. Mimi nitoe mfano mdogo tu Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa nasoma mwalimu wangu alikuwa Mbunge wa Mji Kongwe Mhe. Sanya kanisomesha, lakini baada ya muda kaacha fani ile ya kusomesha kenda kwenye siasa kwa sababu kufuata maslahi labda.

Sasa suala kama hili walimu kama hawa wazoefu na kama Mhe. Haroun Ali Suleiman alikuwa mwalimu mkuu, lakini baada ya muda kaingia kwenye siasa. Mhe. Naibu Spika, hawa walimu wetu wakitiwa kwenye fani hii kwa sababu walimu wazoefu na wenye utaalamu wa hali ya juu kabisa. Kama mwalimu wangu wa Mji Mkongwe Mhe. Sanya alikuwa akinisomesha *geograph*, lakini namshukuru sana kwa upeo wake na mafundisho yake mpaka leo nimefaidika mpaka nimefikia hapa namshukuru sana.

Kwa hivyo, tuangalie sana hawa walimu maslahi yao ili wasitoke kwenye hii fani ya ualimu waendelee na wapate kuwapa uzoefu walimu wengine ili waweze kuwa walimu wazuri kabisa na kuwapa ufahamu mzuri wanafunzi wetu ili waweze kujiendeleza katika maisha yao. Lakini niseme pia tu wale wanafunzi ambao waliokuwa nje ya nchi sasa hivi waliokuwa wameshasoma. Naomba pia na wao waangalie warudi kwenye nchi yao waje kuwapa taaluma pia wananchi wengine ambao wanaotaka taaluma ile ambayo wao wamesoma.

Mhe. Naibu Spika, nitoe mfano wangu mdogo. Kuna rafiki yangu mmoja nimesoma naye na alikuwa Marekani miaka 15, anaitwa Abdillah Shaaban lakini leo kaamua kurudi nchini kwao kuwapa taaluma wananchi wengine au vijana wengine ili waweze kujikwamua na hali ngumu ya maisha. Namshukuru sana kwa kurudi hapa ili kuendeleza na kazi mbali mbali za kuwasaidia wananchi wetu kwa ujumla ili waweze kukwamuka na hali ngumu ya maisha.

Mhe. Naibu Spika, pia nataka niseme tu mimi naunga mkono asilimia mia juu ya mia kwenye bajeti hii. Lakini naseme tu jumla la gharama za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali bajeti yake ni ndogo.

Naiomba Serikali kwa heshima zote fedha hizi milioni 15 kwa kuendesha bajeti hii naomba Mhe. Waziri apatiwe ili aweze kujikwamua haya matatizo yake aliyoyasema. Kwa sababu matatizo haya ni mengi na Mwenyezi Mungu amjaalie Mhe. Waziri wetu aweze kuwasaidia hawa walimu na madarassa mbali mbali ili kupata baraka bora kwa wananchi wetu.

Kwa hivyo, naunga mkono pamoja na wananchi wangu wa Bububu asilimia mia moja.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia Hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa katika hali ya uzima na afya na uzima na kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako hili tukufu ili kutoa mawazo yetu katika Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Spika, pili nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kwa kuweza kutoa mawazo yangu. Vile vile nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Naibu Waziri kwa kitabu chake kilivyopambika. Pia niwapongeze watendaji kwa umahiri wao waliomsaidia Mhe. Waziri kufanyakazi hii.

Mhe. Naibu Spika, nikiwa kama Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii mawazo yetu wameshafanyakazi katika kamati yetu. lakini nimesimama kuipa nguvu zaidi.

Kwanza kabisa nitamke rasmi kabla ya mchango wangu mfupi naiunga mkono hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali asilimia mia juu ya mia.

Mhe. Naibu Spika, sasa nikiendelea na mchango wangu katika ukurasa wa 35 sehemu ya 54 naomba ninukuu:

> "Mhe. Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013 Elimu ya Maandalizi ilitolewa katika Skuli 278 zilizokadiriwa. Kati ya hizo Skuli 34 ni za Serikali na Skuli 244 ni za binafsi".

Mhe. Naibu Spika, hapa mimi naipongeza serikali kwa kuweka umuhimu mkubwa wa kuweka elimu ya maandalizi kuwa elimu rasmi katika mfumo wetu wa elimu ya Zanzibar kwa kuzingatia kuwa elimu ya maandalizi ni msingi wa kumjenga mtoto kwa ajili ya awali.

Mhe. Naibu Spika, nimepongeza kwa sababu unafanya maandalizi ya jambo lolote lile basi mafanikio yake makubwa, na kwa sababu hapa una mjenga mtoto katika kumuwezesha ili atakapofika darasa la kwanza afanye vizuri ni jambo jema sana pamoja na maadili mema mtoto huyu akiwa katika malengo sana. Kwa hivyo, naipongeza serikali sana kuwaomba walimu waendelee kuwafundisha watoto wetu katika skuli za maandalizi ili tupate watoto wazuri watakaotuwakilisha baadae katika siku zijazo.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwenye elimu ya msingi. Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa 2012/2013 elimu wa msingi ilitolewa katika skuli 342 zikiwemo skuli 263 za serikali na 79 za binafsi. Idadi ya wanafunzi katika ngazi ya elimu imefikia laki mbili arubaini na saba mia tatu hamsini na tatu sawa na asilimia 124.4 ikilinganishwa na asilimia 121.5 ya mwaka 2011/2012.

Aidha watoto wote thalathini na tano elfu mia saba na tatu waliandikishwa kuanza darasa la kwanza katika skuli za serikali wamepatiwa nafasi, miongoni mwa watoto hao kumi na saba elfu nane na sitini ni wanawake na kumi na saba mia nane arubaini na tatu ni wanaume.

Vile vile hapa niipongeze serikali kwamba watoto wote waliopatiwa nafasi na kuandikishwa kuanza masomo yao ya darasa la kwanza. Lakini niseme tu pamoja na mambo mazuri ambayo yamefanyika lakini katika elimu ya msingi kuna changamoto nyingi sana, na changamoto ya upungufu wa walimu, walimu wetu ni kidogo sana na hii iko katika Wilaya ya Micheweni, Wete, Chake-Chake na Mkoani kote. Lakini tu naomba nitoe mfano ulio hai ndani ya jimbo langu katika Skuli ya Kojani kisiwani kuna madarasa yasiopungua 16 pamoja na msingi lakini walimu wake ni 16 jambo ambalo halikidhi haja unampa wakati mgumu mwalimu anayefundisha.

Lakini jambo la kusikitisha zaidi ni kuwa kuna vijana wetu wanapoomba nafasi ya kuajiriwa lakini wanapata wakati mgumu. Nadhani wakati wa kuajiriwa kila mtu anapita ndani ya Wilaya yake na nafasi zinapokuja zinagaiwa kwa wilaya kwa nafasi zilizoombwa na zilizopatikana. Jambo la kushangaza mtu anapopeleka maombi hata barua yake haionekani ni afadhali alisipate lakini katika maombi yake yawepo.

Mhe. Naibu Spika, mtu anapeleka maombi yake lakini anaambiwa hatuioni barua yako ni sababu gani za msingi zinazofanya hivyo. Hayo ni matatizo makubwa sana Mhe. Naibu Spikia, lazima tuseme watoto wetu wasome na baadae wapate mafanikio ili kupata ajira na baadae warudi kwenda kuwafundisha wenzao.

Mhe. Naibu Spikia, jambo la kusikitisha na zaidi tumezungumza hapa kama watu wanaomba ajira kwa mujibu wa wilaya zao, lakini leo kaajiriwa mtu kutoka Mkoani Chochoko, waliomba Wilaya ya Wete hawakupata lakini kaajiriwa mtu katika Wilaya ya Wete, anatoka Mkoani Chokocho na anasomesha pale Mzambarau Takao, lakini watu walioomba Wilaya ya Wete hawapati kwa nini hili ni tatizo na naomba lipate ufumbuzi. Sisi kama watu wa kisiwa tunawasomesha watoto wale ili wapate kuwasomesha wenzao Mhe. Naibu Spika, kisomo unakijua na pana usumbufu wa usafiri, hata walimu wanakuwa woga kuvuka mara kwa mara.

Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu kidogo tu nieleze sera fupi tu mwaka 1979 ilitokea pale walimu wanaofundisha Kojani na kurudi majumbani kwao basi Mtumbwi ulizama na baada ya kuzama kwa bahati mbaya mwalimu mmoja alifariki na alipofariki muda wa siku 3 hakujaonekana tukamuona siku ya 4. Leo kama hakuna upendeleo watoto wetu wanaosoma kwenye kisiwa tukipata walimu kutoka pale kisiwani ni jambo zuri, kuna mtoto huyu anaangaliwa cheti, sasa hivi diploma anakwenda kuomba kazi anaambiwa kuwa barua yake haionekani ni tatizo. Mhe. Naibu Spika, tunamuomba Mhe. Waziri ulichukue hilo na alifanyiekazi.

Mhe. Naibu Spika, kijana huyu anaitwa Chum Omar Sheha ni mtu wa kisiwani kule ana diploma lakini barua yake sasa haionekani hili ndio kosa kubwa sana, afadhali ingekuwa imeonekana ukaambiwa hukupata tungeridhika nalo, lakini barua haionekani kwa sababu gani zinachakachuliwa.

Mhe. Naibu Spika, nasema kuna tetesi Chuo cha Ualimu kilichojengwa Mchangamdogo katika Jimbo la Kojani kwa ajili ya wanafunzi wa Benjamin walioko Wete, lakini kuna tetesi kuwa chuo hicho wataletwa wanafunzi kutoka SUZA. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa basi atueleze jambo hili ni kweli au ni hizo tetesi tu, wananchi wana wasi wasi, kule kumejengwa chuo kile kwa sababu nafasi ni finyu Benjamin. Kwa hivyo, tunamuomba atakapokuja hapa Mhe. Waziri aliweke sawa tu hilo.

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, ni ndani ya kisiwa cha Kojani katika skuli ya Kojani, kuna madarasa matatu, yamejengwa tangu mwaka 2005 mpaka hii 2013 ni miaka 8, banda lile bado halijaezekwa. Tunaiomba serikali iwasaidie waliezeke banda lile ili wanafunzi wapate kusoma kwa mazingira yaliyokuwa mazuri, Mhe. Waziri hii ni miaka 8 tena. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa hili suala aliweke sana kwamba banda lile katika bajeti hii litakuwa katika kuezekwa au vipi.

Mhe. Naibu Spika, kama haitoshi hiyo ndani ya Jimbo la Kojani katika Skuli ya Maziwani iliyoanzishwa, watoto wa darasa la nne na la tatu wanasoma kwa pamoja. Mhe. Naibu Spika, hili ni tatizo, hivyo pale Maziwani wameanzisha skuli yao na inaendelea vizuri lakini bado mabanda hayakidhi haja. Wanafunzi wa darasa la tatu na la nne wanasoma kwa pamoja ambapo kuna wingi wa wanafunzi, hiyo inaleta kutofahamu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kunipa maelezo mazuri, wala sina haja ya kupiga buti kwa sababu hii ni wizara yangu nimeifanyia kazi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anipe maelezo mazuri kuhusu mambo niliyouliza. *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu wizara yake itapita bila ya matatizo yoyote. Ahsante sana nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia fursa ya kuweza kutoa mchango wangu kuhusu hoja iliopo mbele yetu. Awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha kuwa hai na kutupa nguvu na uwezo wa kuondoka katika maeneo yetu hadi hapa. Hii ni hazina kubwa aliyotujaalia Mwenyezi Mungu na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Mara baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya wapiga kuwa wa Jimbo langu la Wawi, naomba niendelee kumtakia afya njema Mzee Nelson Mandela, Rais mstaafu wa Afrika ya Kusini (Madiba), ili aweze kusherehekea vizuri mwaka wake wa 95 unaomfikia kesho.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, sasa niende moja kwa moja katika hoja iliopo mbele yetu. Nianze na Idara ya Mafunzo ya Walimu Mhe. Naibu Spika, kama kuna watu muhimu sana katika nchi yetu wanaohitaji kufunzwa na kuenziwa, basi ni walimu. Mhe. Naibu Spika, mwalimu huwezi kumfananisha na sonara kwa sababu sonara anashughulika na vito tu yeye, umpelekee vito avitengeneze, pia huwezi kumfananisha na fundi wa nguo kwa sababu yeye anashughulika na nguo tu, vile vile huwezi kumfananisha mwalimu na mvuvi, kwa sababu mvuvi kazi yake anashughulika na samaki tu hawezi kushughulikia mbao. Aidha, huwezi kumfananisha na kapenta kwa sababu kapenta anashughulikia mbao tu.

Kwa hivyo mwalimu Mhe. Naibu Spika, ni mtu mmoja muhimu sana *multipurpose industry* inatoa kila kitu. Mhe. Naibu Spika, ndio nikasema kwamba kama kuna mtu anahitaji kutunzwa na kuenziwa basi ni mwalimu. La kusikitisha sana katika nchi yetu Mhe. Naibu Spika, kama kuna watu waliopewa mgongo na kama kuna watu ambao jamii na serikali yao haiwaenzi basi ni hawa walimu, hususan hawa walimu wetu ambao elimu yao

ni ndogo, wale walimu wetu wa *grade A* ambao ni wa zamani na hawana elimu, wanatengwa sana kimaslahi na serikali.

Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana kuona mwalimu amemfundisha mwanafunzi wake, mwanafunzi wake karudi kusoma ana digirii yake basi anapitwa kwa maslahi kwa kiasi kikubwa sana, hii inawavunja moyo sana walimu, hususan wale walimu wetu wa zamani ambao wana uzoefu mkubwa sana katika suala zima la kufundisha.

Mhe. Naibu Spika, katika hili mimi nadhani serikali iangalie vizuri ili kuwaenzi hawa walimu hususan walimu wetu wa zamani. Mhe. Naibu Spika, inasikitisha kumuona mwalimu anaajiriwa leo wa *diploma* ya *primary*, anapata zaidi ya shilingi 200,000, lakini mwalimu mwenye cheti cha *grade A* ambaye ana miaka 25 skulini hafiki shilingi 200,000, hili ni tatizo. Kwa msingi huo Mhe. Naibu Spika, nadhani kuna haja ya kuweka *scheme of service* maalum kwa ajili ya walimu na iwaenzi wale walimu wetu wa zamani kabisa.

Mhe. Naibu Spika, unamkuta mwalimu ana umri wa miaka karibu 60 au 55 pale basi anavaa yebo yebo na kanzu yake ina viraka, ni tatizo hivyo tuwasaidie hawa walimu. Aidha, katika suala zima la ualimu kuna hizi likizo za walimu. Mhe. Naibu Spika, kuna walimu ambao karibu miaka minne nyuma hawajapata huduma ya likizo hadi leo hii, hili ni tatizo.

Mhe. Naibu Spika, nimeangalia katika hili buku kubwa kwenye kasma ya 211104, kuna karibu shilingi milioni 500 zipo kwa ajili ya likizo. Kwa hivyo, naiomba sana serikali pesa hizi zitolewe na zitumike kwa dhamira iliyokusudiwa na sio kujenga majengo au kusafiria hizi pesa. Hizi ni lazima ziende moja kwa moja katika kutoa huduma ya likizo kwa walimu wetu.

Mhe. Naibu Spika, nije katika stahiki za walimu baada ya kumaliza masomo, hapa ndio pabaya sana, maslahi ya walimu baada ya kumaliza masomo yao ni tatizo, serikali imekuwa ikiwafumbia macho na kuwafanyia jeuri. Mtu anamaliza masomo anakaa karibu miaka mitatu au minne maslahi yake hayajarekebishwa. Kwa mfano hapa kuna walimu ambao wamemaliza vyuo mwaka 2012 lakini mishahara yao haijarekebishwa. Sasa nataka waziri akija kufanya majumuisho hapa basi anieleze walimu wale mishahara yao hii itarekebishwa lini na tofauti ya maslahi yao watalipwa lini.

Mhe. Naibu Spika, aidha kuna hoja kongwe sana hapa ambayo nilikuwa nayo kwa muda mwingi, kuhusu maslahi ya walimu ambao wamemaliza mafunzo yao yaani *Teachers Advance Programme*(*TAP*). Nimeambiwa katika kipindi kilichopita kwamba walimu hawa watalipwa mafao yao, hoja hii niliianza

zamani sana ndani ya Baraza hili, tangu Mhe. Ramadhan Shaaban Shaaban ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban alinipiga maneno wee! kwamba tutawalipa mpaka kaondoka kwenye hii wizara na kenda kwenye wizara nyengine Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban hawakulipwa walimu hawa.

Mhe. Naibu Spika, kaja mzee wangu hapa anayeishikilia sasa hii wizara Mhe. Ali Juma Shamuhuna, mzee wangu huyu namuheshimu sana na yeye kanipa maneno yale yale kwamba atawalipa walimu wa *TAP*, hadi leo hii walimu wale hawajalipwa mafao yao. Kwa hili pamoja na kwamba namuheshimu sana mzee wangu hapa Mhe. Ali Juma Shamuhuna lakini nataka nizuie kifungu mpaka anihakikishie kuwa ni lini walimu hawa waliomaliza mafunzo ya *TAP* watalipwa. Kama itapitishwa kwa nguvu mimi nitaomba nitoke ndio lipitishwe.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri mzee wangu namuheshimu sana na ninamuogopa kabisa lakini sina vya kufanya tunatetea maslahi ya wananchi hapa, anieleze. Yeye aliniambia kwamba kishapeleka barua kwa Mhe. Haji Omar Kheir ya kuomba malipo yao. Sasa hivi kuchelewa nataka nijue ni jeuri tu ya Mhe. Haji Omar Kheir ama vipi, au ni alikuwa anawafanyia hiyana tu hawa, kama ni hiyana tujue la kufanya na kama ni jeuri ya Mhe. Haji Omar Kheir japo bajeti yake imeshapita lakini tujue vya kufanya vile vile.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani tuwaenzi walimu, hakuna hata mmoja hapa aliyekuwa hakupita mikononi mwa walimu, mpaka wewe Spika wetu unayetuongoza hapa umepita mikononi mwa walimu. Leo walimu wamemaliza mafunzo ya *TAP* mwaka wa tano wanafanyiwa jeuri hapa. Mimi basi nikae tu nipitishe bajeti bila ya kujua. Hii nitazuwia kifungu mara hii kwa sababu ni hoja nzito na ya zamani sana.

Mhe. Naibu Spika, mwaka jana tuliambiwa hapa kwamba walimu hawakuongezwa mishahara yao kwa sababu watapandishwa ngazi za mishahara. Sasa nilikuwa nataka nijue ile ahadi tuliyopewa kwamba watapandishwa ngazi ya mishahara yao walipandishwa au ndio yale yale maneno tu.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu walimu na nauli. Mimi katika hili serikali ione huruma walimu wetu wengi wanatoka mbali, vipando hawana na wengine hata viatu wanavaa yebo yebo ambavyo vinaingia mwiba. Sasa utakuta mwalimu ana sota huku miba inamuuma na mpaka anafika skuli anafundisha, halafu nauli yake inacheleweshwa, hili ni tatizo. Kwa hivyo, naomba fedha hizi tulizoziona huku za nauli basi zitolewe na ziwafikie walimu tena kwa wakati, sio katika masuala ya kukopwa au na wao walimu wakiwa hawakuja

skuli kufundisha waseme mpaka tupewe nauli hawatoonekana wabaya hawa. Basi Mhe. Naibu Spika, katika hili naomba nauli na maposho ya walimu yatolewe kwa wakati tena, maslahi pamoja na nauli.

Halafu Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika majengo ya skuli. Mbali na walimu mazingira ya kufundishia ni lazima wanafunzi wawemo katika majengo mazuri ya skuli ili elimu iweze kupatikana vizuri. La kusikitisha mheshimiwa ni kwamba maeneo mengi kunakuwa na uchache wa majengo ya skuli zetu. Napenda niishukuru Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na mzee wangu pale waziri kwa kuweza kuwahamasisha wananchi kuweza kuingiza juhudi zao katika suala zima hili la kujenga majengo ya skuli katika maeneo yao.

Aidha, napenda niwapongeze wananchi wa maeneo mbali mbali serikali za Shehia, Madiwani, Wawakilishi, Wabunge kwa kuweza kuwa na moyo wa kujenga mabanda ya skuli katika maeneo yao ili kuisaidia serikali yetu. Lakini Mhe. Naibu Spika, serikali huwa inachukua ahadi kwamba mabanda yale baadae watamalizia, inasikitisha sana kwamba mabanda yale hayamalizwi kabisa. Mimi niliahidiwa nitamaliziwa banda lile la ng'ambwa, sijenda kwa siku mbili hizi lakini nina hakika halijamalizwa. Niliahidiwa kuna banda kule la Furaha litamaliziwa, halijamaliziwa, kuna banda la Skuli ya Vitongoji Msingi limeshamaliza mpaka linta sijamaliziwa. Sasa sijui waziri katika hili ataniambia nini na wakati huku zimeombwa katika kasma ya 220702, kasma hii inazungumzia suala zima la matengenezo makubwa ya majengo *major maintenance* katika Ofisi Kuu Pemba huko, mtapatiwa shilingi milioni 140,000,000. Kwanza naomba waheshimiwa hizi shilingi milioni 140,000,000 muwape hawa tena wapewe kwa wakati, lakini mkipewa tu basi muende mkanimalizie banda langu la Ng'ambwa kule, mrudi mje mnimalizie banda langu la Skuli ya Vitongoji ya Msingi pale.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kuna mabanda mengi sio ya skuli yangu tu, kuna waheshimiwa wanalalamika kuwa hayajamalizwa. Kwa hivyo, kila penye mabanda basi tujitahidi tuyamalize.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie suala zima la mabanda ya skuli zetu na hati miliki. Mhe. Naibu Spika, kumekuwa na tatizo, ardhi za skuli zimekuwa zikimezwa, zikivamiwa, zikichukuliwa na wafanyabiashara pamoja na watu tu jambo ambalo ni tatizo sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nashangaa kwa nini tangu tuzianzishe miaka ya 60 skuli hizi hazina hati miliki. Wewe Waziri wa Elimu uko hapo, Waziri anayeshughulika na mambo ya ardhi huyo hapo ni suala la kumnong'oneza tu na yeye akatoa amri, sijui ni lugha gani mnazotumia hasa, mna urasimu gani.

Ikiwa wewe Mhe. Shamuhuna uko hapo na Mhe. Ramadhan Abdalla anayeshughulikia mambo ya ardhi yuko pale ukimwambia kwa mdomo tu, bwana skuli fulani inataka hati miliki anasikia na yeye ataagiza watendaji watoe hati miliki. Sasa huu urasimu wa aina hii unatoka wapi. Mimi ndio nikasema kwamba mambo yanawashinda nyinyi serikali, sisi tupeni au tuazimeni hiyo serikali kwa muda wa kama miezi mitatu tu, chini ya uongozi wa Mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi hapa na Mnadhimu wa CUF pale, mtupe wiki tatu tu, skuli zote tutazipatia hati miliki. Nyinyi siku zote mnatuhangaisha kiasi hiki jamani, hebu ondokeni huko mbele kiasi cha wiki tatu muje *backbenchers* huku, aah! aibu, *shame*, inasikitisha. Skuli nyengine tangu miaka ya 60 hazina hati miliki, hati miliki hizo zinataka dhahabu ndio zipatikane kwamba hatuna hapa Zanzibar au zinataka kitu gani, naona ni maneno tu kutoka kwa waziri mpaka kwa waziri na Mhe. Ali Juma Shamuhuna yuko karibu sana na Mhe. Waziri Ramadhan Abdalla Shaaban, ukimwambia kwa mdomo mtu. Hebu tupisheni hapa tuongozwe na Mhe. Abdalla Juma na Mhe. Salmin Awadh waje waongoze serikali chini yetu sisi muone kama mambo hayakwenda safi sisi *backbenchers* hapa, mshashindwa bwana.

Jengine sasa, Mhe. Naibu Spika,...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ujali muda bado dakika tano.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante Mhe. Naibu Spika. mradi wa uimarishaji elimu ya maandalizi. Mhe. Naibu Spika, napenda sana niiambie serikali katika hili kwamba imefanya jambo la msingi sana kuimarisha elimu hii ya maandalizi. Lakini kuna mapungufu mengi hivi sasa wakati nazungumzia elimu ya maandalizi hakuna ile mitaala ya pamoja ambayo inasimamia elimu hii. Kila skuli ya maandalizi ina mitaala yake, jambo ambalo linaifanya hii elimu isiwe *homogeneous*, matokeo yake baada ya kumaliza elimu ile kwa miaka mitatu wale wanafunzi wanatofautiana kiuwezo. Sasa mimi naomba kwamba katika hili kuwe na mtaala wa pamoja utakaosimamia skuli zote za serikali na zile za binafsi, msiwaachie tu huko.

Halafu Mhe. Naibu Spika, kiko wapi chuo cha mafunzo ya walimu wa maandalizi, hawana chuo wanategemea ile skuli ya maandalizi ya Saateni, kwa nini tusiwajengee chuo hawa walimu wanaosomesha hii skuli ya maandalizi ikawa ni chuo cha walimu wa maandalizi peke yake, lakini mnategemea lile jengo pale la Chekechea vipi mambo haya jamani. Mimi nadhani kuna haja Mhe. Waziri kuwepo na chuo hasa kitakachofundisha walimu wa skuli za maandalizi kijulikane hiki ndio chuo cha walimu wa maandalizi tu, lakini kudandia tu pale, hiyo sio vizuri.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende haraka kwa sababu umeniambia muda, sasa niende kwenye chuo cha mafunzo ya amali. Mhe. Naibu Spika, kipengele chengine nitakachozuwia shilingi ni hapa, ni kutolipwa kwa wananchi wa Vitongoji baada ya mazao yao kukatwa katika kupisha ujenzi wa hiki Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji. Mhe. Naibu Spika, wameshaanza kulipwa wale, lakini wamelipwa kidogo sijui watamaliziwa lini. Sasa nataka Mhe. Waziri aje aniambie kaanza kweli kuwalipa wale watu wa pale Vitongoji kwa ajili ya kujenga kile Chuo cha Mafunzo ya Amali pale Vitongoji lakini wamepewa malipo robo. Sasa hivi fedha zilizobakia watalipwa lini au ndio atakuja kunipiga maneno tu hapa. Mimi mara hii nataka uniambie hasa ni lini mtakuja kuwalipa.

Jengine Mhe. Naibu Spika, kwa haraka niende katika suala zima la Kitengo cha Michezo na Utamaduni katika ukurasa wa 78. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri hapa naomba unisikilize vizuri kwenye hii wizara. Mhe. Naibu Spika, katika hili mambo ya utamaduni sisi hatuna matatizo tena kwa sababu rusharoho ninavyoiangalia huko kwenye TV inavyochezwa basi naamini kwa utamaduni hivi sasa tuko mbele sisi, tatizo letu ni michezo.

Mhe. Naibu Spika, mimi naishauri wizara ianzishe mitaala ya michezo kuanzia *primary*, ni jambo la aibu katika nchi kwenye tasnia ya michezo kuwa tumekuwa vichwa vya wenda wazimu. Mzee Ali Hassan Mwinyi alisema katika kipindi fulani kwamba sisi katika timu zetu tunakuwa ni vichwa vya wendawazimu. Mimi naomba kwamba utujengee msingi, naiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ianzishe mtaala wa mambo ya michezo. Hapa palikuwa na chuo kinachotoa Stashahada ya mambo ya *Physical Education* pale Nkrumah kipindi kile haipo tena.

Sasa namuomba *professor* Rai hapa wao ndio ma-*technician* wetu na wataalamu wetu katika masuala haya, watuondoshe katika dhila hii ya kufungwa kila siku. Kila siku timu zetu zikienda nje zinafungwa. Naamini mimi kwamba mkitutolea wataalamu pale SUZA, mkianzisha ile *Department* ya *Physical Education and Force* hapo, basi mngetuzalishia wataalamu ili waje wawafunze vijana wetu huku baada ya mtaala kuanzishwa ili tuweze kujiweka vizuri katika masuala ya hii tasnia ya michezo na burudani.

Mhe. Naibu Spika,

Mhe. Naibu Spika: La mwisho.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Nimalizie Mhe. Naibu Spika, kwa kuomba kwamba taasisi zetu hizi za elimu ya juu kikiwemo Chuo chetu Kikuu cha SUZA na hivi Vyuo Vikuu vyengine vya binafsi, vitusaidie yaani *faculty*

ziende kwa mujibu wa mazingira. Nimpongeze *Professor* Rai ameanzisha *Department of Environment.* Juzi tulishiriki katika kufungua mambo ya madawa. Tunasema na kile Chuo cha Zanzibar kule Tunguu na wao waweze kuanzisha mambo haya, kusudi tuweze kukabiliana vizuri na mazingira pamoja na tiba. Kwa hivyo, waanzishe na wao hizi sayansi za tiba kama vile wenzao wanavyotaka kuanza SUZA.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, naomba nikae huku nikimsubiri waziri anipe jibu la kwa nini walimu waliomaliza mafunzo ya *TAP* pamoja na wale wakufunzi wao watawalipa mafao yao, sambamba na kumaliziwa fidia zao wale waliokatiwa miti yao pale katika Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji, naomba kukaa. Nitakapopata maelezo ya kutosha katika hili nadhani nitakuwa sina sababu ya kutokuunga hoja yako mkono. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Abdalla Mohamed Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia fursa asubuhi hii ya kuzungumzia makadirio na mapato ya wizara ambayo kwa maoni yangu ni muhimu sana kwa maendeleo ya mwanadamu.

Mhe. Naibu Spika, wengi wamezungumza hapa na mimi nataka nijitokeze kuzungumzia machache. Mhe. Naibu Spika, hivi sasa wizara yetu inapita maskulini na kuwahamasisha wananchi hasa walimu, wakiwaeleza kwamba tunahitaji uwepo mkubwa wa mabanda ili kutosheleza wanafunzi wetu. Kwa jumla wananchi wetu wameitikia wito huo, kila skuli hivi sasa ukenda unakutia kuna mabanda mapya. Aidha wameshafika hatua ya kuezekwa au hatua za kupigwa plasta na mengineyo.

Mhe. Naibu Spika, ninachokijua ni kwamba hatua ya umalizikiaji wa mabanda haya mara nyingi unakuwa chini ya wizara. Lakini la kusikitisha ni kwamba mabanda haya yanakaa muda mrefu, kiasi kwamba mengine hata zile linta zinaanguka na inapofika wakati wa kutaka kuyaezeka inakuwa ni usumbufu mwengine kwa wananchi. Sasa labda niulize tu.

Je, utaratibu ukoje wa kuyakarabati mabanda haya na labda kwa mwaka huu wa 2013/2014 unatarajia kukarabati mabanda ya sehemu gani. Hii ningepata kujua, labda ingenisaidia kwa sababu waheshimiwa na sisi huwa tunajitahidi katika kuchangia maendelezo ya mabanda haya. Sasa ningepata kujua labda banda la Skuli ya Wambaa au Skuli ya Ng'ombeni itaezekwa basi nitajua fedha za mfuko wa maendeleo ya jimbo nizipeleke sehemu gani.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa tunavyoambiwa kwamba elimu ya lazima sijui ni mpaka kidato cha IV. Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi nina masikitiko kidogo na maendeleo ya elimu ambayo tunayo hivi sasa, tukiangalia *data* za mwaka

2012/2013 basi utakuta asilimia ya ufaulu ni 17 ya kidato cha IV, mitihani hii haiko katika mikono yetu, iko katika Serikali ya Muungano.

Sasa labda niulize Mhe. Naibu Spika, kwa mwenendo huu kuwa kila leo matokeo yetu yanakuwa duni na mabaya, sijui hatuoni haja ya serikali kuona kwamba mfumo huu ambao tunao tuubadilishe na tuuweke katika ngazi nyengine. Lakini hata nikienda katika kidato cha VI matokeo pia yako 32.6. Hii pia inatia unyonge kuona kwamba matokeo yetu ni mabovu. Sasa je, utaratibu huu tutaendelea nao mpaka lini na hatuoni kwamba kuna haja hivi sasa ya utaratibu huu kuubadilisha.

Mhe. Naibu Spika, niende katika sehemu ya uhamisho wa walimu. Mara nyingi skuli zetu Mhe. Naibu Spika, zina walimu wa jinsia mbili; kuna wanawake na wanaume. Jinsia moja mara kwa mara huwa inahama kutoka sehemu moja na kwenda nyengine. na hasa pale inapotokea riziki ya nusra. Lakini inapotokea jambo kama hilo wizara inakuwa ngumu kutoa uhamisho hasa kwa walimu wanawake. Sasa sijui haioni kwamba kufanya hivyo au kumzuia mwalimu ambaye amepata nusra inakuwa ni kinyume na haki za binadamu. Kwa hivyo, lini itaona iweke utaratibu maalum wa kuona kwamba hawa na wao wanapewa haki yao ya msingi ya kijamii ili linapotokea jambo kama hilo basi na wao ile fursa wakapewa wakaondoka na kuweza kuitekeleza na kuwanyima haki zao nafikiri si jambo la busara. Nadhani ni vyema tungeandaa utaratibu ambao na wao utawawezesha kupata haki yao hii ya msingi. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, katika hilo pia niseme kwamba walimu mara nyingi wanakuwa hawana utaratibu wa kujua hasa mwaka gani watapata likizo lake na inakuwa ni usumbufu, hata ukaandikiwa hiyo barua kwamba wewe umepata likizo basi hujui ile huduma yako ni mwaka gani au utaipata vipi na inakuwa ni usumbufu.

Labda taratibu zao Wizara ya Elimu hasa za kutoa likizo ziko vipi? Mhe. Naibu Spika, najua kwamba ni kila wakati maalum na pia siku hizi ni *flat rate*, yaani kila mfanyakazi anatakiwa apewe kiwango maalum, lakini upatikanaji wake ni wa kusumbuka sana na wala hauna uhakika. Vile vile wafanyakazi hawa Mhe. Naibu Spika tunawakutia na wao wana usumbufu wa kupata malimbikizo yao. Kwa kweli walimu wengi wanaporudi vyuoni wanakuwa hawapati marekebisho ya mishahara yao haraka sana na sijui hii inasababishwa na nini, kwa sababu na wao wanakuwa tayari wamo kwenye *nominal role* wanajulikana kwamba mwaka fulani watarudi na kipindi gani wataripoti kazi, lakini wanaporipoti inakuwa ni usumbufu kupata haki au nyongeza zao.

Pia malimbikizo yanachukua muda mrefu mpaka kwamba yanakatisha tamaa. Kwa hivyo, sijui wizara hii na kwa nini iwe ni wizara hii tu, kwa sababu huko kwengine utaratibu naona unaendelea vizuri.

Mhe. Naibu Spika, sasa kidogo niende kwenye sehemu nyengine za kutoa huduma ya elimu. Ninachokijua ni kwamba katika nchi hii Mhe. Naibu Spika, kuna vyuo vingi ambavyo vinatoa elimu kama vile Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka, Chuo cha Afya, Chuo cha Kilimo na vyenginevyo. Sasa nikiangalia idadi ya raia wa nchi hii nawaona ni kidogo sana na nina mawazo na ninajiuliza sijui kwa nini vyuo hivi visiungwe katika hichi chuo chetu tulichonacho kimoja cha Chuo Kikuu cha Zanzibar (*State University of Zanzibar). (Makofi).*

Hivi sasa Chuo cha Kilimo kiko miaka mingi lakini maendeleo yake Mhe. Naibu Spika, ni machache sana na sijui kama hiyo *diploma* wameshaanza. Kwa nini wizara au serikali isione umuhimu, sasa kwa mfano vyuo hivi tukaviunga vikawa kama ni *school of agriculture*, ili tukapata kuviendeleza zaidi kwa sababu nina imani kwamba vyuo hivi. vitakapokuwa chini ya *umburella* ya *State University of Zanzibar*, basi maendeleo yake yatakuwa kwa haraka sana kuliko kwenda wao peke yao.

Mhe. Naibu Spika, pia tukenda katika Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka. Mimi nasikitika sana kwamba chuo hichi mitihani yake inatoka *NACTE* ambayo inasimamiwa Tanzania Bara. Sasa hatuoni kwamba wakati wowote labda kwa rasimu tuliyonayo pengine itakuwa kila mmoja kwake na chuo hichi tukakirudisha na kikawa kinafanya mitihani ambayo iko chini ya Chuo Kikuu cha Zanzibar (*State University of Zanzibar*). Pia na Chuo cha Karume ambapo na wao wana mfumo huo huo. Je, hatuoni hivi sasa kwamba upo umuhimu wa vyuo hivi kuviingiza katika Chuo Kikuu cha Zanzibar ili navyo vikapata kuhuwika na kupata maendeleo ya haraka sana.

Mhe. Naibu Spika, tunayo Bodi ya Mikopo ambayo inashughulika na kuwapa wanafunzi wetu wanaoingia vyuoni mikopo kwa ajili ya kukimu masomo yao. Kwa kweli fedha zinazoingizwa katika idara hii nahisi ni kidogo sana. Kwa mfano, wanafunzi tulikuwa tunao kwa miaka iliyopita karibu 200 au 300, lakini hivi sasa Mhe. Naibu Spika, wanafunzi wameongezeka sana kiasi kwamba wamefika 800.

Lakini ukiangalia kasma iliyotengwa mara hii Mhe. Naibu Spika, imeongezeka chini ya bilioni 1. Sasa kweli tutakuwa na uwezo wa kuwasomesha wanafunzi hawa au wananchi wetu ambao kila leo idadi yao inaongezeka. Jambo la kushangaza zaidi ni kwamba kile kinachotengwa kwa ajili ya kuwalipia wanafunzi hawa hakikamiliki, unajua unaposoma chuoni

mpaka ulipe ndio unapopewa cheti chako au unapoambiwa endelea na muhula wako wa pili au watatu.

Kwa hivyo, fedha ambazo wanapewa zinachelewa kiasi kwamba zinawafanya wanafunzi hawa wawe na ati ati ya kuendelea na masomo yao. Kutokona na hali hiyo naiomba wizara inayohusika kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwa sababu hii ni sehemu maalum ni tofauti na sehemu nyengine wanayoweza kusubiri, kwani tunaowalipa hatuna mamlaka nao wana hiari yao kutuambia endelea na kusoma au nitakufukuza nitakuondoa katika muhula huu. Hivyo, kwa wale ambao wanao wajibu wa kutoa fedha kwa ajili ya bodi hii basi wahakikishe kuwa fedha zile zinatolewa kwa wakati, si hivyo kuna wananchi wetu walioko nje ya nchi hii watakuja kulazimika kwenda kuosha maiti na mengineyo wakati lengo lao kubwa waliloliendea ni la kujifunza na kurudi katika nchi yao.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa katika nchi hii tunao mfumo wa maandalizi katika skuli zetu na tunatakiwa kila skuli tuwe tunacho kitengo hichi. Vile vile tunazo skuli za madarasa na hizi nazo zinatoa elimu hiyo ya maandalizi. Sasa sijui serikali itaona lini kwamba hawa wanaotoa elimu ya maandalizi na hawa wakatambulika rasmi wakaonekana na wao ni sehemu moja ya skuli kiasi kwamba wakapewa mfumo ule wa serikali na kuendelezwa.

Katika utaratibu tulionao leo skuli hizi Mhe. Naibu Spika, zinatoa elimu ya lugha ya Kiarabu ambayo pia kwa hivi sasa darasa la kwanza yataanza kutoa masomo hayo ya lugha ya Kiarabu. Kwa hivyo, kwa nini hawa tusiwawezeshe nao na tukawaona kwamba hii ni skuli yetu na tukawasaidia wale walimu ambao japo posho dogo na baadae watakapokuja kwenye skuli zetu wakawa wako rasmi.

Mhe. Naibu Spika, nafikiri kwa hayo machache naunga mkono.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, nakushukuru kwa kujali muda. Sasa nafasi tunampa Mhe. Asha Abu Haji, baadaye Mhe. Jaku Hashim Ayoub na ajiandae Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na Mhe. Ali Salum Haji.

Mhe. Asha Abu Haji: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema asubuhi hii. Pili napenda kumshukuru Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri pamoja na watendaji wao kwa kuleta bajeti yao na kuijadili.

Mhe. Naibu Spika, pia napenda kuipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuweka Skuli za Wilaya. Lakini jambo la kusikitisha Wilaya ya Kusini hadi leo skuli ile bado haijamaliza na mkandarasi tuliambiwa kwamba

amekimbia, tujue kwamba bado hajatokea mkandarasi mwengine na ikiwa ameshatokea mkandarasi mwengine sijui ni lini skuli ile itamalizika ya wilaya na skuli yenyewe ni Paje Mtule.

Mhe. Naibu Spika, walimu wa skuli za msingi ni walimu, kwa kweli hawa hatuwajali, tena ni walimu ambao wanafanya jitihada kubwa kwa sababu msingi ni wa chini na masomo yote yanaanzia chini na wajuu wanakuwa hawana shida kubwa, lakini walimu wa chini wanakuwa na shida kubwa. Kwa mfano, tukiangalia siku zote walimu wa chini kipato chao ni kidogo na walimu wa juu wanategemea vyeti vyao. Kwa hivyo, naiomba wizara kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba iwaangalie sana walimu hawa wa msingi. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa serikali imelipokea sana suala la kuanzisha Elimu ya Mjumuisho maskulini. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naiomba wizara iliangalie sana suala hili kutokana na vifaa vyao ni ghali sana, basi ni vyema wizara kuwapatia vifaa vya kufundishia, ili waweze kufundisha kwa ufanisi. Mhe. Naibu Spika, walimu wa mjumuisho ni walimu ambao wamechukua mafunzo ambayo ni magumu, kwa mfano kama tunavyowaona mbele hapo kwenye kioo, elimu hii ni ngumu na si rahisi kuijua hivi hivi, yaani wanapata shida sana. Kutokana na hali hiyo Mhe. Naibu Spika, naomba walimu hawa maslahi yao yawe mazuri.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu walimu wa *TC* wamejitolea kuchukua mafunzo kwa muda wa miaka miwili. Sasa naomba kumuuliza Mhe. Waziri kwamba je, walimu hawa vyeti vyao vinatambulika kimaslahi au wamejiongezea elimu tu lakini maslahi ni yale yale. Hivyo, naiomba wizara kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, nipatiwe majibu. Vile vile suala la Maktaba Kuu Pemba bado haijajengwa. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, naiomba wizara suala hili na mimi nilikuwa kwenye kamati tokea mwanzo mpaka tumemaliza juzi na kila tukenda tunaambiwa kuhusu suala hili. Kwa hivyo, tunaiomba wizara kwamba suala hili lichukuliwe kwa haraka sana.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu maktaba ninaiomba wizara kuwa ijenge Maktaba za Wilaya, yaani kila wilaya iweke Maktaba Kuu. Kwa mfano, Wilaya iweke *center* kama vile Wilaya ya Kusini iweke maktaba yake Kitogani ni *Center* kwa Wilaya ya Kusini. Hata hivyo, kuna wafanyakazi ambao wanalalamika kwamba hawapati taaluma kama vile madereva. Kwa hivyo, ninaiomba wizara iwapatie taaluma madereva hawa ili kuwaongezea ujuzi, kwani elimu haina mwisho. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana kwa mchango wako. Sasa tunampa nafasi Mhe. Jaku Hashim Ayoub baadaye Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na Mhe. Ali Salum Haji ajiandae.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kusimama hapa. Nitakuwa ni mwizi wa fadhila kama sikukushukuru wewe ambaye umenipa fursa hii ya kuchangia wizara ambayo ni muhimu, yaani ukiachia Wizara ya Afya basi hii ni wizara ya pili kwa umuhimu wake na yenye matatizo mengi sana wizara hii.

Baada ya hapo nataka niwashukuru sana watendaji wa wizara hii akiwemo Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake wote na mimi nilikuwa mjumbe wa kamati hii Mhe. Naibu Spika. Vile vile niwashukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa ahadi ya Rais wao kwa Skuli ya Kitogani kwamba hivi sasa ahadi hiyo imetimia na wananchi wa Kitogani Mhe. Naibu Waziri wanakushukuru sana kwa ahadi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache nitahitaji maelezo katika sehemu zifuatazo. Kwanza kuhusu kukamilika kwa jengo la Skuli ya Mtule. Mhe. Naibu Spika, ule mzimu umekaa muda mrefu na hivi sasa karibu mwaka watatu au wanne hakuna kinachoendelea. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika atakapokuja Mhe. Waziri atueleze kwamba huyu mkandarasi ni wa aina gani, hata hivyo nyumba ya ndege huwa inajengwa jengo moja moja na kama nyumba sita au saba ingekuwa zimeshamalizika.

Nikiondoka hapo Mhe. Naibu Spika, sasa nije kwenye Skuli ya Mapopwe.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, Waheshimiwa Mawaziri hawasikii, inamia kipaza sauti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, nitahitaji maelezo kuhusu Skuli ya Mtule na huu ni muda mrefu na wala hakuna kinachoendelea mpaka muda huu. Kwa kweli sijui ujenzi huu ni ujenzi wa aina gani kwamba mpaka leo haujakamilika na wala hakuna kinachoendelea na huyo *contractor* sijui amesaini mkataba wa aina gani? Kwa hivyo, hapa nitahitaji maelezo ya kuridhisha na tukizingatia Skuli hiyo ya Mtule iko katika Jimbo la Muyuni.

Pia ninahitaji maelezo kuhusu Skuli ya Mapopwe Pemba Jimbo la Gando kwa Mhe. Said Ali Mbarouk, kwa kweli wanafunzi wana dhiki na shida kubwa sana kuhusu maji, kwa sababu maji wanayotumia pale hayako safi na salama kwa maisha ya wananfunzi wale. Kwa hivyo, hili nalo nitahitaji maelezo

kama kile kisima tayari kimeshatengenezwa au bado na wala hakihitaji bajeti kubwa hivyo karibu shilingi milioni 4,000,000/= mpaka 5,000,000/= na niliwahi kuvuka hapo Mapopwe.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu ajira ya walimu wa *science*. Mhe. Naibu Spika, huu wimbo umekuwa ni wa muda mrefu na tunaupigia kelele lakini naiomba wizara na uzuri Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora nafikiri yupo, kwa bahati mbaya ameshatoka, angalau kwa mwaka huu ajaribu kuajiri walimu 25 na tutaweza kufika kidogo kidogo na mtu hujikuna anapojipata. Mhe. Naibu Spika, nahitaji maelezo hapa kwamba wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora angalau walimu 25 wapatikane.

Nikiondoka hapo naomba niungane na mwenzangu Mhe. Saleh Nassor Juma kuhusu maeneo ya skuli na vyuo vinavyovamiwa hivi sasa. Mhe. Naibu Spika, tunamuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho atueleze ni lini skuli hizo zitapata hati ukizingatia Chuo cha Kiislamu hivi sasa kiko katika hali ya hatari tena ni hali mbaya. Vile vile tukiangalia Chuo cha Nkurumah kwamba maeneo haya yote yanahitaji hati, pia na kwa Pemba. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho kwamba afanye jitihada na wizara hii ilikuwa ikiongozwa na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali alikuwa Mhe. Ramadhan Abdalla Shabani, kutokana na hali hiyo, hivi sasa skuli zote za Unguja na Pemba imefika wakati zipate hati miliki. Kwa maana hiyo, hapo itabidi nije nipate maelezo ya kina.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na kilio kikubwa kuhusu kuajiriwa madereva Chuo cha Ufundi Kengeja. Kwa kweli suala hilo nililipigia kelele muda mrefu hapa na Mhe. Haji Omar Kheir Waziri mwenye dhamana wa Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora aliahidi, sasa kama wizara yenyewe imefuatilia au haikufuatilia basi nitahitaji maelezo.

Jambo la kusikitisha sana Mhe. Naibu Spika, kuhusu Vyuo vya Kiislamu vya Unguja na Pemba tofauti ya fedha zinazotiliwa na ukilinganisha. Kwa mfano, mwaka 2010 Chuo cha Kiislamu Unguja kilipata shilingi milioni 23,000,000/= na Pemba shilingi milioni 24,000,000/= na huko tuachilie mbali Mhe. Naibu Spika. Lakini kilio changu hasa kipo katika Chuo cha Kiislamu cha Micheweni. Mhe. Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa kimepewa shilingi milioni 31,000,000/= katika bajeti hii wakati Chuo cha Kiislamu cha Unguja ni shilingi milioni 57,000,000/=. Kwa hiyo, hapa nitahitaji maelezo ya kuweza kufahamishwa na ukizingatia Chuo cha Kiislamu cha Micheweni

Pemba kina matatizo makubwa sana na wala sioni fedha hizi kwamba zimegaiwa vipi kwamba hii ni haki au vipi.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nizungumzie kuhusu mabadiliko ya teknolojia ya ulimwengu iko haja kwa wafanyakazi wa sekta mbali mbali kupewa fursa ya masomo tofauti ya kazi ili wasirudi nyuma. Mhe. Naibu Spika, hapa nitahitaji maelezo kwamba wizara kwa mwaka 2011/2012/2013 imesomesha madereva kwa Unguja na Pemba wangapi?

Baada ya hayo, sasa naomba nianze mchango wangu kwenye ukurasa wa 74 na hapa kidogo Mhe. Naibu Spika naomba kunukuu.

Ukurasa wa 74 unaeleza hivi:-

> "Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha.
>
> … Aidha, kitengo kimefanya utafiti kupata takwimu za wanafunzi wenye mahitaji mbali mbali ya kielimu, wakiwemo wenye ulemavu, katika skuli 334 za serikali zote 420. Jumla ya wanafunzi 73,241 wamegunduliwa kuwa na mahitaji maalum, miongoni mwao 37,152 wa kike na 36,089 wa kiume".

Mhe. Naibu Spika, idadi hii ni kubwa kwa hivyo tunamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako atupe walimu wenye ujuzi wa kuwafundisha wanafunzi wenye matatizo ya macho wako wangapi na mahitaji yao kwa Unguja na Pemba wangapi. Vile vile watu wenye ulemavu wa kusikia maarufu tunawaita viziwi wako wangapi wenye ujuzi wa kuwafundisha watu namna hii.

Pia nilitembelea Skuli ya Michakaeni kisiwani Pemba. Mhe. Naibu Spika ukifika pale unaweza kukaribia kulia na hali mbaya. Hata hivyo, nataka niombe radhi kwamba kamati hii ambayo imemaliza muda wake iliahidi kulipatia ufumbuzi kuna banda pale la watoto linavuja vibaya na ikifika wakati wa mvua wale watoto hutoka nje wakatafuta pahala wakajificha mvua na tuliahidi kuichangia skuli ile, lakini kwa muda mrefu hatukuwahi kupata mawasiliano.

Kwa hiyo, ninahitaji maelezo kama lile banda bado halijaezekwa na kamati iliyomaliza muda wake iko tayari kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kulimaliza banda la Michakaeni watoto kule wanapata usumbufu sana. Mhe. Naibu Spika, atakapokuja kufanya majumuisho Mhe. Waziri nafikiri azungumze na watendaji kuhusu suala hili la Skuli ya Michakaeni Pemba kama bado lile banda halijaezekwa basi ahadi yetu iko

pale pale ingawa sisi si wajibu wetu, lakini kutokana na ile hali iliopo pale ikabidi sisi tujivute mifuko yetu.

Mhe. Naibu Spika, kuna mwanafunzi Ruwaida mwenye ulemavu wa macho, ilikuwa kitendawili kupokewa Chuo Kikuu Tunguu kutokana na kutokuwepo kwa vifaa. Sasa wizara imejipanga vipi kuangalia suala muhimu kuhusu wagonjwa wa aina hii. Mwanafunzi huyu hivi sasa anachukua *degree* Mhe. Naibu Spika, ni kitendo cha ujasiri kabisa na cha kupigiwa mfano. Kwa hivyo, wizara iangalie walemavu wa aina hii. *(Makofi).*

Baada ya maelezo hayo, Mhe. Naibu Spika sitaunga hoja mkono mpaka nitakapopata maelezo ya kina.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa nafasi tunampa Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na baadaye Mhe. Ali Salum Haji na ajiandae Mhe. Rufai Said Rufai.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia kidogo hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri pamoja na watendaji wake kwa hotuba yao hii walioiwasilisha katika Baraza hili tukufu.

Mhe. Naibu Spika, nianze mchango wangu katika ukurasa wa 32 kwenye kifungu cha 45, ambapo naomba kunukuu kidogo Mhe. Naibu Spika.

> Ukurasa wa 32 kifungu cha 45 kinaeleza hivi:-
>
> > "Kwa mwaka 2012/2013 jumla ya walimu 578 (343 Unguja, 235 Pemba) walioajiriwa …"

Mhe. Naibu Spika, hapa naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa uajiri huo. Hata hivyo, naomba nimueleze Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba wapo walimu ambao wamemaliza mafunzo yao mwaka 2008 hadi hii leo Mhe. Waziri bado hawajaajiriwa na hasa ukiangalia katika skuli zetu kuna upungufu wa walimu. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika naomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho basi atupe jibu.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, pamoja na kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuajiri walimu hao. Lakini niseme kwamba kuna walimu ambao wameanza kusomesha mwaka 1980 na wengine 1990 ambao walimu hawa mishahara yao ni midogo kuliko walimu ambao wameanza kusomesha miaka ya hivi karibuni. Mhe. Waziri hii ni sababu gani inayosababisha kwamba walimu

wale ambao wamesomesha miaka ya nyuma ikawa mishahara yao ni midogo na walimu hawa wa miaka ya hivi sasa ikawa mishahara yao ni mikubwa. Hivyo, Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anisaidie ufafanuzi.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nije katika ukurasa wa 8 kuhusu mpango wa elimu kwenye kifungu cha 13, ambapo naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika.

Ukurasa wa 8 unaeleza hivi:-

> "Skuli zote za Msingi na Sekondari ziweze kufanyiwa kufanyiwa ukaguzi kila mwaka".

Mhe. Naibu Spika, nampongeza Mhe. Waziri kwa kufanya ukaguzi katika maskuli kwa kila mwaka. Pia naomba nimueleze Mhe. Waziri kwamba asifanye ukaguzi kwa kila mwaka isipokuwa afanye ukaguzi kwa wilaya ili waweze kukaguliwa walimu wale na kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Sasa naomba niende kwenye ukurasa wa 27 kuhusu mradi wa uimarishaji wa elimu ya ufundi. Naomba kunukuu kidogo Mhe. Naibu Spika.

Ukurasa wa 27 kifungu cha (i) kinaeleza hivi:-

> (i) "Kuanza ujenzi wa dakhalia mpya wa Skuli ya Sekondari ya Ufundi Kengeja".

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba pamoja na hilo nimpongeze pia Mhe. Waziri kwa kuanza dakhalia hii kwa skuli ile kwa sababu watoto wetu watapata unafuu wa mwendo pamoja na makaazi. Pamoja na hayo Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba na wenzangu wengi wameshasema hapa kwamba skuli ile bado haijapatiwa hati miliki na hili ni jambo muhimu sana Mhe. Waziri, kwa sababu wananchi wengi huyavamia majengo mengi kutokana na kukosa hati miliki za majengo yale. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, suala hili alifanyie umuhimu wa haraka sana.

Mhe. Naibu Spika, kuna deni la nyumba ambazo wanakaa walimu hao, hivyo deni hili nalo pia linaleta usumbufu. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri alikamilishe ili kuwe na unafuu.

Sasa naomba nizungumzie kuhusu elimu ya madrasa ya Vyuo vya *Kur-ani* kwenye ukurasa wa 34 kifungu 52 ambapo naomba kunukuu kidogo Mhe. Naibu Spika.

Ukurasa wa 34 kifungu cha 52 kinaeleza hivi:-

> "Idara inashughulikia jumla ya madrassa na Vyuo vya *Kur-ani* 2,251. Aidha zipo skuli za maandalizi 84, Unguja na Pemba zinazosimamiwa na kuhudumiwa kupitia Kituo cha *Zanzibar Madrasa Resource Centre(ZMRC),…*"

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba katika kitabu chake cha mwaka jana Mhe. Waziri alisema hivyo hivyo, lakini na mwisho alisema kwamba idara haikuwezo kuendesha mafunzo ya ualimu kutokana na ukosefu wa fedha. Je, naomba nimuulize kwamba hivi sasa tayari fedha hizo zimeshapatikana za kuendeshea hayo mafunzo ya walimu. Hata hivyo, niseme kwamba bado kuna matatizo kwa upande wa walimu wa madrassa. Kwanza wana usumbufu wa majengo yao ni mabovu na madrassa pamoja na vifaa vya kufundishia. Pia wana wakati mgumu wa kufundishi Mhe. Waziri kutokana na ufinyu wa maisha na hali duni za walimu hao. Kwa hivyo, inawalazimu kuwakamua wazee wa watoto kwa ajili ya kuendeleza mahitaji yao. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri hili alione kwa walimu hawa wa vyuoni.

Nikiondoka hapo sasa naomba nizungumzie kuhsuu suala la michezo katika skuli. Kwa kweli siku za zamani michezo ilikuwa ni mingi katika skuli na ilikuwa watoto wanapata hata muamko pamoja na kuondoa maradhi. Lakini kwa hivi sasa hali hii ya michezo imepungua Mhe. Waziri ambapo michezo hii hutoa vipaji

Nam104

IMESAHIHISHWA

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: (Anaendelea) imepungua hali hii ya michezo ambayo hutoa vipaji vya wachezaji wetu wanaokwenda wakicheza sehemu za nje, vipaji hivi huanzia maskulini. Namuomba Mhe. Waziri hili nalo pia airudishe michezo ile ili wachezaji wetu waweze kupandisha vipaji vyao zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwa dhati kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya makadirio ya bajeti ya Wizara ya Elimu ya mwaka huu wa 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mhe. Waziri kwa jitihada anazozichukua wakati wa kusimamia Wizara hii ya Elimu katika kutuletea maendeleo kwa wananchi wa nchi hii. Mimi moja kwa moja nitaanza na kuchangia Bodi ya Mikopo kwenye kitabu hichi kwenye ukurasa wa 63. Niipongeze Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa jitihada na namna wanavyoweza kusimamia shughuli zao za utoaji wa mikopo katika taasisi zao. Pongezi zaidi nipeleke kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa namna walivyoweza kuongeza mikopo kwa vijana wetu kutoka wanafunzi 209 mwaka 2011 hadi wanafunzi 881 mwaka 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, hii inaonesha dhahiri kwamba namna gani serikali yetu inavyowajali vijana wake. Ongezeko liliongezeka la wanafunzi karibuni 600 ni ongezeko la kupigiwa mfano. Niiombe serikali bado iendelee kuonesha jitihada katika kuwasaidia wanafunzi hawa.

Mhe. Naibu Spika, nataka nizungumzie Bodi ya Mikopo kwa kina zaidi. Kila mjumbe kajaribu kuichangia bodi hii kwa namna vile anavyoona. Imani yangu mimi panapokuwa pana keki ndogo basi kila mtu keki hii atakuwa ananyang'anyia na anaihitaji. Keki inapokuwa ndogo lawama hazishi, ndio pale unapokuja upendeleo na ubinafsi. Imani yangu mimi kutokana na kwamba hii keki ndogo, niiombe serikali itafute namna au njia mbadala ili keki hii iweze kutosheleza na wanafunzi wetu wapate mikopo kwa wingi zaidi ili kuondosha manung'uniko ya hapa na pale.

Mhe. Naibu Spika, niiombe Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, kwa mujibu wa taratibu na sheria za nchi hii kwamba kuna fungu la wafanyakazi waliomaliza elimu ya juu, hawa wanakuwa wanakatwa makato maalum. Makato haya yameelekezwa katika maeneo mawili, maeneo ya vyuo vya amali na maeneo ya Bodi ya Elimu ya Mkopo wa Juu. Lakini bado upande mmoja umeshaanza kunufaika na fedha hizi, wenzetu wa vyuo vya amali lakini upande wa Bodi ya Mikopo, fedha hizi bado hawajanufaika nazo.

Niiombe serikali tujitahidi kuhakikisha kwamba zile fedha zinazopatikana ili kuweza kuondoa zile kasoro au matatizo ambayo yameweza kuonekana. Tunafahamu serikali ina nia njema lakini jitihada za kupata fedha hizi bado zimekuwa zinasua sua na wahusika wa Bodi ya Mikopo wamekuwa

wanakwenda wakigonga hodi leo na kesho kupata fedha hizi lakini bado mafanikio hayajafanikiwa.

Katika hapo hapo katika Elimu ya Bodi ya Mikopo bado niseme kwamba kuna tatizo ambalo mara nyingi tumekuwa nalipigia kelele, tatizo la kuchukua mikopo katika sehemu mbili. Sheria zinaelekeza vijana wetu bado wamekuwa wana usumbufu wa kuomba mikopo Tanzania Bara na Zanzibar. Suala ambalo linakuwa linaleta tatizo kubwa kwa wale waliokuwa na malengo ya kuomba sehemu moja. Nalo hili niiombe serikali itafute njia nyengine mbadala ambayo tutahisi hii njia inaweza kuliondosha tatizo hili moja kwa moja na kuwasaidia vijana wetu wale wanaoweza kuchukua mikopo katika sehemu moja. Kwani bado tatizo lipo na hili tatizo limekuwa linaleta usumbufu kwa vijana wetu, unamkuta mtu anachukua mkopo Tanzania Bara, anachukua mkopo na Zanzibar. Muda unakuwa mrefu kufuatilia hata ukishakugundua tayari kuna wenzao mikopo ile wamekosa, hili linakuwa ni tatizo.

Hapo katika Bodi ya Mikopo Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka nizungumzie niombe Wizara ya Elimu kutafuta njia ambazo tunaweza na tunahisi zinaweza kumaliza tatizo la namna ya urejeshaji. Kwa mwaka huu kidogo kunaonekana kuna ufadhali lakini bado tatizo hili limekuwa likisumbua Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa wale watu wanaochukua mikopo kwa namna ya urejeshaji. Imani yetu tunaporejesha kwa haraka na wenzetu wengine tunapata wepesi wa kuwarejeshea.

La kumalizia katika eneo hili nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha. Namuona Mhe. Waziri anakuwa anatoka kidogo kwenda shughuli nyengine za kiserikali. Kuna tatizo la kuingiziwa fedha katika Elimu ya Mikopo, tunakuwa tunaomba fedha kwa makisio ya wanafunzi. Wanafunzi wanakuwa wapo vyuoni, tatizo inakuwa ni ucheleweshaji wa fedha. Wakati mwengine inafikia wakati wanafunzi wanakuwa wapo katika hatua ya ku-*graduate* wanazuiliwa ku-*graduate*, kwa sababu malipo hayajafikia. Vile vile wanafunzi wanakuwa wanahitaji vyeti vyao wanashindwa kupewa vyeti kwa sababu pesa bado hazijaingizwa.

Niiombe serikali tujitahidi kuhakikisha yale matarajio ambayo yanakuwa yanapangwa basi yende na wakati ili kuweza kuondosha usumbufu wa vijana wetu ambao waliokuwepo vyuoni katika masuala mazima ya malipo. Nimalizie hapo kama nilivyosema, niwashukuru ndugu zangu wa Bodi ya Mikopo, kuanzia Mkurugenzi pamoja na watendaji wake na naomba wajitahidi katika kutusaidia ili kuweza kuondosha migogoro na wanafunzi wetu.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nataka nichangie ukurasa wa 17. Ukurasa huu umeelezea masuala mazima ya kujenga makuli ya sekondari kupitia serikali yetu, Benki ya Dunia, *BADEA*, nia ni njema na suala hili limeanza kuonesha muelekeo uliokuwa mzuri. Niiombe Wizara ya Elimu kwa dhati kabisa wajaribu kuwa karibu sana na wakandarasi ambayo wamepewa kazi ya kujenga makuli haya. Baadhi ya maskuli ambayo yamo katika hatua za kumalizika, yanaonekana kwamba ubora wake hauna umakini. Hii ni hatari tunajenga majengo lakini baada ya muda mfupi majengo yale tunakwenda kutumia fedha nyengine nyingi za walipa kodi katika kuyafanyia ukarabati. Niiombe sana Wizara ya Elimu kuwa karibu.

Mfano wa hili Mhe. Naibu Spika, nawaomba waende wakaangalie ghorofa ya mwisho ya Kwerekwe 'C', waangalie mazingira na muda wa skuli ambayo imakabidhiwa, kwa kweli hali ya Skuli ya Kwerekwe 'C' hairidhishi inaonekana kwamba haikuwa na ubora unaostahili. Hii pia inajenga hofu katika masuala mazima ya skuli nyengine. Tuwe karibu na wakandarasi kuona kwamba ujenzi unakwenda kwa namna vile tulivyokusudia. Ili ile dhamira na nia ya serikali ya kuondosha matatizo haya isije ikatokea kadhia baada ya muda kuanza tena kutafuta fedha nyengine kutenga fedha kwa ajili ya kuja kufanyia ukarabati katika majengo haya.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo naomba nichangie Idara ya Elimu Mbadala ya Watu Wazima ukurasa wa 44. Kama alivyosema mheshimiwa serikali ina nia njema lakini watu wanasema panapo mafanikio na matatizo hayaachi. Sijui kama Mhe. Waziri au Mhe. Naibu Waziri wamewahi kukitembelea kituo cha Forodhani sijui. Kama wamewahi kukitembelea mimi nimefika kwenye kituo kile karibuni wiki mbili zilizopita nilikwenda kukabidhi ahadi ya Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo seti ya *Computer* katika kituo kile. Hali halisi niliyoikuta pale bado inaonekana kwamba kituo kile kina matatizo makubwa sana na kinahitaji Wizara ya Elimu kuwa karibu nacho sana.

Nimekuta kuna *computer* tatu za mtumba, mazingira yake mabovu. Baada ya kukabidhi nimetembezwa katika maeneo mbali mbali nilifika katika eneo la ushoni, vyarahani vyake havistahiki, idadi ya vyarahani ni kidogo, wanafunzi ni wengi lakini hali ya darasa lenyewe pia halipo katika mazingira mazuri. Pia nilitembelea katika sehemu ya useremala, nimuombe Mhe. Waziri ajaribu kukiangalia chuo kile kwa jicho la huruma sana. Walimu wanajitahidi na vijana wengi wanakwenda katika yale maeneo kuchukua taaluma. Lakini bado inaonekana kwamba kuna ufinyu wa vitendea kazi, vitenda kazi vyao vipo hali duni sana. Kama utakwenda mwenyewe utakiri kwamba hapa kweli kuna tatizo. Nimuombe Mhe. Waziri ajitahidi kuiangalia hiyo sehemu. Naomba akitembelee Chuo cha Elimu Mbadala cha Watu Wazima kituo cha Forodhani. Mazingira sio mazuri na vitendea kazi kama nilivyosema hawana.

Mhe. Naibu Spika, nataka nizungumzie suala zima katika kupatiwa hati miliki. Hili bado ni tatizo. Tatizo ambalo linafikia pahala linarejesha nyuma maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa nini niseme hivyo? Nasema hivyo mimi naitolea mfano Skuli ya Muungano *Primary School* ya Jimbo la Kwahani. Skuli hii imeanza kuombewa hati miliki tangu Mwakilishi aliyepita, amepiga kelele ameandika mabarua, amekwenda ardhi, mpaka Mwenyezi Mungu kajaalia kamaliza muda wake. Mimi mwenyewe nimekwenda Ardhi nikipanda nikishuka, sasa hivi nina mwaka wa pili na nusu, skuli wameandika barua wameomba hati, kila siku ukenda njoo kesho, njoo keshokutwa, ukenda bado.

Tatizo hili litatugharimu katika maeneo mawili. Eneo la kwanza maskuli yanavamiwa na inakuwa skuli mipaka yake inakuwa haielewi kwa sababu hazijapimwa. Eneo la pili skuli zetu zinafanya kujaribu kutafuta wahisani ili watufanyie marekebisho, lakini unashindwa kuwapata wahisani kwa sababu huna *documents* ambazo inaonekana kwamba wewe unamiliki ile skuli yenyewe haina *document* ya umiliki, kwa sababu hazijapimwa.

Mhe. Naibu Spika, huu urasimu umekuwa mkubwa, hili namuomba sana Mhe. Waziri na Waziri mwenzake hebu wanong'one, watakapokuja watueleze tatizo ni nini Mheshimiwa katika suala la upimaji, miaka 13, maombi hayo nayafuatilia bila ya mafanikio. Hili kwa kweli linanisikitisha, nimeshafika mpaka Wizara ya Elimu nijaribu kuulizia nikaambiwa sijui tunakushanya maombi kwa pamoja ili maombi yale yatakapokuwa tayari skuli zipimwe kwa pamoja lakini hebu tuangalie hivi sasa ni muda gani.

Nimuombe sana Waziri wa Elimu najua hili haliko mikononi mwake, liko ndani ya mikono ya Mhe. Waziri wa Ardhi, lakini imani yangu watakapokaa pamoja hebu walifanye hili suala limalizike ili tuweze kutatua matatizo ya skuli zetu katika masuala ya kuvamiwa na kuweza kutafuta wafadhili angalau watusaidie katika masuala ya ujenzi wa skuli zetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie hili Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie jawabu la kutosha. Kulikuwa kuna mradi wa kuendeleza walimu wa sayansi na hesabati (*TAP*), mradi huu ulikuwa umeanzishwa tangu mwaka 2005, baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ndugu zetu wa *US Aid* na *Agakhani*. Kinachoonekana hadi sasa bado kuna tatizo la malipo ya mafao kwa wale wakufunzi. Inakadiriwa sio chini ya shilingi milioni ishirini na tatu na laki nne, pesa hizi hazijalipwa katika muda huu. Kama tunavyofahamu hali ya maisha sote tunaijua, watu wamelitumikia taifa, watu wametoa elimu zao lakini bado suala la malipo katika suala lao linasua sua na limekuwa linapigwa dana dana halieleweki lini litakuja.

Mhe. Naibu Spika, imani yangu na ninavyomjua somo yangu Mhe. Ali Juma Shamuhuna inawezekana hili labda alikuwa hajalipata vizuri. Basi naomba atakapokuja aje na jawabu la kutueleza kwamba ni lini yale mafao kama bado yangalipo hayajamalizwa basi hawa ndugu zetu wanaweza kupatiwa malipo yao ili na wao waweze kukidhi maisha yao ambayo kila mtu anayaelewa kwamba yanaukwaza na kila mtu anakwenda mbio.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo nasema kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani, mimi sina tatizo na naunga mkono hoja hii. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja basi anisaidie kuweza kupata majibu sahihi ambayo yataondosha au yataleta matumaini katika mchango wangu ambao nimechangia. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Rufai Said Rufai: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii na mimi kuweza kutoa mchango wangu japo kuwa ni mdogo kutokana na hali yangu ilivyo. Awali ya yote kwanza nimshukuru Allah (SW) kwa uwezo wake kutujaalia tukiwa wazima wa afya na leo tukaweza kukutana hapa na kuweza kutoa michangio yetu katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nitoe shukurani zangu za dhati kwa Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia Idara yake ya Sera, Mipango na Utafiti, kuweza kuandaa mipango ya maendeleo kuratibu na kufuatilia raslimali na misaada mbali mbali ya wahisani. Kuna mashirika, mabenki, nchi mbali mbali na hasa ndugu zetu wa *SIDA* kwa jitihada zao kubwa walizozifanya katika Wizara hii ya Elimu.

Shukurani nyingi ziwafikie kwa umahiri na moyo wa kujitolea hasa kwa Wizara yetu ya Elimu. Misaada hii ni vyema tuiheshimu na tuzitunze fedha hizi baadhi yake sisi wananchi ndio tunaolipa kodi na zile nyengine ni misaada, lakini baadhi ya fedha hizi tutakaozirejesha ni sisi na kizazi chetu kijacho. Wenzetu walituonesha moyo wa kutusaidia basi na sisi tuwe na moyo wa kuvienzi vile ambavyo wametusaidia. Juzi tu hapa Waziri ametangaza kwamba kuna karibuni skuli 10 anataka kuzisajili nazo zinahitaji kupata vifaa mbali mbali. Kama ni hivyo basi hawa walioanza kutusaidia tuoneshe moyo wa kuvienzi na kuvitunza ili haya maskuli mengine yanayokuja na yaliyopo basi wawe na moyo wa kuweza kutusaidia zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nikiacha shukurani zangu hizo nije katika ukurasa wa 35 *paragraph* ya 54, Elimu ya Maandalizi. Katika elimu hiyo nimekusudia kuyazungumzia kidogo haya madarasa ya maandalizi ya vituo vya Tucheze na Tujifunze umaarufu wake unaitwa *TUT*. Ama neno hili la tujifunze na

tucheze, kwa kweli watoto wetu wanajisikia vizuri, wanacheza, lakini neno tujifunze baadhi ya vituo hivi wamekosa mafunzo.

Mimi kwa upande wangu naona kwamba Wizara imechangia kukosa haya mafunzo ya watoto wetu. Moja wizara hawakuyashughulikia baadhi ya maeneo, hasa nikiangalia kwa Pemba nzima mafunzo haya yapo Wilayani Micheweni tu. Lakini watoto hawa hawana mwahala mwa kusomea wapo chini ya miti ni hasara tupu kwa kweli na hawa walimu wanaotoa mafunzo haya ushughulikiaji wao ni mbovu sana inafika miezi sita hawajapata maposho yao. Kama mtu utakuwa humshughulikii kimaposho na hii kazi itakuwa ni nzito kwake, kitakachoendelea hapo ni watoto kucheza na kuumizana.

Wizara naona hapa imetwambia kwamba kiwango kimeongezeka sana cha hizi Skuli zetu za Kucheza na Tujifunze, lakini zinavunja moyo kwa walimu wanaoshughulikia watoto hawa. Ni vyema wizara ikaacha uvivu wake wakawashughulikia hawa vijana ili waweze kuliendeleza hili suala. Mtoto anapopata maandalizi pale anapofika darasa la kwanza anakuwa ni mtoto mwenye muelekeo. Kama wizara itaendeleao kutokuwathamini hawa walimu wanaotoa mafunzo ni kweli hawa watoto watacheza, kujifunza kutakuwa kupo mbali.

Mhe. Naibu Spika, wanalalamika sana walimu wa vijana hawa kwamba hawana posho wanalolipata kwa muda mrefu. Wizara ijitahidi kuwaona, kwani wizara imekubali hili liwepo na liendelee. Wakati tumeshawaweka watu ni vyema kuwashughulikia na kuwajali katika maslahi yao ijapokuwa ni machache. Wengi wao ni watu wenye familia ni watu wenye wazee, ni watu wenye kuhitaji huduma mbali mbali za kuogo na kuosha. Kama itakuwa hawapati posho la aina yoyote kwa kweli kutakuwa hakuna kujifunza bali kutakuwa kuna hilo moja tu la kucheza.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo nije katika ukurasa wa 36 hadi 41 *paragraph* ya 57 Elimu ya Msingi. Elimu hii ndiyo elimu ya mwanzo kwa kumuandaa kijana ili aweze kupambana na masomo ya sekondari kama msingi utakuwa mbovu basi tunatarajia matokeo yaliyokuwa sio mazuri kwa vijana wetu. Hapa walimu wetu wa msingi wanajitahidi sana kuwaandaa vijana ili wanapofika sekondari wawe walimu wa sekondari, kazi yao ni ndogo mno. Hata ukiangalia matokeo ya *form II* yanakuwa mazuri na wanafunzi wetu wengi wanapasi. Lakini sielewi kuna mpango gani, wizara huwa inaweka kima gani cha kuwapasisha wanafunzi lakini tunashuhudia katika vyombo vya habari matangazo ya vijana wetu yanakuwa ni mengi na kila skuli inatoa wanafunzi wengi. Tatizo ni sekondari.

Mhe. Naibu Spika, wanafunzi wengi wanapofika sekondari hasa mtihani wa *form IV* ama hapa vijana wetu wengi wanafeli masomo yao. Baadhi ya skuli nyengine hata vile vyeti havipatikani. Huwa sisi tunajiuliza ni wanafunzi au ni hawa walimu, kwa sababu haiwezekani kwamba mtoto alipotoka msingi ameandaliwa vya kutosha lakini anapofika sekondari elimu ile inakuwa ni *loose* kabisa, vijana wetu wanafeli. Ni kipi kinachosababisha hili ni walimu au ni wanafunzi wenyewe. Hapo kwa kweli wazee tunavunjika moyo kuona kwamba vijana wetu hawawezi kusonga mbele katika masomo ya sekondari. Hili ni tatizo na mwaka huu tumeshuhudia kwamba wanafunzi wengi sana wamefeli mpaka mitihani imekwenda kupitiwa kwa mara ya pili na juu ya hivyo pia ikawa suluhisho la wanafunzi bado ni dogo la kupasi kwao. Sasa tatizo ni nini Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, na huu mpango tuliouandaa wa malipo ya walimu, nikwambie kwamba walimu wengi wa msingi wamevunjika moyo kwa kutokujaliwa mishahara yao na maposho yao. Nataka nimwambie tu Mhe. Waziri ajiandae kupokea walimu kustaafu kwao, walimu wengi wamevunjika moyo na wengi wametaka kustaafu kabla ya wakati wao wa kustaafu. Ukiangalia hivi sasa Wizara ya Elimu ina mapungufu makubwa ya walimu na walimu kuvunjika kwao moyo wameona bora kustaafu kuliko kuendelea kufundisha, jambo ambalo maslahi kwao yamekuwa ni madogo mno.

Mhe. Waziri nakuomba sana yajali mishahara ya walimu hawa wa msingi, hawa ndio walimu wanaowaandaa vijana. Sasa mwalimu huyu ndio msingi kama hukumjali nadhani kama hatokuwa na moyo wa kufundisha basi itakuwa ni kazi kuanza walimu wa sekondari. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri itabidi wizara yako ikae chini ijali sana maslahi ya walimu hawa wa msingi, utakapomuandaa kijana vizuri kwenye msingi basi ndio unaanza hisia mwalimu wa sekondari unapofika mtihani wa darasa la kumi na mbili aweze kutoa vijana wetu kwa wingi.

Mhe. Naibu Spika, nikija hapa katika majengo ni kweli kwamba Wizara ina maeneo mengi, maskuli mengi yanahitaji kuezekwa, mabanda yanahitaji kukarabatiwa. Lakini pia katika maeneo yangu ya Jimbo la Tumbe nina skuli nyingi zinahitaji kuezekwa karibuni zote, lakini japo nisipate zote, japo skuli mbili au tatu lakini ni vyema kipaumbele ikapewa skuli yetu ya Shumba Viamboni. Hili banda limekuwa la muda mrefu halijapata kuezekwa na wanafunzi ni wengi mno. Angalau mara hii naiomba sana Wizara jengo hili walitilie maanani ili na wale watoto wetu waweze kusoma na kuingia madarasani ili mwalimu apate nafasi ya kufundisha wanafunzi wachache kuliko msongamano wa wanafunzi wengi.

Mhe. Naibu Spika, mwaka jana nilipochangia Wizara hii ya Elimu nilitoa agizo langu moja la skuli ya Sizini, kuna Mwalimu Mkuu pale kastaafu tokea mwaka 2012. Mwalimu aliyeshikilia nafasi ile hadi leo anakaimu, huu ni mwaka wa pili Wizara imeshindwa kutuletea mwalimu pale. Kwa hivyo sijui sheria inasemaje lakini nakumbuka sheria nyingi zinasema kukaimu ni miezi sita. Lakini hadi leo mwalimu huyu anakaimu, kuna tatizo gani? Naomba nijuilishwe hili tatizo linalosababisha hadi leo tukawa hatujawekewa Mwalimu Mkuu pale akajijua kwamba yeye ndiye mwalimu Mkuu.

Ningeiomba sana Wizara tubadilike na tuache haya mambo ya kizamani tuliyokuwa nayo ya kuangaliana, haya hayatufikishi pahali. Awekwe mwalimu awe ana sifa ya kuwa Mwalimu Mkuu Msaidizi, urasimu huu hautotufikisha pahali. Tukiangalia skuli zetu nyingi za Pemba pana urasimu sana wa Walimu Wakuu na Walimu Wasaidizi. Leo unamuweka Mwalimu Mkuu elimu yake ya kidatu cha tatu lakini pana walimu pale wana *Diploma*, pana walimu wana Vyuo Vikuu, sijui atawaongoza vipi walimu hawa. Haya mambo ya urasimu nadhani hayatufikishi mahali pazuri ni bora tumuweke mtu ambaye ana sifa, uwezo, kuliko kumuweka mtu kumuangalia ana msimamo gani. Hili halijengi na ndio tukakuta kila siku elimu yetu inazidi kushuka. Nitaliomba sana hilo lakini pia naiomba kwamba hii skuli iweze kupatiwa Mwalimu Mkuu ili wajue kwamba mwalimu wetu ni huyu aweze kupambana na majukumu ya ile skuli.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kwa kumalizia pia skuli zilizojengewa za Wilaya na nyengine za maeneo mbali mbali za majimbo kwa bahati katika jimbo langu la Tumbe nimebahatika kuna skuli inayoitwa Skuli ya Chwaka/Tumbe. Naipongeza sana Wizara kwa kuwezesha kuwa na jengo hili. Lakini pia tuone kwamba yale makusudio kwamba hii skuli iwe ya Wilaya kwa mwaka huu haikuwa hivyo bali zimevunjwa baadhi ya skuli na kujalizwa skuli ile. Hapa naomba kujua hii Skuli ya Wilaya ya Chakwa/Tumbe itaanza lini. Naomba Mhe. Waziri utakapokuja aje unambie.

Mhe. Naibu Spika, hizi skuli tunazozivunja tukaweka ile ili tufanye kuwa skuli pale tumeongeza usumbufu wa walimu katika hizi skuli nyengine. Kwa hivyo tuna tatizo kubwa la walimu na hasa hii skuli ya Chwaka/Tumbe kuna baadhi ya masomo hayana mwalimu hata mmoja. Kwa hivyo wanafunzi hawafaidiki na masomo haya na ni wanafunzi wa darasa la 9, 10, 11 na 12 ambao wengine wanatarajiwa kufanya mitihani kipindi hichi tulichonacho. Lakini hapana mwalimu wa *biology* haisomwi hiyo, hapana mwalimu wa hesabu wala *physics*. Sasa kama masomo haya hayana walimu vipi tutaweza kuzalisha walimu wa sayansi, hili ni tatizo.

Kuna baadhi ya walimu wanasomesha skuli mbali mbali halafu wanapata muda siku nyengine kuja kusomesha na skuli hiyo. Niliomba sana wizara ilione hili kwamba ile skuli wanafunzi wametoka katika skuli zao, baadhi ya skuli nyengine wamebakishwa huko huko lakini wengine wameletwa pale Tumbe. Kama yatakosekana masomo haya basi ni kuirudisha nyuma ile skuli na wazee wataona kwamba hakuna haja ya kuwapeleka watoto wao Skuli ya Chwaka/Tumbe. Jengine, kubwa lililokuwepo pale skuli, ile skuli ni mpya lakini hivi sasa inavuja, mabanda yote yanavuja, ni tatizo sijui usimamizi ulikuaje na baadhi mmetiwa viraka lakini bado skuli inavuja na nadhani Mhe. Waziri, hukwenda ukaikagua hii skuli, lakini tatizo hili kwa nini liwepo. Halafu pia vifaa havijakamilika, tunashukuru kwamba sehemu ya maabara vinavyohitajiwa vyote tayari, kuna mambo madogo tu Mhe. Naibu Spika, na Mhe. Waziri hebu yakamilisheni mambo madogo tu ya viti na meza, lakini viti vya maabara tayari vipo tatizo ni namna ya kuviweka tu basi. Halafu na hizi nyumba, tunazo nyumba pale za walimu.

Mhe. Naibu Spika, juzi tu tulipata walimu kutoka Dodoma walikuja kutoa mafunzo pale, lakini kuna kitanda kipo lakini godoro hapana, kwa hiyo ikawa ni tatizo. Tunaomba matatizo kama haya mengine madogo Wizara ijikaze ili kuweza kulimaliza hili suala.

Kwa kumalizia Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba naunga mkono hoja na pia Mungu ajaalie Wizara hii iweze kufanikishwa kwa sababu ndio uti wa mgongo wa vijana wetu.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi kwa kunipatia nafasi hii niweze kutoa mchango mdogo katika Wizara hii. Kwanza kabisa napenda na mimi nichukue fursa ya kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote ambao kwa kweli wanajitahidi na hasa ukizingatia wizara hii, mimi nasema ni wizara mama kwa sababu hii ndio kiwanda ambacho kinazalisha wataalamu wa kila aina. Kwa hivyo Wizara hii inastahiki kupongezwa na mimi nichukue fursa hii ya kuwapongeza walimu wote ambao wamesomesha wataalamu mbali mbali na inshallah Mwenyezi Mungu atawalipa kheria za dunia na kesho yaumul kiyama.

Mhe. Naibu Spika, na mimi nianze mchango wangu katika ukurasa wa 35 ambapo hapa kunaonesha kuna elimu ya maandalizi. Wenzangu wengi wemesema lakini na mimi naendeleo kusema juu ya hili.

Mhe. Naibu Spika, elimu ya maandalizi kama tunavyojua ni muhimu sana na elimu hii kwa kweli walimu wanaosomesha elimu ya maandalizi na elimu ya msingi nachanganya pamoja hapo hapo, maana ukitoka maandalizi unaingia msingi. Walimu wanaosomesha kwa ukweli elimu ya maandalizi ya msingi ni

walimu ambao wana kazi moja kubwa sana na ngumu sana, kwa sababu wanawasomesha vipofu, viziwi kwa sababu mtoto ambaye hajajua lolote maana yake ni sawa tu na kipofu na kiziwi, kwa sababu haoni wala hajui lile analolitenda. Sasa mwalimu ana kazi ya kumrekebisha mpaka aweze kupata mtu ambaye ataweza kusoma, ataweza kuona na ataweza kusikia. Kwa hivyo Mhe. Waziri nikuombe sana kwa kweli tuyajali maslahi ya walimu hawa ambao wana kazi moja ngumu ya kuwasomesha mabubu, vipofu, viziwi kwa sababu mtoto akiwa mdogo anakuwa haelewi chochote. Ni kweli maslahi yao tuyajali ili tuweze kufidia zile kazi zao ngumu wanazozifanya.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia hawa walimu wa maandalizi ambao wanasoma pale Saateni, wengi bado wapo hawajaajiriwa na hawa naomba tuweze kuwafikiria kuwaajiri ili hayo maandalizi yaweze kuwa mazuri.

Mhe. Naibu Spika, niendelee na mchango wangu katika ukurasa wa 51. Mhe. Naibu Spika, hapa kuna Ofisi ya Mkaguzi wa Elimu. Mimi nimuombe sana Mhe. Waziri au nimshauri kwa kweli tukitaka ufanisi wa elimu basi wakaguzi hawa mimi naona watokane na ngazi ya Wilaya kwa sababu ukaguzi ambao unafanywa hivi sasa unachukua muda mrefu bila ya skuli hizo kukaguliwa, majukumu yanawazidi yanakuwa ni mengi lakini laiti tungelikuwa tumeweka wakaguzi wa Wilaya ingekuwa wako karibu na maskuli ya Wilaya zao, basi wangeweza kuzipitia skuli hizi mara kwa mara. Tunaelewa Mhe. Waziri kama ikiwa skuli hazina ukaguzi mzuri basi hata na ufanyaji wa kazi unakuwa hauko vizuri kwa sababu walimu wanakuwa wako *free* wanajifanyia kazi zao wanavyoweza kwa kuwa wanakuwa hakuna kizuizi ambacho kinawaangalia wao mara kwa mara angalau kujenga hofu.

Mhe. Naibu Spika, pia nitoe ushauri wangu katika maafisa hawa wa elimu. Maafisa wa Elimu mimi niombe waweko wa ngazi ya msingi na ngazi ya sekondari, kwa sababu majukumu tunayajua yanakuwa yako mengi sana. Kwa hivyo ili kupata ufanisi mzuri basi hawa tungewaweka maafisa wakawa wapo katika skuli za msingi na za sekondari.

Mhe. Naibu Spika, pia niiombe sana Wizara kuviangalia vituo vya walimu kuvipatia bajeti kwa sababu wana kazi ngumu za kuwasaidia walimu, lakini wanaviendesha katika mazingira magumu sana. Nakuomba sana Mhe. Waziri, hili ulijue wanafanya kazi kubwa lakini hawana uwezo wa kuweza kuzifanya kazi hizo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile niiombe sana Wizara pamoja na jitihada kubwa ya kuwaajiri tumeona uajiri umefanyika lakini pia nakuomba kuweza kuwazingatia walimu ambao wamesoma kwa muda mrefu sana. Tuna walimu ambao wamesoma tangu 2007 na mpaka hii leo wakawa hawajaajiriwa. Mhe.

Naibu Spika, hili ni tatizo kwa sababu mwalimu ambaye kasomea tangu mwaka 2007 mpaka leo hiyo elimu yake itakuwa iko wapi, tutakuwa tumemdumaza kwa kiasi fulani, kwa sababu hicho alichokisoma atakuwa na yeye kishakisahau, raha ya kusoma ukimaliza kusoma lile ulilosoma maana yake ulifanyie kazi. Naomba sana Mhe. Waziri katika uajiri wako unapoajiri basi uwazingatie na walimu hawa ili waweze kumalizika waweze kupata ajira na waifanyie kazi ile elimu ambayo wameipata.

Mhe. Naibu Spika, niende na mchango wangu katika Baraza hili la Mitihani la Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, Baraza lina jukumu la kutathmini mwenendo mzima wa malengo ya utoaji wa elimu pamoja na kutathmini mwenendo wa mitihani. Mimi nasema kwa kuwa hili jambo lipo la kutathmini na tukiangalia elimu inashuka kiwango siku hadi siku kwa ufaulu wa watoto, watoto wanafeli sana, labda niulize Wizara imepanga mikakati gani juu ya kuona jambo hili linapungua au linamalizika kabisa watoto wetu waweze kufanya vizuri, kwa sababu inaumiza mtoto amesoma miaka yote hiyo lakini matokeo yake anafeli na anavunjika moyo.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 78 ambapo kuna kitengo pale cha michezo. Kwanza kabisa nachukua fursa hii kuipongeza sana Wizara kwa kuliona hili la kurejesha michezo katika maskuli, kwa sababu tunasema sasa ajira ziko katika sehemu nyingi wengine wanapata ajira kupitia njia za michezo. Kwa hivyo itakuwa ni jambo muhimu sana kulirejesha maskulini, lakini pia linarejesha uchangamfu wa wanafunzi wanajengeka kiafya. Lakini mimi hapa niongezee neno moja ili pia nalo lirejeshwe katika maskuli.

Mhe. Naibu Spika, gwaride mimi naomba lirudishe kufundishwa katika maskuli kwa sababu kwanza linaleta ukakamavu kwa wanafunzi, lakini pia wanafunzi wale wanapotoka pale wanabahatika pengine kuajiriwa katika Jeshi, Polisi, Vikosi vyetu hivi vya SMZ, kwa hivyo inakuwa tayari tumepata njia rahisi ya kumjenga mwanafunzi anaondoka na uwelewa tangu yuko skuli. Kwa sababu nasema hili kwa mfano hai. Wanafunzi wa miaka hii ambao hawakuwahi kucheza magwaride maskulini anapoajiriwa anapopata kwenda hata katika mafunzo ya pale JKU tu unapomfikisha basi inakuwa ni mtihani mkubwa kwake, haelewi kushoto, kulia kabisa inakuwa ni tatizo. Sasa tukimuandaa tangu pale maana yake itakuwa tushamuweka jeshi mzuri tayari, tumeshamuweka askari mzuri ambaye ataondoka pale analielewa sana gwaride na huko atakwenda kujifunza mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, pia nilitaka nielezee hawa walimu wa maandalizi wa tucheze tujifunze. Hawa walimu mimi ningeiombaWizara pale inapotokea nafasi basi katika walimu wa maandalizi hawa wawaajiri, kwa sababu wameshatumia muda wao mwingi kuwafunza hawa watoto. Sasa lakini

utakuta bado wapo nje wamekaa hawana kazi yoyote, mimi naomba na wao hawa wanajenga taifa tuwafikirie kuwaajiri zinapotokea nafasi.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 54 kwenye mafunzo ya amali. Tunaipongeza serikali kwa kuweka vyuo hivi vya amali ambavyo vinawasaidia wanafunzi baada ya kumaliza masomo yao na wakakosa kuendelea wakarudi wakaja kufanya kazi ambazo zitawasaidia katika maisha yao. Lakini wanafunzi hawa mimi nianze na wale wa Mkokotoni ambao hata siku ya ufunguzi wao wa chuo nilibahatika nikawepo, wanafunzi hawa waliahidiwa kupatiwa fedha za kuanzia maisha watakapotoka pale watapatiwa mikopo ili waweze kuwaendesha kupunguza umasikili, lakini mpaka muda huu inaonekana maandalizi haya hayajawa tayari labda Mhe. Waziri utakapokuja uje unieleze ni lini wanafunzi hawa watawezа kupatiwa fedha zile ili ziweze kuwaendesha. Lakini pia mimi niiombe Serikali kwa sababu hawa ndio wanafunzi wa mwanzo wanaotoka lakini hapo 2014 tutawatoa wengine ni vizuri maandalizi yao yakaweko mapema ili inapofika basi wasiwe wanasumbuka huku na huko. Lakini pia wanafunzi hawa waliomaliza vyeti vyao bado hawajapa ni lini pia watapata vyeti vyao ili waweze kushughulika na mambo mengine ya kutafuta ajira sehemu nyengine.

Mhe. Naibu Spika, pia niende katika elimu hii ya watu wazima nayo ni muhimu mtu kujua kusoma na kuandika. Mheshimiwa idadi inaonekana hapa lakini mimi sidhani kama elimu hii kweli ipo kivitendo, mimi naomba sana Mhe. Waziri uweze kufanya ziara na kuyatafuta hasa haya madarasa ya elimu ya watu wazima. Inaonekana pengine unapewa idadi lakini hayo madarasa ukiyataka pengine hayako vizuri. Mimi naomba sana kwa sababu elimu ingeweza kuwasaidia wale ambao hawajui kusoma na kuandika na wakaweza kufikia mahala pazuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu ulikuwa ni mdogo na namuomba sana Mhe. Waziri aweze kunipatia ufafanuzi kwa yale ambayo nimeyachangia na baada ya hapo naunga mkono hotuba hii kwa asilimia 100. Ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia uhai na uzima na kutupa tawfiki ya kuendelea na saumu ya mwezi mtukufu wa Ramadhan. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na wewe kwa kunipa na mimi nafasi kuchangia bajeti hii ya Wizara muhimu sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Spika, niruhusu vile vile nimpongeze Mhe. Waziri wa Elimu, Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na watendaji wao wote ambao wengi wao huko juu ni walimu wangu. Nadhani ni fahari kwao na ndio faida ya elimu katika nchi kwamba wanafunzi wao tuko katika chombo hiki tukifanya kazi ya

kusimamia maslahi ya nchi yetu na watu wake. Mhe. Naibu Spika, kutokana na wingi wa hoja nilizokuwa nazo naomba nianze kusema kwamba nitaugawa mchango wangu katika sehemu mbili.

Sehemu ya kwanza ilikuwa inahusu vifungu mbali mbali vya matumizi ambavyo hivi tayari kutokutoa usumbufu na kutokupoteza muda nilivyowasilisha tangu jana kwa Mhe. Waziri, ili atakapokuja kufanya majumuisho anisaidie maelezo yake. Kwa hivyo sitovigusa nategemea vimefika pale. Sehemu nyengine Mhe. Naibu Spika, naomba niulize maswali mafupi yafuatayo nipate maelezo halafu baadae ndio nijikite hasa katika maudhui ya mchango wangu.

Mhe. Naibu Spika, la kwanza sote tunajua kwamba matokeo ya mitihani hasa kidato cha nne yamekuwa hayaridhishi na kwa sababu masuala haya nayasimamiwa kwa pamoja na Jamhuri ya Muungano, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano aliunda kamati kufanya uchunguzi na katika Baraza hili alitokea mjumbe mmoja ambaye aliteuliwa kushiriki. Nilikuwa naomba Waziri atakapokuja hapa atusaidie kutwambia kwamba je, sisi kama Wawakilishi wa wananchi ambao tunahusika na kuisimamia serikali kwa upande wa Zanzibar, lini tutapata fursa ya kujua kilichomo katika ripoti hiyo na labda kuitolea maoni yetu.

La pili Mhe. Naibu Spika, katika muktadha huo huo wa matokeo mabaya ya mitihani katika kikao kilichopita Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali alituahidi kwamba serikali inafikiria kufanya kongamano maalum kujadili suala hili na baadhi yetu nikiwemo mimi ambaye nilikuwa na nia ya kuleta hoja binafsi kujadili suala lile hapa. Niliondosha nia ile kwa sababu niliona maadam kunafanywa kongamano tutapata nafasi ya kwenda kutoa maoni yetu pale. Nataka kujua suala hili limefikia wapi.

La tatu Mhe. Naibu Spika, ambalo naomba ufafanuzi niipongeze sana kwanza serikali katika hatua iliyochukua ya kujenga majengo mbali mbali ya skuli hasa za sekondari, yapo majengo ya chini yapo ya ghorofa. Lakini ninashukuru katika jimbo langu la Mji Mkongwe vile vile kwamba kuna skuli ambazo zimefanyiwa matengenezo makubwa. Skuli ya Tumekuja na Skuli ya Forodhani Mhe. Naibu Spika, hapa nilitaka kukumbusha tu kwamba ziko na skuli nyengine za asili ambazo zina historia kubwa katika mfumo wa elimu Zanzibar. Kwa mfano Skuli ya Haile Selassie, Ben Bella, Mkunazini ziko katika hali mbaya sana. Hebu naomba Waziri akija aje anisaidie wana mpango gani kuhusu skuli hizi.

Jengine Mhe, Naibu Spika, kwa haraka vile vile niliuliza suala mwaka jana sikupatiwa jawabu na mwaka huu ninaliuliza tena. Niliuliza katika Skuli ya

Forodhani kuna eneo ambalo limetolewa limegeuzwa hoteli nikataka maelezo hapa mwaka jana sikupewa maelezo mpaka leo, naomba Waziri akija anisaidie maelezo.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka katika jimbo langu kidogo na mimi niisemee Skuli ya Kengeja, sio ile ya ufundi, nilipata nafasi Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwenda kulikagua jumba pale Kengeja la maendeleo. Tukasema kutokana na malalamiko mengi yanayotajwa na wananchi kuhusu Skuli ya Kengeja hebu tukaione, sina haja ya kurudia maelezo Mhe. Hussein jana aliizungumza kwa urefu sana naomba Wizara ilitupie jicho la rehma Skuli ya Kengeja iko katika hali mbaya si pahala pa kusoma watu. Mimi Mhe. Naibu Spika, kwa sababu paliwahi kutokea majibizano hapa nilipiga mpaka picha katika simu yangu akihitaji ushahidi Mheshimiwa nitampatia mimi juu ya hali ilivyo katika sehemu mbali mbali za ile skuli.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, katika masuala haya yaliyotaka maelezo mafupi mafupi tu nizungumzie vile vile suala la Mrajis wa Walimu na suala la kutoa leseni kwa walimu. Kuna malalamiko nimeyapokea na kupewa uthibitisho kwamba wanakwenda kulipia pale leseni lakini hawapewi stakbadhi. Sasa hii ni ofisi ya serikali kwa nini wanachangi na katika buku la mapato inaonekana mapato, lakini hatuwezi kuyajua uhalisia wake kwa sababu hakuna stakbadhi zinazotolewa. Naomba maelezo katika hili.

La mwisho katika ninayoomba Mhe. Naibu Spika, maelezo ni suala la mikopo ya elimu ya juu, huko tunakotoka palikuwa na sera kwamba mikopo hii inatolewa kwa wanafunzi wanaotaka kwenda kusoma shahada ya kwanza. Lakini katika vitabu vya Mhe. Waziri imeonekana humu kuna wanafunzi wa *Diploma*, *Advance Diploma*, kuna wengine wana *PHD* wamepata, sasa nataka kujua hii sera imebadilika kwa sababu kuna wengine wakenda huko na viwango kama hivyo wanaambiwa hawapati mikopo kwa sababu mikopo ni kwa ajili ya shahada ya kwanza lakini bado katika utekelezaji wako waliopewa, kuna nini hapa nilikuwa naomba maelezo katika hili.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maswali hayo mafupi mafupi sasa naomba nijikite hasa katika mchango wangu. Mhe. Naibu Spika, ukitizama kitabu hiki cha Mhe. Waziri kuna picha inajitokeza. Kwanza na mimi niungane na wengine wote waliompongeza yeye na watendaji wake kwamba kitabu hiki kina hotuba fupi lakini kina viambatisho vingi ambavyo vinakupa picha na sura hali ya halisi ilivyo, katika hili ninampongeza sana kwa kazi kubwa ambayo imefanyika.

Mhe. Naibu Spika, tukitazama katika majadweli hali halisi ilivyo ya mfumo wetu wa elimu, kuna mafanikio tunayazungumza kuhusu kuongezeka kwa

idadi na aina ya vituo vya elimu vilivyosajiliwa kuanzia mwaka 2009 mpaka 2013 na hii Mhe. Naibu Spika, unaipata katika jadweli ya kwanza. Zilikuwa 624 mwaka 2009 sasa imefikia 774. Jadweli namba 2(b) Mhe. Naibu Spika, inazungumza ukuaji wa uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi mbali mbali, utaona kutoka mwaka 2009 walikuwa ni 329732, sasa wamefika 363537 hii ni katika viwango mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, hiyo ni sura moja ambayo inaonekana. Kwa hivyo katika kuonekana majengo na aina ya vituo vya elimu tumepiga hatua katika kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga katika vyuo mbali mbali, tumepiga hatua. Lakini Mhe. Naibu Spika, suala la kujiuliza katika ubora wa kiwango cha elimu na mafanikio yenyewe ndio msingi hasa hali ikoje. Mhe. Naibu Spika, tukitizama kwanza nizungumzie matokeo ya kidato cha pili tunaletewa takwimu ambazo zinaonesha kwamba tunapiga hatua lakini kuna suala tulilizungumza sana katika Baraza hili Mhe. Naibu Spika, kwamba mpaka leo kuna usiri mkubwa juu ya matokeo ya kidato cha pili, tofauti na matokeo ya mitihani mengine ambapo unajua mtu katika somo hili, mimi nimepata kiwango kadha, matokeo ya kidato cha pili tunatangaziwa tu kwamba hawa wamefaulu wameingia katika kidato cha tatu. Lini Wizara ya Elimu itaanzisha utaratibu wa kujua kwamba wanafunzi wanaofanya mitihani wajijue walipasi na kwa kiwango gani katika kila somo? Hiki ni kitu kizuri cha kuweza kupima Mhe. Naibu Spika, lakini matokeo ya kidato cha nne hali inatisha. Mhe. Naibu Spika, ukichukua takwimu zilizomo kwenye jadweli namba 66 111 iko katika ukurasa wa 96 asilimia utaona ilikuwa imekaa vizuri lakini sasa inaporomoka iko katika ukurasa wa 96. Utakuta mwaka 2008 waliopasi na hawa wanajumuishwa mpaka waliopata *division 1V* kiwango cha nne cha kufaulu ni asilimia 77.4 2009 ni asilimia 81.0 2010 ni asilimi 71.7 2011 asilimia 75.9 lakini 2012 ni asilimia 53.1, hii ni picha inayotisha Mhe. Naibu Spika.

Lakini twende kidato cha sita. Mhe. Naibu Spika, tukenda kidato cha sita utakuta vile vile kwamba kidogo hali inaridhisha lakini mimi naomba kiambatisho ambacho kipo ukurasa 99 ukitizama utagundua kwamba wakati picha ya jumla inaonekana kama vile imepanda, tumefikia asilimi 79.1 lakini tuangalie viwango vya kufaulu, *division one* tumetoka mwaka 2008 zilikuwa 39 mwaka 2009, 2010 zikawa 41 mwaka 2010, 2011 zilikuwa 24 na mwaka 2011/2012 17 mwaka 2012/13 *division one* kwa Zanzibar nzima Mhe. Naibu Spika.

Sasa Mhe. Naibu Spika, hii ni picha halisi ya kazi hii kubwa inayofanyika lakini mwaka jana nilisema na mwaka huu narejea kusema kiwango cha kufaulu hasa kama tunataka tukitazame kinapaswa kile ambacho kinamuwezesha mwanafunzi kutoka hatua moja kwenda hatua ya pili.

Umepata *division four* wewe huendelei umepasi nini Mhe. Naibu Spika, una cheti lakini tunamuhesabu huyu pia kafaulu anakwenda kukaa barazani hana la kufanya. Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi nimefanya hesabu ya haraka haraka, nimefanya haya kwa nia njema kabisa kwa sababu nataka kuonesha hali halisi.

Ukichukua kidato cha nne Mhe. Naibu Spika, ukichanganya *division zero* ambazo kwenye kitabu cha Mhe. Waziri hazioneshwi lakini ukifanya hesabu utapata kujua, *division four* na *division zero* na ukizichanganya utapata una asilimia 47.3 na asilimia 46.1, jumla utakuta kwa mwaka 2012 asilimia 93.4 ndio waliopata *division zero* na *division* hawa hawendi mbele Mhe. Naibu Spika, tunawahesabu wamefaulu hawa.

Chukua kidato cha sita Mhe. Naibu Spika, *division zero* kwa kufanya hesabu hapa kwa mwaka 2012/2013 ni kama asilimia 20.9. *Division four* ni asilimia 22.8 ukijumlisha jumla ni asilimia 43.7 hawa hawasongi mbele lakini kwa matokeo tuliyoyafuatilia sisi kwa mwaka huu hata hao waliopata *division three* Mhe. Naibu Spika, ambao ni asilimia 54.4 wengi wao alama zao ni za chini sana ambazo zinawapa ugumu sana kupata nafasi ya kuendelea mbele. Kama na wao tunawajumlisha katika kundi lile Mhe. Naibu Spika, ukiichanganya na ile 43.7 na hii 54.4 ya *division three* utakuja kugundua una asilimia 98.1 waliopata *division three, four* na *ziro* na kama nilivyosema katika hii *three* wengi wameshindwa kupata viwango vya kuendelea mbele. Kwa hivyo waliopata *division one* na *two* ni asilimia 1.9, hiyo ndio hali halisi ya elimu katika nchi yetu Mhe. Naibu Spika.

Kwa hivyo tunapotangaza mafanikio tusifiche uhalisia huu wa takwimu. Mhe. Naibu Spika, nimefanya hesabu hizi kama nilivyosema kwa nia njema kabisa ya kuionesha hali halisi ilivyo katika mfumo wetu wa elimu.

Mhe. Naibu Spika, haraka haraka naomba pia tupate picha halisi tuangalie wanafunzi wa faragha wanaitwa *private candidate* wanaofanya mitihani kwa kujisomesha wenyewe. Ukitizama ukurasa wa 101 matokeo ya *form four* kwa wanafunzi wa faragha mwaka 2008/2012, 2008 walikuwa asilimia 48.4, 2009 walikuwa 53.0, 2010, walikuwa asilimia 48.1, 2011 asilimia 63.9, 2012 Mhe. Naibu Spika, asilimia 17.0. Na kiwango cha kufaulu hapa kinahesabika hata umepata *division four* bado ni asilimia 17 na ukenda kwa *form V1* hali ni hivyo hivyo unakipata kiambatanisho katika ukurasa 103, 2008/2009 waliopasi walikuwa asilimia 75.02, 2009/2010 asilimia 62.09 mwaka 2010/2011 asilimia 53.78, 2011/2012, asilimia 30.31, 2012/2013, asimilia 32.62. Mhe. Naibu Spika, hii picha inatisha sana.

Sasa Mhe. Naibu Spika, tujiulize tatizo liko wapi, kwa maana ya bajeti, ukitizama kuanzia 2010 mpaka mwaka huu 2013/2014, bajeti ya Wizara ya Elimu imeongezeka. Kwa hakika ukichukua 2010 mpaka mwaka huu imeongezeka maradufu ilikuwa kwenye milioni 40 na ushei mwaka huu Mhe. Naibu Spika, bajeti ya Wizara ya Elimu ni bilioni mia moja kumi tano, mia saba arubaini na saba milioni, laki sita kumi na tisa elfu. Katika bajeti ya serikali ya jumla ya kama bilioni mia sita na hamsini, bilioni mia moja kumi na tano zinakwenda katika elimu. Sasa kwa nini tunapata matokeo mabaya Mhe. Naibu Spika? Haya masuala lazima tujiulize.

Mhe. Naibu Spika, mimi kuna mambo nimeyaorodhesha nilikuwa nadhani yanapaswa tuyatizame. Kwanza Mhe. Naibu Spika, kuna suala la kutazama huu mfumo wetu mzima wa elimu wote. Mimi nadhani ikiwa hali ndio hii ninayoionesha hapa kwa vitabu vyao wenyewe vya Wizara ya Elimu, picha inayopatikana ni kwamba maamuzi, sera zetu, utekelezaji wetu si sahihi. Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi nimeona mambo yafuatayo:

Mhe. Naibu Spika, kwanza nadhani kuna udhaifu wa mfumo rasmi wa elimu unaotokana na sera, mitaala na muhtasari ya elimu yetu. Pili kuna kupitwa na wakati kwa sera yenyewe ya elimu na si vyenginevyo, mitaala yetu na muhtasari yote mingi imetungwa tangu zama za ukoloni tunabadilisha kidogo kidogo bado tunashindwa kabisa kuakisi mahitaji yetu ya sasa. Lakini hata vitabu vyetu vinavyotumika Mhe. Naibu Spika, vingi vimeshapitwa na wakati, katika skuli za msingi na skuli za sekondari. Tatu kuna kukosekana hata kwa mitaala rasmi ya kitaifa katika skuli za msingi na sekondari. Mhe. Naibu Spika, kila skuli inaonekana sasa hivi kila moja inafanya kivyake na skuli za *private* ndio kabisa kila moja inafanya vyake. Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, la nne mihutasari iliyopo maana kuna mitaala mbali halafu mitaala imetafsiriwa katika muhtasari, lakini muhtasari iliyokuwemo mingi ipo kwa mazoea tu na uwepo wake na mfumo wa elimu umekuwa hauna malengo yanayoeleweka vyema, kwa hivyo matokeo yake tunakosa viwango vya kitaalamu vinavyotegemewa.

Mhe. Naibu Spika, la tano ni kwamba tuna uzoefu mkubwa katika vitabu vyetu vya kusomeshea hivyo wanavyoviita vitabu vya kiada na vitabu vya ziada. Kwanza kuna mfumo mbaya sana katika kuvitafuta na kuviidhinisha. Mimi nataka Mhe. Waziri aje aangalie sana Taasisi ya Elimu katika kupasisha vitabu hivi, upande wa wenzetu, Tanganyika kumeonekana kuna madudu mengi sana katika mfumo wa kuidhinisha vitabu, mimi nina hakika hali kama hii inaweza kuwepo Zanzibar kama tutafanya utafiti wa kina.

Mhe. Naibu Spika, hayo ni kwa upande wa mitaala lakini huwezi kuimarisha mfumo wa elimu kama hujawatazama walimu. Ukiangalia katika mafunzo

wanayopata wengi tumeambiwa hapa muda mrefu hawajaendelezwa lakini maslahi yao Mhe. Naibu Spika, mwaka jana niliyasema na sitaki kuyarejea hapa. Leo Mhe. Naibu Spika, Mwalimu Mkuu unayempa dhamana ya kusimamia skuli yote unampa posho la shs.12,000/=, hivyo kweli unategemea huyu atakuwa na moyo na ari ya kujituma asimamie elimu ya watoto wetu. Mazingira ya kazi Mhe. Naibu Spika, yanatisha sana hali ya skuli zetu tunazijua zilivyo. Nimezungumza kuhusu mitaala na mihutasari lakini kumezungumzwa na wengi humu sitaki kurejea suala zima la maadili na nidhamu ya wanafunzi wetu, kuanzia wanafunzi mpaka walimu tumekosa kuyasimamia.

Mhe. Naibu Spika, leo tunazungumzia adhabu mbadala katika kitabu hichi na jana kazungumza Mhe. Abdalla Juma, mimi naunga mkono hoja ile kwamba tunapochukua haya mambo mengine tunayoletewa na Wazungu huko kwao, sasa hivi wanafanya mapitio kwamba baada ya kuyatumia wameona yamewarejesha nyuma. Kwa hivyo leo wanatazama vipi kuondosha adhabu kwa mfano ya mikwaju, skuli imepelekea kuteremka kwa nidhamu, sisi tumeletewa tunachukua tu, haya tunapaswa kuyatizame. Vifaa kuanzia vya maabara vya sayansi, madeski, tunazungumzia elimu ya teknohama, kuwepo kwa kompyuta katika maskuli, halafu kuna suala zima la uwiano wa mwalimu na mwanafunzi. Humu ukitizama muhtasari unasema walimu tulionao wamegaiwa kwa idadi yote ya wanafunzi, tunasema mwalimu mmoja kwa wanafunzi 26 lakini darasani unakuta *ratio* au uwiano unapitiliza kama alivyozungumza jana Mhe. Hussein hapa kuna wanafunzi mara nyengine 100 katika darasa, tunategemea tutakuwa na elimu gani. Kwa kifupi haya ni mambo mengi ambayo yanahitaji kutazamwa.

Mhe. Naibu Spika, nimeyasema haya kwa sababu kwa sababu kama haturekebishi haya tutaendelea kuwa na viwango vidogo vya elimu, tutazalisha watendaji wabovu Serikalini, tutajenga jamii ambayo haina maadili, jamii ambayo haifuati sheria kwa sababu walivyolelewa katika msingi hawakuwa na msingi wowote.

Mhe. Naibu Spika, suala langu la mwisho. Nimezungumzia masuala ambayo yanatuhusu sisi ndani lakini hatuwezi kuzungumza mfumo wa elimu na hali hii bila ya kuzungumzia suala la muungano hasa katika Baraza la Mitihani Mhe. Naibu Spika, ndio suala langu la mwisho hilo.

Mhe. Naibu Spika, ninao ushahidi hapa mwaka juzi wazee hapa walipiga kelele sana kuhusu matokeo ya mitihani, mwaka jana wamepiga kelele sana. Mhe. Naibu Spika, sasa kuna ushahidi kwamba kuna hali ya kuchakachua matokeo ya mitihani, ushahidi huu hapa nnao Mhe. Naibu Spika. Hali hii haipo kwa Zanzibar tu, mfano hai nilionao ni Baraza la Wakuu wa Skuli za

Kiislamu Tanzania, Mwenyekiti wa Baraza anajiita Mwalimu Khamis Togwa, aliandika barua kwa Waziri Mkuu ninayo hapa, kulalamikia kuhusu matokeo hasa ya somo la Dini na Kiarabu na matokeo yake ikapelekea kuundwa kamati. Muhtasari na mapendekezo yake ninayo hapa, sina muda Mhe. Naibu Spika, kuyasoma lakini kilichogundulikana ni nini. Kuna mambo yanafanyika katika Baraza la Mitihani la Taifa, kwanza tumezoea tulikotoka kote kwamba viwango vya kupasisha na viwango vya kufeli vinakuwa sawa sawa. Mhe. Naibu Spika, sote tulipotoka skuli ukipewa cheti chako kinaonesha kwamba alama 70-100 ni A, alama 50-60 huo ni ninatoa mifano tu, lakini leo kwa mujibu wa ushahidi huu kwamba kila somo limepangiwa viwango vyake halafu somo hilo hilo kila mwaka viwango vinabadilishwa vya kupasi. Kuna watu wanajipa mamlaka ya kuamua nani anapasi na nani hapasi kwa utaratibu huu.

Mhe. Naibu Spika, katika hali hii tunategemea mfumo huu utatupasishia watoto wetu kwa kutegemea kiwango hichi cha elimu hata siku moja. Hapa nataka maelezo katika hili, nilisema pale mwanzo paliundwa Kamati, sisi Baraza la Wawakilishi hatujaambiwa, kamati ile iliyoundwa na Waziri Mkuu ambayo Zanzibar imeshirikishwa kwa sababu sisi inatuhusu tumeona nini na tutachukua hatua gani.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo niseme kwamba tulipitisha sheria hapa ya kuunda Baraza la Mitihani Zanzibar, ikawa maneno mengi sana lakini leo katika rasimu ya haya ya kuwa na Baraza la Mitihani tunahitaji kwa madudu haya tunahitaji kujiandaa Zanzibar. Niiombe Wizara ya Elimu ijipange vizuri kwa sababu Baraza la Mitihani tuliwapitishia hapa itafutwe njia itakapokuja kukabidhiwa mamlaka haya vipi tutaweza kuyatumia vizuri kusimamia mitihani ya viwango vyote vya kidato cha nne, kidato cha sita na kuendelea.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo nataka kusema wala sina ya kuzuia bajeti hii mimi kwa hakika nawaonea huruma Mhe. Waziri na Naibu Waziri na walimu wangu watendaji waliokuweko juu huko kwa hali waliyokuwa wanayo, lakini ningeomba kuja kupata ufafanuzi kwa zile hoja ambazo nimezitoa na Serikali kwa ujumla kuangalia kama ilivyopendekeza suala zima la mfumo wetu wa elimu namna tunavyouwendesha na jinsi baadae itatuletea jamii ambayo haiwezi kabisa kuaminiwa kaleta maendeleo katika nchi hii.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza kabla ya yote na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha leo kufika katika Ramadhani hii ya nane, Mungu atusaidie inshallah. Lakini pia nichukue nafasi hii Mhe. Naibu Spika, kukushukuru wewe kunipatia nafasi hii, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikumpongeza

Waziri pamoja na Naibu Waziri na Watendaji wake wote ambao walishirikiana kwa pamoja ili kuandaa kitabu hichi ambacho ni kitabu chenye mambo yote, imejionesha moja baada ya moja na ni mambo ambayo kwa kweli ukiyaangalia, isipokuwa kuna dosari ambazo mwenzangu aliyekaa kitako sasa hivi ameyazungumza.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu watu wengi wameshazungumza mambo mbali mbali, mimi niko katika maslahi ya walimu. Mhe. Naibu Spika, maslahi ya walimu kwa kweli ni jambo kubwa sana hasa kwa mtiririko huu ambao tunakwenda nao hivi sasa, kwa sababu mwalimu huyu ambaye saa nyengine amepelekwa skuli mbali na nyumbani, mbali na makaazi yake, mbali na taratibu zote ambazo zinaweza zikamsaidia mwalimu huyu kujiona kwamba yuko huru na anaweza kutumia akili yake kuwafundisha wale wanafunzi ambao anatarajia kwamba wafunzwe. Sasa mimi nizungumze la maslahi Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, unajua serikali yetu pamoja na matatizo madogo madogo lakini kwa kweli ni vyema ikakaa tena upya kuangalia maslahi ya walimu, naomba sana Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Naibu Waziri kwamba maslahi ya walimu kwa kweli, kwa sababu miongoni mwa watu wanaofanya kazi ngumu kwenye mazingira magumu ni walimu, lakini niunganishe hapo hapo kwa nini nikasema mazingira magumu, kwa sababu hizo enzi zetu sisi walimu walikuwa na nyumba, wanaishi karibu na skuli. Lakini leo kuna matatizo mwalimu anatoka Mkoa wa Mjini/ Magharibi anakwenda kufundisha Mkwajuni au anakwenda kufundisha Mfenesini, ni saa ngapi atatoka kwake mwalimu huyu, ni saa ngapi atakaa a-*prepare* mambo yake na kurudi na kuhakikisha kwamba anafika kwa wakati. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, naomba kupitia Serikali kila pahala ambapo pana skuli na walimu basi paweko na nyumba za walimu ili walimu hawa wajisikie na wao, lakini matatizo yanayojitokeza ni kwamba tunaanzisha kitu halafu tunakisahau njiani. Ninamuomba sana Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, sasa nakuja katika suala jengine. Kuna wanafunzi ambao wamemaliza na wanakaa katika shehia zao, wanafunzi hawa bado hawajapatiwa ajira lakini wanaona kwamba ni vyema kujitolea katika kijiji chao kama pana skuli karibu wanajitolea kusomesha. Matokeo yake Mhe. Naibu Spika, wanafunzi hawa tena wana vyeti vyao vizuri wakiomba kazi kama alivyosema Mheshimiwa wa Kojani hapa hawapatiwi wanachukuliwa watu ambao hata waliokuwa wanaranda tu hawajitolei katika kusomesha. Mimi naiomba Wizara ya Elimu kwa kweli watu wanaokaa wakajitolea kuona kwamba wasaidie pale wanapoishi kwao kuwasaidia wenzao kama

walivyosaidiwa wao, naomba Wizara ya Elimu ichukulie suala la kuajiri hawa vijana wetu. Naomba sana Mhe. Waziri na Naibu Waziri watakapokuja hapa na wakitaka ushahidi mimi ninao, wanieleze ni sababu zipi za watoto wetu ambao wanajitolea katika Shehia hawalipwi mishahara lakini wakiomba kuajiriwa hawaajiriwi, ni sababu zipi. Hilo ni moja.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije katika likizo la walimu na wenzangu wamelizungumzia sana. Mtu anapokwenda likizo na hasa mwalimu maana yake mwalimu ana shida katika darasa, mwalimu ana-*deal* na wanafunzi wake, mwalimu ana-*deal* na wazee pia maana na sisi wazee wakati mwengine tunawageukia walimu utafikiri hatuhitaji kitu kwao, ana shida akitaka kupumzika. Mhe. Naibu Spika, mwalimu anachukua likizo wanaambiwa wakae sijui baada ya miezi mingapi maana yake hata sielewi. Mimi naomba Mhe. Waziri aje anielimishe vizuri hapa kama unawapa walimu likizo hawana pesa za likizo kwa nini usiwaombee mapema ukahakikisha kwamba katika walimu wangu 1,000 ambao wanakwenda likizo, safari hii nitawapatia pesa zao za likizo walimu 200, lakini mwalimu anakwenda likizo akirudi hana chochote anaambiwa angojee.

Mhe. Naibu Spika, sasa niunge mkono suala la wanafunzi kuanzishwa kuwa na gwaride. Kwa nini nikaunga mkono hilo, ni kwa sababu kwanza kutakuwa na nidhamu. Sisi enzi zetu tulikuwa na nidhamu za hali ya juu na mpaka leo mimi pamoja na uheshimiwa wangu nikiona huyu mwalimu kaingiza mkono wako kunisomesha basi hata nikawa niko wapi lazima nisimame kama ana mzigo nimpokee niuchukue, najua kwamba mimi miongoni mwa mtu aliyenifanya nifike hapa katika Baraza la Wawakilishi na yeye ni mmoja. Lakini leo hakuna nidhamu ya wanafunzi wetu Mhe. Naibu Spika, naomba mambo ya nidhamu yarejeshwe, zitafutwe sera ambazo zinaweza zikamsaidia mwanafunzi kuhakikisha kwamba mimi sijakuwa mkubwa kuliko mwalimu, lakini leo skuli mwanafunzi anafika hadi kumpiga mwalimu, unafikiri mwanafunzi huyo kweli atakuwa mwanafunzi bora, apate madigrii na madiploma hawi hata siku moja, mwalimu ni sawa sawa na mama na baba.

Mhe. Naibu Spika, nieleze na mimi na niunge mkono maneno aliyoyazungumza Mhe. Jussa, kwa kweli mfumo wa elimu unataka uangaliwe upya. Tulivyosoma sisi ni tofauti na sasa. Sasa hivi tumeongeza maskuli kwa wingi, tuna vyuo, tuna sekondari nyingi lakini zamani watu wakitoka shambani wakija skuli ya Utaani, watu wakitoka Konde wakija Skuli ya Utaani ndio Sekondari kubwa tena ina *boarding*. Leo ni tofauti Mhe. Naibu Spika, mimi naiomba Wizara ya Elimu kwa sababu wao ndio wanaozaa wataalamu watafute wataalamu wa kuhakikisha kwamba sera zinaangaliwa upya na mfumo wote wa Wizara ya Elimu unaangaliwa upya. Tunajitahidi kufungua maskuli, tunajitahidi kufungua masekondari, kufungua vyuo lakini

vijana wetu bado hawajafika kiwango kinachotakiwa. Kwa hivyo tuna jukumu kwa Mwenyezi Mungu.

Mhe. Naibu Spika, tusijaribu tu kupeleka peleka taaluma ni kitu muhimu katika dunia na sisi ndio iliyotusaidia be, te, che, ikatufikisha hapa leo. Kwa hivyo kwa kweli tuhakikishe na watoto wetu ambao wale wengine wanakusudia kusoma. Mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, kama hatukubadilisha mfumo tutakosa vijana wetu wa sayansi, tutakosa kweli kwa sababu hawa walimu hatuwaangalii vizuri na kuna haja walimu wa sayansi kuangaliwa vizuri. Mimi vile vile nitoe wito kwa vijana ambao sasa hivi wawe na hamu ya kusoma masomo ya sayansi na sisi angalau tubadilike, bila ya sayansi na teknolojia Mhe. Naibu Spika, huwezi ukabadilika, tutabakia hapa hapa, tutafungua vyuo, sekondari, tufanyaje lakini kwa kweli kama hatukujikaza, tujikaze vipi na hizo zana za sayansi ziko maskulini? Hamna. Naomba Wizara ya Elimu kile kitu ambacho tunakihitaji kwa nguvu zote basi na tukitilie mkazo Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba mimi nitaiunga mkono hoja hii nitapopata maelezo ambayo yataniridhisha hasa kubadilisha mfumo mzima wa elimu. Pili sera ziangaliwe upya. Sera ya mwaka 1957, nilivyokuwa mimi skuli si sera kwa sababu sisi tulikuwa kidogo, sasa hivi kila sehemu ina wanafunzi tunashindwa hata kuwadhibiti, tuende kwa mfumo ambao tulionao hivi sasa, wakati huu wa sayansi na teknolojia.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba sina dhamira ya kuzuia lakini nipate maelezo mazuri, nikishakupata maelezo mazuri ya kuniridhisha basi hapo naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kutoa mchango wangu mdogo katika kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, hotuba inayohusu Makadirio na Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2013/14. Kwanza niipongeze Wizara kwa kupitia watendaji wake kwa kazi kubwa waliyoichukua na umakini katika hotuba ya kitabu hichi cha bajeti na chenye majadweli ya kutosha kinachofahamika na kilichosheheni kila jambo kiasi ambacho mtu akikisoma vilivyo ataridhika kuwa kweli Wizara ya Elimu inafanyakazi katika kujua mambo yake katika uhalisi ulivyo.

Pia naomba kuchukua nafasi hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Wizara ya Elimu kwa kusaini hati ya maelewano baina ya Wizara ya Elimu ya Juu ya Falme ya Oman, juu ya ushirikiano katika ngazi ya elimu ya juu, kupitia maelewano hayo Serikali ya Falme ya Oman imewezesha mpango wa kugharamia masomo ya juu wanafunzi wetu kwa kupitia Chuo Kikuu cha

Taifa cha Zanzibar, mpango ambao unaitwa *Sultan Qaboos Academi for SUZA*. Baada ya kutoa pongezi zangu hizo naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, elimu ni moja kati ya jambo la lazima ambalo ni lazima binadamu awe nalo. Elimu imegawika mafungu makubwa mawili, kuna elimu ya kurithi ambayo hapa hatuizungumzi na tuna elimu hii inayopangwa makusudi ili binadamu awe nayo kuanzia tokea udogo wake na kuendelea. Hii elimu ya kupanga ina maandalizi makubwa sana na hadhari kubwa ili elimu hii iweze kupatikana katika hali inayohitajika. Kwanza hatuwezi kabisa tukamfanya mtoto akaelimika ikiwa hatakuwa na mazingira mazuri ya mahala ya kupatiwa ile elimu yenyewe, uwe na majengo mazuri, vikalio, madaftari, vitabu vya kusomea, vitabu vya kusomeshea, maabara kwa wale wanaochukua sayansi, halafu maktaba na mengi mengineyo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kunahitajika watu wa kutoa mafunzo na hawa ni walimu wenye ujuzi wa kutosha wa kazi wanayoifanya ambao wanapata malipo mazuri na wanafanya kazi ikiwa wanapata huduma zote. Na si hivyo tu tunatakiwa tuwe na mitaala ambayo itakuwa ni mitaala inayofundishika kutoka katika sehemu moja kwenda sehemu nyengine katika maeneo kadhaa ya elimu hii. Sasa Mhe. Naibu Spika, ukiangalia hali halisi hasa ilivyo kwa hapa Zanzibar katika tendo zima la kutoa elimu, kuanzia *primary* mpaka *secondary* ni hali mbaya sana. Kuna majengo mengi tu yamejengwa na wananchi lakini yanasomewa hayakukamilishwa, kuna wanafunzi wanasoma mpaka darasa la 12 lakini hawana maabara katika skuli zao. Halafu mitihani wanayoifanya ni ya *practical* na kwa sababu ya kuwa mipango yetu si mizuri kama inavyohitajika na matokeo yetu siku zote yanakuwa ni mabaya sana, na kubwa kabisa na walimu nao kupata malipo kidogo kiasi ambacho baada ya kufanya kazi hawana muda wa kukaa na kushughulikia masomo ya baadae na badala yake huwa wanawajibika kutafuta maisha.

Mhe. Naibu Spika, kwa maana hiyo Wizara hii ina kazi kubwa ya kujiimarisha ili iweze kuingia katika mkumbo wa elimu kama unavyohitajika na kwa sababu ya kutokuwa katika hali hii ndio sababu watoto wetu wanafeli vibaya sana sana kwa walimu kushindwa kufundisha ipasavyo na vile vile kwa ukosefu wa mambo chungu mzima kama nilivyotangulia kuzungumza. Nitatoa mfano Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, nikiangalia ukurasa wa 7 wa kitabu chetu hapa pana kitu kinaitwa mpango kazi wa elimu. Hapa kwenye mpango kazi wa elimu ukiangalia utaona pameelezwa kuwa Wizara imeandaa mpango kazi wa maendeleo ya elimu kwa kipindi cha miaka 4 ya mwisho, yaani kuanzia mwaka 2012/13 ambao ndio huu hadi mwaka 2015/16 na nasema kuwa

mpango kazi huo umezingatia dira ya maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2020, vile vile awamu ya pili ya Mkakati wa *MKUZA*, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini yaani *Mkuza II* na mwisho ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 hadi 1015. Kitabu kimeeleza katika kutumia mikakati hiyo mpango kazi huo utatoa muongozo wa njia ya kufikiwa kwa malengo ya elimu kwa wote na malengo ya milennia kwa upande wa elimu ifikapo mwaka 2015. Shabaha za mpango kazi huo ifikapo mwaka 2016 ni kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kuwa ifikapo wakati huo asilimia ya wanafunzi wanaofanya mtihani wa kidato cha II na kufaulu na kuchaguliwa kuendelea na masomo ya kidato cha III ifikie asilimia 70 na vile vile pia hoja ya asilimia 50 za wanafunzi wote watakaoandikishwa kufanya mtihani wa kuingia kidato cha tatu waweze kufaulu katika masomo ya kiingereza, hisabati, *biology*, kemia pamoja na fizikia. Sasa ikiendelea inasema kuwa asilimia ya wanafunzi wa kidato cha nne wanaofaulu na kupata sifa za kuendelea na masomo ya kuingia kidato cha tano iongezeke hadi kufikia asilimia 20 ya wanafunzi.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa hawasikii wenzio kipaza sauti umekiacha mbali sana, hebu kisogelee usiiogope.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naendelea. Asilimia ya wanafunzi wa kidato cha nne wanaofaulu na kupata sifa za kuendelea na masomo ya kuingia kidato cha tano iongezeke hadi kufikia asilimia 20 ya wanafunzi wote walioandikishwa kufanya mtihani.

Sasa Mhe. Naibu Spika, haya ndio malengo ya mpango kazi wa elimu lakini tukiangalia ukurasa wa 94 mpaka 96 wa kitabu hiki Kitabu cha Bajeti cha Wizara ya Elimu kinaonesha matokeo ya wanafunzi wa kidato cha nne kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo, kwa sababu ya wakati nachukua hii ya pamoja yaani ya wavulana na wasichana.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia matokeo waliyofanya mtihani mwaka 2011 walikuwa ni 11,877; waliopata daraja la kwanza ni watoto 60 tu, waliopata daraja la pili ni watoto 107 na waliopata daraja la tatu haijambo kidogo ni watoto 772. Wa daraja la kwanza ni asilimia 0.3, daraja la pili asilimia 1.1 na daraja la tatu ni asilimia 4.3 ambao hawa ndio tunaowatarajia waingie katika darasa la 12 kwa idadi hiyo ya asilimia 20 kama Mhe. Waziri alivyoeleza.

Vile vile tukiangalia matokeo haya niliyoyataja na tukiangalia hali halisi ilivyo ni kuwa watoto wetu wanafeli tena wanafeli sana kupita kiasi. Sasa ningeliomba Mheshimiwa anambie mpango kazi huu wa elimu atatumia ufafanuzi gani au mbinu gani au mwelekeo gani kwa sababu skuli ndio zile

zile, mazingira ndio yale yale, walimu ndio wale wale isipokuwa ni watoto tu wanabadilika wanakuja wengine, ili kiwango hiki kiweze kupanda kwa awamu ya kwanza, ya pili, ya tatu mpaka awamu ya nne tuweze kufikia hilo lengo alilokusudia. Hilo ni moja.

Jengine Mhe. Naibu Spika, katika kitabu hiki cha bajeti kumeelezwa ujenzi wa skuli mpya za sekondari ambazo ni jumla ya skuli 16. Skuli hizo zimetajwa katika ukurasa wa tano kama ifuatavyo:-

Kwanza Mhe. Naibu Spika ni Skuli ya Mwanda, Chaani, Matemwe, Uzini, Dole, Utaani, Ngwachani, Wawi, Kiwani-mauani, Tumbe, Konde, Pandani na Madungu. Hizi ni skuli mpya za sekondari 16 lakini ambazo zimeshakamilika kujengwa ni 13. Wakati Mhe. Naibu Spika, wizara hii imehimiza wazee watumie nguvu zao kama inavyowezekana wajenge mabanda na halafu baada ya kujenga mabanda hayo yaweze kuezekwa, na wakati hivi sasa kuna mabanda chungu nzima hayajaezekwa. Kwa mfano, madarasa yanayofikia hatua ya kutaka kuezekwa yaliyojengwa na wananchi kwa wilaya kumi ni madarasa 230, kuna na afisi 30, ghala 12, kuna na mambo mengine kama maabara, mambo ya kompyuta na kadhalika 23.

Tukiangalia kuna madarasa ambayo yamo katika ujenzi wa ukuta na nguzo yaliyojengwa na wananchi wenyewe kwa Zanzibar nzima ni madarasa 102, afisi 11, ghala 7 na mambo mengineyo ni 7 na yote hii ni nguvu za wananchi na halafu madarasa yaliyo katika hatua ya ukusanyaji wa vifaa haya ni 33, afisi ni sita, ghala ni tano, mengineyo ni nne, ukichukua kwa jumla ni madarasa 465 kama ujenzi utakamilika, afisi 47, ghala 24, mengineyo ni 34 na hizi ni nguvu za wananchi na wizara imeshindwa wala hakuna tamaa ya kuyamaliza madarasa haya watu wakapata kusoma; mpaka leo kuna skuli zinaingia kwa awamu, wanaingia asubuhi na jioni na mabanda yapo yanashindwa kuezekwa na halafu kuna sekondari mpya hizi 12.

Vile vile katika majimbo yetu kwa Zanzibar nzima skuli ambazo zimefika mpaka darasa la 12 watu wanasoma na kwa bahati mbaya kwa kukosekana kwa vifaa ndio tukapata haya matokeo mabaya. Mimi nataka nijue madarasa haya ambayo yatakuwa 16, yashajengwa 13 na yanaanza kazi, yatakuwa na mfumo huu huu wa uendeshaji sawa sawa na madarasa haya ambayo siku zote yanatumika wala hatupati matokeo mazuri au yanapewa vipa umbele maalum na kupata *facility* zote za kufundishia ikiwa ni pamoja na maabara, walimu wazuri, maktaba na kadhalika. Hapa naomba nipate jibu.

Halafu nilitaka kujua hizo skuli tatu za sekondari zilizobakia ambazo hazijajengwa, tuna tamaa zitajengwa wapi na wapi mana nilisikia na Jimbo la Mtambwe kuna moja itajengwa.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna ujenzi wa sekondari za ghorofa sasa na hizi ni Kiembesamaki, Kwamtipura, Mpendae, Kibuteni pamoja na Mkanyageni. Mimi nikitaka kujua vigezo vilivyotumika katika ujenzi wa sekondari hizi za ghorofa Unguja zikaweko nne na Pemba ikaweko moja na ile ya Pemba ikawekwa mwisho wa Pemba kule Mkanyageni, au sijui wanaoingia Baraza la Mapinduzi huko waliomba wakakubaliwa au vipi, nataka nijue.

Nikitoka hapo sasa niingie katika Skuli ya Ndagoni. Mhe. Saleh Nassor Juma alizungumza hapa kwa ukali kwa kutetea watu na haki zao, kule kuna mzee ambaye alimtaja, Mzee Ayoub Suleiman kishakufa maskini, ana shamba lake kubwa, ana waraka kamili na ana warathi na mmoja katika warathi ni Bwana Suleiman Bin Ayoub, shamba lake limechukuliwa na kujengwa skuli na uwanja mkubwa wa mpira. Kwa bahati mbaya wamelalamika mpaka kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais baada ya kupita kwa Afisa Mdhamini wa Wizara ya Elimu kule Pemba, wamekwenda kwa Makamu wa Kwanza wa Rais lakini hakuna lolote linaloendelea wakati hili ni shamba yake mwenyewe ya urathi.

Sasa Mheshimiwa ninalosikitika sana kama ni kweli na nasema makusudi kwa sababu wenyewe wapo, mwalimu mkuu anapolalamikiwa kuhusu suala hili anasema sisi ni kazi yetu kuchukua mashamba ya Warabu mpaka tuyamalize. Hii ni kauli mbaya sana kuisemea serikali kwa sababu serikali hii haidhulumu na kama Mwalimu Mkuu si wa kusema kauli hii. Mimi kwa sababu majengo yaliopo ni Wizara ya Elimu na kuna matatizo kama haya ya kumnyang'anya mtu haki yake, ningeliomba wizara itoe kauli kuhusu sehemu hii.

Halafu jengine tatizo liliopo kila mwaka walimu wetu huchukuliwa kusahihisha mitihani ya darasa la saba, mitihani ya darasa la kumi na kadhalika. Lakini huwa wanacheleweshwa sana kupewa posho lao, nataka niulize hao waliosahihisha hivi karibuni tayari wameshapewa posho lao au bado, kuna sababu gani zinazofanya mtu kupewa kazi halafu tena asipewe malipo yake akachelewa kiasi hicho.

Jengine Mheshimiwa katika miaka hii ya 1990 kwa makusudi kabisa ya kuwaonea huruma wenzetu Mwenyezi Mungu aliowapa ulemavu na wanahitaji elimu. Wizara iliwapeleka walimu kuchukua mafunzo ya mjumuisho wanavyoita wenyewe, katika hii skuli tuliyonayo hapa ya Kiisilamu. Tuna walimu wengi tu na wamepata vyeti na wengine wameshaanza kazi ya kuwasomesha watu hawa wenye ulemavu wa aina kwa aina, yaani ni watu wenye mahitaji maalum. Lakini kwa taarifa nilizonazo ni kuwa bado walimu wale hawajalipwa chochote kutokana na kazi ya ziada

waliyoichukua ambayo ni nzito na ni muhimu sana. Nikitaka kujua Mhe. Waziri ana mpango gani wa kuwapa haki yao hawa kwa sababu ndio wamesoma na vyeti wanavyo. Pia wale ambao tayari wamelipwa kidogo wako wa kupewa *areas* zao za nyuma iliyokuwa haipungui miezi minne.

Tukiendelea Mhe. Naibu Spika, nimeona katika ukurasa wa 78 katika kitabu cha bajeti kuwa kuna kitengo cha michezo na utamaduni. Lakini tunajua kuna Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Swali la mwanzo, kitengo hiki kiliingia ingiaje Wizara ya Elimu ikawa ni kitengo rasmi?
Halafu pili, kwa sababu sikuona katika kitabu kizima namna gani wao wamejipanga katika kuendeleza hii michezo isipokuwa wamesifu tu kwa kupewa mipira 20,000 kwa kuwagawia watoto wa skuli. Hivyo haoni Mhe. Waziri kuwa kuchukua suala hili akaliingiza katika Wizara ya Elimu wakati lilikuwepo na likatolewa likapewa wizara nyengine, ni kubeba kazi iliyokuwa itamshinda na hii Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo sasa ifanye kazi gani, wakati ndio wenye wataalamu wanaohusika na mambo haya.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo napenda kuzungumza ni kuwa kwanza hakuna kitu muhimu kama kuheshimu kauli ya Mhe. Rais, hiki ni kitu muhimu sana. Rais anaposema basi wizara inayohusika ni lazima itekeleze na Rais anapozungumza jambo ikawa serikali kwa kupitia wizara inayohusika haikutekeleza, mimi nasema itakuwa hatumtendei haki Mhe. Rais.

Mhe. Rais katika siku za kampeni alifika katika Jimbo ka Mtambwe akiongozwa na Mhe. Asha Bakari Makame vile vile na Mhe. Haroun Ali Suleiman wakati ule alikuwa ni Waziri wa Elimu, na akaahidi katika Jimbo la Mtambwe kujenga Chuo cha Amali. Na kwa sababu ni kauli ya Mhe. Rais nimpongeze Bi. Asha Bakari Makame kwa kutoa shamba lake ili kujengwa chuo hicho. Lakini baada ya utafiti na kuonekana kidogo ni kando ikabidi nitafute pahala pengine na nilitafuta. Natoa pongezi sana kwa Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban alipokuwa Waziri wa Elimu nilipomueleza hili alichukua hatua ya kumpeleka Naibu Katibu Mkuu wa wizara na tulikwenda pamoja na aliyekuwa mratibu wa elimu kule Pemba tukaenda tukaangalia eneo ambalo linalozungumzwa lina mikarafuu mingi wala ilikuwa halina.

Sasa Mhe. Waziri mimi nataka nijue, hii kauli ya Mhe. Rais ndio imedharauliwa? Kwa sababu tokea alipotoa kauli hii nusu ya kipindi kishapita na hakuna utekelezaji na kile Chuo cha Elimu ya Amali si kwa jimbo la Mtambwe ni kwa Mkoa mzima wa Kaskazini Pemba, lakini mwenyewe kasema kijengwe katika Jimbo la Mtambwe kwa sababu zake. Kwa nini hadi leo hatujaona utekelezaji wowote, ni kwa sababu wizara imeshindwa kupata fedha hizo au imeona kwa sababu ni Mtambwe leo nizungumze hivyo, ndio ikawa hapafanywi chochote. Nasema tena eneo tulilonalo halina mikarafuu

kama hivyo inavyozungumzwa na Naibu Katibu Mkuu wa wizara yupo namtaka Mhe. Waziri amuulize na atahakikisha kuwa lile eneo liko kweli.

La mwisho Mheshimiwa ninaloomba ni kuwa wizara inapofanya mambo ya kutekeleza ahadi zake iangalie majimbo sawa sawa. Mimi nashukuru katika Jimbo la Mtambwe nina majengo mengi tu mpaka hivi sasa tumejenga wala hayajaezekwa na katika jimbo langu skuli kubwa kuliko zote ni Skuli ya Uondwe na kuna jengo la miaka mingi lakini hata humu kuzungumzwa halikuzungumzwa lolote. Kwa hivyo, Mhe. Waziri namuomba anipe majibu ya kutosha vyenginevyo leo nitakuwa mkali sana. Nashukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyeniwezesha kusimama hapa. Pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Naibu Spika, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa sababu hii ni bajeti ya tatu lakini sijawahi kuona kitabu kikubwa kama hiki chake.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa nianze mchango kwa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote wa Wizara ya Elimu kwa kazi kubwa wanazozifanya. Vile vile nataka kumpongeza kwa mikopo wanayotoa ya elimu ya juu. Mimi nawapongeza sana kwa sababu hapa tulianzia na wanafunzi 200, tukaja wanafunzi 881, na hivi sasa tunatarajia wanafunzi 1000. Hilo ni ongezeko kubwa na wanastahiki kupongezwa.

Lakini hapa namuomba Mhe. Waziri anifahamishe hawa wanafunzi waliyoomba ni wangapi, waliokuwa na sifa, isijekuwa tunajivunia kupata mkopo wa watu 1000 lakini ikawa kuna watu laki moja walioomba. Naomba Mhe. Waziri atakaposimama anifahamishe ni wanafunzi wangapi walioomba na wanaotarajiwa kupata ni hao. Vile vile namuomba anifahamishe zile shilingi bilioni nane zimepatikana kiasi gani, kwa sababu sijaona maelezo yanayoonesha hicho kiasi cha fedha zilizopatikana.

Sasa Mhe. Naibu Spika, nataka nipeleke mchango wangu kwenye likizo la walimu.
Hapa namuomba Mhe. Waziri atakaposimama anieleze hawa walimu wana likizo au wana mapumziko tu kwa sababu Mhe. Naibu Spika, mimi ninavyojua likizo huwa analiomba mfanyakazi pale anapohitajia. Aidha awe ana dharura ya kuumwa, kualisa mzee wake au jambo lolote lile au ana safari hata biashara na hata wakulima wakati mwengine huchukua likizo kwa ajili ya kipindi cha mavuno. Lakini Mhe. Naibu Spika, hawa walimu hulazimishwa wachukue likizo pale zinapofungwa skuli. Mimi hili sioni kama

ni likizo kwa sababu mfanyakazi huomba kwa dharura ni haki yake, lakini mara nyingi huwa wanaliomba pale wanapokuwa na tatizo, leo kumlazimisha mwalimu achukue likizo kipindi kile, ile si likizo.

Halafu pia hata aliyekuwa hayuko kwenye likizo naye yuko kwenye mapumziko. Sasa sijui hapa kuna tofauti gani ya yule aliyekuwa kwenye likizo na wale waliopumzika tu kwa ajili ya kufunga skuli. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anifahamishe hilo na anambie hasa wana mpango gani wa kuwapatia walimu haki yao ya likizo kwa sababu hii ni haki ya kila mfanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, sasa niendelee na mchango wangu kwa kugusia Vyuo Vikuu kidogo. Hapa mimi nina masikitiko makubwa kwa sababu Vyuo Vikuu vyote vimejengwa upande mmoja. Kule Pemba Mhe. Naibu Spika, hakuna chuo kikuu hata kimoja na wananchi wa Pemba wengi tunajua kama ni maskini, uwezo wao ni mdogo. Kwa hivyo, mtu kutoka Pemba akaja akasoma huku ni gharama. Sasa sijui hapa imejipanga vipi wizara kuwasaidia angalau wale wanafunzi wanaotaka kusoma kutoka Pemba kwa sababu hapana asiyejua hali ya maisha na hali ya Pemba, mara nyingi tunasema kwamba wananchi na hali zao ni duni, kumchukua mtu akatoka kule kuja hapa kumkalia mtu ni tatizo, lakini ingelikuwa kuna vyuo kule kule wangeliweza kukaa majumbani mwao na wakajisomea. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri hapa aniambie wizara yake imekusudia nini au imeandaa mpango gani kwa ajili ya vyuo vikuu kule Pemba.

Suala jengine ambalo naomba nilizungumzie kidogo ni Skuli ya Ole. Mhe. Naibu Spika, mimi ni jirani na Skuli ya Ole, si wilaya yangu lakini ni jirani sana na kijiji ninachoishi na mara nyingi katika pirika zangu huwa napita pale. Mhe. Naibu Spika, skuli hiyo ina jengo moja ambalo ni bovu sana na linahatarisha maisha ya wanafunzi na hata tukisema wanafunzi wazuiwe pale, watoto hawazuiliki, huwezi kusema kwamba ushawaambia kuwa wasiende pale na jengo ni bovu wakasikiliza wasiende.

Hili Mhe. Naibu Spika, wakati alipokwenda Mhe. Rais Afisa Mdhamini alichukua jukumu la kusema atalijenga banda hili na hadi leo halijajengwa hili banda. Sasa namuomba Mhe. Waziri anambie banda hili litajengwa lini?

Suala jengine ambalo nataka nilizungumzie kidogo ni kuhusu walimu wa sayansi. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli walimu wa sayansi ni tatizo na hapa nataka nizungumzie kuhusu Skuli ya Vikunguni ambayo nina kumbukumbu. Bajeti ya mwaka jana niliichangia lakini katika majumuisho Mhe. Waziri alinambia skuli ile sio ya sayansi. Namuomba Mhe. Waziri atakaposimama anambie ni vigezo gani wanavyotumia vya kusema skuli hii ni ya sayansi, hii

sio ya sayansi wakati skuli ile ina wanafunzi kuanzia darasa la kwanza mpaka la 12 na ni wanafunzi wengi wanaotoka vijiji vya karibu wanasoma pale. Sasa hivyo kweli vijana wale wote hawana haki ya kupata hii elimu ya sayansi, ikiwa wana haki na skuli ile inaambiwa sio ya sayansi wende wakapate pahala gani. Namuomba Mhe. Waziri anieleze hili na mimi nilitegemea kuwa elimu hii ya sayansi inaanza toka *primary*, msingi wake hasa unaanza mapema, leo ikiwa pale wanafunzi wanamaliza *Form IV* na serikali kila siku inahimiza watu wasome sayansi sasa pale napata majibu ya kuambiwa sio skuli ya sayansi ile kwa kweli inasikitisha Mhe. Naibu Spika.

Hivi sasa katika skuli ile pana mwalimu mmoja tu wa sayansi na walikuwepo walimu watatu, lakini wawili waliondolewa wakapelekwa Fiedel Castro. Sasa namuomba Mhe. Waziri anambie hapa wale vijana wa pale hawana haki ya kusoma sayansi, nikishapata jawabu nitaridhika ikiwa hawana haki wataamua, aidha wahame kwenye vijiji watafute vijiji vinavyosomeshwa sayansi kwa sababu hivi sasa tunahimizwa kusoma sayansi na tunaona wengi waliosoma *art* wanahangaika kupata ajira. Sasa sijui Mhe. Waziri atanambia nini pale au kakusudia ndio wale walale tu.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo nataka niligusie kidogo ni kuhusu maktaba. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli inasikitisha maktaba iliyoko Pemba nzima maktaba ni moja iliyopo Chake Chake na kwa kweli haifanyi kazi vizuri kwa kuwa haina hata hiyo nafasi. Nimeshawahi kusikia kuwa Wizara ya Elimu ina lengo la kujenga maktaba kule Pemba. Sasa namuomba Mhe. Waziri anambie hii maktaba itajengwa lini. Vile vile skuli nyingi zinafundisha hazina maktaba madhubuti na wala hazina vifaa vya sayansi. Mhe. Naibu Spika, ni tatizo linapelekea wanafunzi kukosa utamaduni wa kujisomea, ikiwa Wizara ya Elimu haitojipanga, haitokuwa na mikakati madhubuti ya kushughulikia matatizo haya basi tutaendelea kutegemea wataalamu kutoka nje, kwa sababu mtu huwezi kumsomesha sayansi lakini hapana vifaa, hivyo kweli mafanikio yatapatikana hapo?

Mhe. Naibu Spika, naomba niendeleze mchango wangu kwa ushauri. Hivi sasa Mhe. Naibu Spika, skuli nyingi zimepatiwa kompyuta lakini skuli hizo hazina walinzi. Sasa namuomba Mhe. Waziri zile skuli zipatiwe walinzi kwa sababu zinaweza kwenda kuibiwa kompyuta zile ikawa serikali haikufanya kitu. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri ushauri wangu zile skuli ambazo tayari wameshazipatiwa kompyuta basi waweke walinzi.

Mhe. Naibu Spika, nadhani mimi kwa leo mchango wangu ni huo na namuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi wa masuala yangu, akishakunipa ufafanuzi basi nitampitishia bajeti yake bila ya wasi wasi, lakini nikiwa sikupata ufafanuzi mzuri Mhe. Naibu Spika, nitazuwia fungu. Nakushukuru.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyetujaalia uhai tukawepo hapa kutekeleza majukumu yetu. Lakini pia nikushukuru na wewe kwa kunipatia nafasi wakati huu kwa kutoa mchango wangu mdogo katika mada iliyopo mezani wakati huu.

Mhe. Naibu Spika, nianze na kumpongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake kwa kutuletea mpango kazi wao kwa mwaka 2013/2014 unaohusiana na mambo ya elimu.

Mhe. Naibu Spika, nianze kusema kwa utangulizi huu ufuatao: Wengi wanasema kwamba elimu ni nuru, elimu ni muangaza, elimu ni ufunguo wa maisha, lakini elimu ni moja katika nyezo za maendeleo ya taifa lolote lile duniani linalohitaji maendeleo ya nchi. Hivyo, kama hayo ni ya ukweli hebu tujitathmini sisi wenyewe na tujiulize katika elimu sisi tumejipangia bajeti ya kiasi gani ambayo itakidhi haja katika mambo ya elimu, tukielewa kwamba katika serikali yetu mambo mbali mbali yanayogusana na shughuli zetu za kimaendeleo na kiutendaji yanahitaji kabisa kuwa na wataalamu na wataalamu hao hawapatikani popote pale isipokuwa mwanzo wake huzalishwa kupitia Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mimi kwa upande wangu ningependa kusema kwamba tujiulize, hivi serikali iliwahi kuchukua utaratibu wa kufanya tafiti kuhusu mpango mzima wa taaluma hii au wa Wizara hii ya Elimu hapa petu Zanzibar tangu mwaka 1964? Kama ilifanyika je, mifumo tuliyonayo sasa inakidhi haja? Mitaala tunayotumia ni sahihi? Mihutasari nayo ndivyo ilivyo? Baada ya kuyasema hayo Mhe. Naibu Spika, sasa nirudi kwenye mchango wangu.

Nianze kwenye ukurasa wa 35 katika kifungu cha 54 kinachosema, "Elimu ya Maandalizi". Niipongeze wizara kwa kuanzisha rasmi utaratibu wa vijana wetu kwa kuanza ngazi za maandalizi, hapa nawapongeza sana. Lakini niwaambie kwamba hapa ndio pahala muhimu sana kabisa kwa kumtayarisha kijana huyu kumbeba katika msingi, silka, utamaduni na mambo kadhaa.

Je, skuli hizi za maandalizi zipo za serikali na za *private*, zile za watu binafsi na za mtaala unaosomeshwa katika skuli zote hizi kama wizara wanausimamiaje, ni utaratibu gani labda akija Mhe. Waziri anieleze wanaofanya katika ukaguzi kuhakikisha kwamba vijana wote wanaopata taaluma hizo kupitia skuli za maandalizi za serikali na za watu binafsi zinafuata utawala mmoja ambao wizara ndio ambao wasimamizi wake.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea katika mchango wangu niende katika ukurasa wa 47 katika kufungu cha 64 ‘Idara ya Mafunzo ya Ualimu’. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli tuna walimu wengi ambao tumewasomesha kupitia hapa serikalini vijana hawa kwa kweli hawajapatiwa ajira na wengine miongoni mwao wana sifa zinazokubalika kabisa. Serikali inambie au iliambie Baraza hili kwa ujumla kuna mpango gani wa makusudi uliochukua kuona walimu hawa walipewa taaluma na mpaka wakati huu bado hawajaajiriwa. Serikali imewaekea utaratibu gani kuona vijana wote nao wanapata ajira lakini pia elimu nayo waliyoipata itatumika kwa utaratibu na kuwapatia wanafunzi wetu ambao ndio kero letu kwamba tuna upungufu wa walimu kadhaa wa kadhaa.

Pili inambie serikali kupitia Wizara ya Utumishi kwamba katika tathmini zetu zote kama nilivyotangulia katika utangulizi wangu wa mwanzo ni kusema kwamba elimu haiwezi kusonga mbele bila ya kwenda na mahitaji ambayo tunayahitaji. Mahitaji ya mwanzo kuwa na walimu, walimu tunao lakini tatizo ni ajira. Serikali itafute utaratibu maalum ijenge mikakati madhubuti kama vile tulivyopangiwa ikawa hatuna meli, baada ya kuzama meli, serikali ikafanya utaratibu na hatimae sasa tunatarajia kupata meli hiyo. Lakini na hili la kuajiri walimu kwa skuli ambazo hazina walimu ni suala la msingi na serikali si la kulifanyia mzaha kwani kama kweli tunataka kupitia maendeleo ya kweli, hili lazima tuweze kulifikiria.

Lakini pia niulize kuwa ina utaratibu gani wa kuwahamisha walimu kutoka skuli nyengine na kuwapeleka skuli nyengine pale ambapo mwalimu mwenyewe husika hakuomba kama mimi naomba uhamisho. Tumezoea kuwaona walimu wanahamishwa kutoka skuli moja na kuwapeleka skuli nyengine hali ya kwamba wao wenyewe bado walikuwa wanataka kubaki katika skuli zile ambazo wanazosomeshea.

Mara nyengine walimu hawa tayari wameshazoeleka na utaratibu wao katika skuli zile ni mzuri na wanafunzi wetu wanafaulu vizuri. Lakini kwa hafla tunaona walimu hao wanapatiwa uhamisho bila ya ridhaa zao au bila ya utaratibu. Naomba Mhe. Waziri ukija hapa kufanya majumuisho hili nalo unipatie. Lakini jengine kuhusu walimu nalo niliweke hapa hapa la kuwapa posho la nauli. Huu ni ukweli usiofichika kwamba bado wapo walimu ambao wanatoka mbali na maeneo ambayo wanafanyia kazi. Lakini walimu hao bado hawajapatiwa nauli na wale ambao wanapatiwa nauli basi haikidhi haja.

Umefika wakati sasa kama ni kweli ni haja yetu kuboresha elimu basi walimu hawa nao sasa waboreshwe ipasavyo wapate posho na kuwakidhi haja. Waswahili wanasema, "Ukimuudhi mchinja mbuzi utakosa mchuzi". Tutaipata taaluma hiyo bila ya kuwatunza walimu hawa, sasa mimi niombe hilo lifanyike walimu hawa wafikiriwe na wapatiwe utaratibu huo.

Lakini jengine ni Ofisi ya Mkaguzi Mkuu hichi ni kilio cha Serikali. Mhe. Waziri ofisi nyengine hazina majengo lakini kwenye Wizara ya Elimu tatizo la majengo kuwa machakavu kwenye Kitengo cha Mkaguzi Mkuu wa Elimu hili lipo. Hali hii haijengi ustawi wa ukaguzi katika elimu yetu kwani hata sehemu anayofanyia kazi ni duni sana.

Tuelewe kwamba historia ilikuwa inatuonesha mimi wakati nilipokuwa nikisoma nilikuwa na walimu walikuwa na heka heka siku ambapo wanagundua kwamba wao wanakuja kukaguliwa na huu ndio mfumo mzuri unaonesha kujenga ustawi wa elimu. Lakini pia walimu kufuata utaratibu ule unaotakiwa katika kuwafundisha vijana wetu. Leo walimu hawana nafasi hiyo ya kufanyiwa ukaguzi na ndio maana tunapiga kelele nyingi na ndio maana tunasema kwamba kiwango cha elimu kimeshuka.

Ninavyofahamu mimi mara kwa mara zilikuwa skuli zinakaguliwa na hili lilikuwa linajenga kwamba mwalimu anakuwa anajua kwamba nafanya kazi na wakati wowote nitakuja kukaguliwa na anajenga utaratibu na nidhamu ya kazi. Lakini leo jambo hili halipo, nimeona jinsi ya hizo fedha walizotengewa kwamba hawawezi kumudu, skuli nyingi sana wanahitaji usafiri, wanahitaji mambo mbali mbali ili waweze kuzifikia hizo skuli. Imefika mahala tunaambiwa kuwa kuna ukaguzi wanaufanya wenyewe walimu wakuu wa maskuli. Mimi hili kidogo linanipa mashaka na mwalimu ni binadamu naye ana mashaka yake ya kuona kwamba hawa nawaongoza mimi na mimi ninaongozwa na wengine. Lakini pamoja na hayo ni vizuri kabisa wakaguzi wapatiwe vitendea kazi usafiri lakini pia majengo yaendane na wakati wa kileo, twende na wakati.

Baada ya kusema hayo sasa niende kwenye Maktaba. Niseme kwamba kwa upande wa Unguja niipe pongezi kubwa wizara kwa kufanya juhudi na kufungua ile Maktaba mpya pale. Lakini lengo ni kuwaweka sawa Wazanzibari wote bila ya kujali upande wowote wanaotokea. Kutokowepo kwa maktaba Pemba iliyopo ni ndogo mno na finyu, nikaona kwamba maelezo yote yametolewa katika kitabu cha mwaka jana kwamba itajengwa maktaba na mwaka juzi pia walisema kwamba itajengwa lakini tatizo bado linaonekana lipo.

Niambie Serikali kwa kuwa mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati katika awamu iliyopita tuliziona jinsi ya fedha zilivyoingia, zilikuwa ni kidogo mno hazitoshi kabisa hata kuanzia chochote. Niombe Serikali ifanye juhudi za makusudi ili kuwajenga usawa wanafunzi walioko Unguja na Pemba waweze kwenda kwenye maktaba hizo kujisomea na kuweza kujiongezea taaluma zao. Niiombe wizara kwa makusudi ipange hilo na ujenzi huo ni matarajio yangu

kwamba mwaka huu itaeleza kuwa mwaka huu itaanza rasmi utaratibu wa ujenzi huu.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende katika ukurasa wa 52 katika kifungu cha 111 ambacho kinagusia Taasisi ya Elimu Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, hichi ndicho kitengo ambacho kinashughulika na mambo ya elimu Zanzibar. Niwaambie kwamba nimeona kwenye kitabu kwamba sasa wanaanzisha mambo mapya katika elimu ya msingi na wamesema kuwa walimu watawapatia maposho. Niwaambie ukweli wanajaribu kuleta mtaala mpya unapoanzishwa ni lazima mwalimu apate ile taaluma yenye kuanza mapema na hatimae aweze kusimamia mtaala ule. Lakini hiyo taaluma ndio inaanzishwa. Walianzisha hii kwa darasa la kwanza hadi la nne na taasisi inasema kwamba skuli 72 walililifanya hilo.
Mhe. Waziri utakapokuja hapa naomba utupe taaluma au utuelimishe tufahamu katika muhtasari, lini hasa mmekigundua inawezekana tuendelee nayo hali hiyo. Hapa nimeona tu kwamba mmeifanya hiyo katika skuli 72. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hapa utakapokuja anifahamishe kidogo. Jengine ni kusema kwamba huu muhtasari pale maskulini hautoshi wakati huu. Nimeona kwamba kuna walimu hili jambo halipendezi na wala halijengi moyo katika jambo hili la taaluma, wanaazimana. Kwa hivyo, hilo ni tatizo hatuwezi kufikia malengo.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende katika uimarishaji wa elimu ya msingi. Kuna mambo mengi yamepangwa kufanywa kuna mtaala mpya ambao unaazishwa lakini nimeona kwamba katika skuli zetu za msingi kuna matatizo makubwa makubwa ya msongomano wa wanafunzi, uwiano wa walimu na wanafunzi ni vitu tofauti kabisa. Haiwezekani kwamba mwalimu mmoja wanafunzi 120 aweze kumudu kuwasomesha hao vizuri waweze kuandika na waweze kufikia malengo na tuseme kwamba tumeboreka kielimu. Hili jambo haliwezekani kabisa na kukosekana kwa jambo hili ndiko kunakoweza kuonesha kwamba ukifika darasa la saba unawataka vijana wa kuingia sekondari. Kwa hivyo, kuna mapungufu unakuta tatizo limejitokeza hapa, msingi mzuri ndio wenye kujenga nyumba imara.

Kwa hivyo, jengo letu kielimu kwa kweli hatuwezi kufikia vyuo vikuu pamoja na kuanzisha kwetu vyuo hivyo na tulikuwa na hamu kweli ya kuanzisha. Kama hatukuona huku chini kukoje na tukaweza kuleta mabadiliko ya kweli kabisa uwiano wa walimu kwa wanafunzi ni mkubwa sana, hali hii ni ngumu na mara nyingi imezoeleka wanawake tunaopewa majukumu ya wale watoto wa darasa la kwanza hadi kufikia darasa la sita. Msongamano ni mkubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu sasa nigusie kuhusu dakhalia. Mhe. Naibu Spika, niipongeze Wizara ya Elimu kwa kukamilika skuli 13. Lakini hapa kuna kauli ambayo inalingana kidogo na kitabu cha pili cha muelekeo wa hali ya uchumi kwa mpango wa maendeleo kwa mwaka 2013/2014 ambacho alikisoma Mhe. Waziri wa Fedha, nyinyi mmesema mna 13, yeye kasema zimekamilika 16 humu. Kwa hivyo, utakapokuja hapa utanambia sahihi ni ipi. Lakini sasa Mhe. Naibu Spika, niwaambie kuwa zile skuli ni mzuri za kisasa ziko vizuri. Lakini skuli zile zimejengwa kitaalamu zinahitaji vifaa mbali mbali vya sayansi ni sambamba na walimu wa sanyansi. Lakini hayo yote hayatoshi kwa kuwa skuli zipo kati kati kila wilaya inahitaji kutoa wanafunzi kutoka sehemu tofauti, wataniambia nini kuhusu skuli hizi na daghalia zake na nyumba za walimu.

Skuli ni nzuri zipo na tunatarajiwa kuzitumia lakini je, mpango wa walimu ukoje kwa sababu tunaona nyumba zile nyengine zimejengwa hazina nyumba za walimu vile vile. Lakini pia daghalia hakuna, tutafanya vipi mpaka tuweze kufikia malengo hayo na majengo tumeshakuwa nayo. Mimi hapa ningeishauri Serikali pale ambapo tunapokea miradi kama hii basi tungeweza kujenga yale majengo machache. Lakini yale yaliokamilimishwa utaratibu wake wote ukoje.

Hizi ni 16 lakini hazina daghalia inaonesha kwamba hazitotumika vizuri hatufikii kabisa matumizi mazuri zitakuwepo. Matumizi yake yatakuwa madogo hazina daghalia, hazina nyumba za walimu. Mhe. Naibu Spika, Kiwani-Mauani ni moja katika skuli hizo wanafunzi wake wanapatikana kutoka Mkoani, watatoka Mtambile na kwengineko waje pale. Si rahisi kwa skuli ilipojengwa kuweza kusema kama mwanafunzi atoke pale halafu arejee katika maeneo husika. Lakini jengine hapa hapa katika skuli hizi ningependa Mhe. Waziri utakapokuja uniambie hivi wanafunzi wa sekondari utawatoa kwa utaratibu gani na kuwaweka pale kuanza skuli hizi.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende katika mradi wa kuimarisha Vyuo vya Kiisilam. Mhe. Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa kabisa Chuo cha Mazizini ni kimoja katika Chuo cha Kiislamu kilicho kizuri, lakini kimeahidiwa kuweka uzio kila bajeti inayokuja hadi tunamalizia kamati uzio huo haujapatikana. Lakini jengine la mwisho kabisa ni kusema kwamba ardhi zote karibu maeneo yetu yote ya Wizara ya Elimu hayana hati miliki, hili ni tatizo. Ardhi hizo zinamegwa megwa na hutoka watu wakasema zao na wakati mwengine husababisha migogoro mbali mbali ambayo walimu huwa inawakuta wanapelekwa mpaka mahakamani.

Kwa kweli bado tatizo la hati miliki za maeneo yote yanayomilikiwa na Wizara ya Elimu hakuna. Ningeiomba Serikali maana Wizara ya Elimu

ijitihidi. Mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati yake na jitihada kubwa wamechukua lakini kwa kweli bado kabisa ina maeneo mengi ambayo hayajawa na hati miliki.

Baada ya kuyasema hayo Mhe. Naibu Spika, sasa niguse kwenye Vyuo vya Elimu Amali. Serikali imeamua kuvijenga vituo hivi vya elimu amali kwa nia mahsusi kabisa kuona kwamba vijana wetu wanakwenda pale watakapomaliza taaluma zao waweze kujiajiri wenyewe na tulipata ahadi kwamba kuna mambo yao wametengewa watakapomaliza.

Mhe. Waziri utakapokuja hapa naomba unifahamishe kwa kuwa kipindi chote cha miaka hii mitatu ilikuwa bado hatujapata wanafunzi ambao wamemaliza kwa mwaka huu, tumepata wanafunzi ambao wamemaliza kwa mwaka wa tatu, tunaomba utuambie, umewapangia mpango gani wa kuona kwamba tunaweza kuwawezesha ili waweze kujiajiri wenyewe.

Jengine niliangalia hapa katika hivyo Vyuo vya Elimu Amali. Niliangalia fani zao kwenye Chuo cha Mkokotoni nimeona kuna fani ya uhunzi, katika mwaka wa kwanza na wa pili na wa tatu, nikakuta kwamba mwaka wa kwanza kabisa kuna wanafunzi 7, mwaka wa pili kuna mwanafunzi 1 hiyo ni jadweli ya 40(c).
Sasa kilichokuwa kimenipa mashaka ni mwaka wa tatu kuna wanafunzi 10 nikawa najiuliza ikiwa walianza mwaka wa kwanza walikuwa 7. Lakini mwaka wa pili alikuwa 1 na mwaka wa tatu wanamaliza 10. Sasa nilikuwa najiuliza walisoma wapi hao wengine wakajazwa hapa kwa upande wa Mkokotoni. Lakini niulize nimeona katika *figures* hizi zimenionesha kwamba kuna fani nyengine hazisomeshwi katika vituo vyengine ni upungufu wa walimu na vifaa. Kuna utofauti baina ya zile fani ambazo wanasomea. Je, haya ni kutokana na upungufu huo.
Baada ya kusema hayo na kupatiwa ufafanuzi kidogo mimi kwa kweli sina nia ya kusema kwamba nizuie fungu, naielewa sana Wizara ya Elimu na matatizo yao lakini ninachokiomba wajitahidi kwa yale ambayo wameyalenga waweze kufikia malengo na wazitumie vyema hizo fedha.
Lakini pia niiambie Serikali nayo iwe na utaratibu kwa ile miradi ambayo pekee ndio ambayo inatoa. Kwa kweli wana ucheleweshaji mkuu wa kuwapa hizi fedha. Mara nyingi hii miradi iliyosimama na wafadhili huwa wanamaliza muda wao. Sasa naiomba Serikali ifanye hivyo.
Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, nasema ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. (*Makofi*).

Mhe. Salmin Awadhi Salmin: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi hii mchana wa leo na mimi nikatoa mchango wangu juu ya hotuba hii

ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi wa mwaka 2013/2014.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuwapongeza wote Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wao wote kuweza kusimamia wizara hii ambayo ni wizara muhimu, wizara ya taaluma ambayo ndio msingi wa mafanikio katika nyanja au katika sekta mbali mbali za nchi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri hapa ametuwasilishia vitabu viwili; kimoja hiki kinachozungumzia juu ya bajeti inayotumia programu na chengine cha hotuba yake, kimeelezwa kwa ufupi. Lakini kimesheheni viambatanisho juu ya mambo mbali mbali ambavyo vitatusaidia katika kujua juu ya mafanikio yaliopo katika wizara yetu.

Mhe. Naibu Spika, katika kitabu hiki cha Mhe. Waziri cha hotuba kwenye ukurasa wa 4 ametueleza mafanikio yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2012/2013 na kuna mambo hapa ameelezea kuna sehemu karibu nane au sita, nimejaribu kuona na kwa kweli nitumie nafasi hii kuwapongeza kwa mafanikio ambayo wameweza kufanikiwa. Watu wamesema kwenye mafanikio hakukosi matatizo, hayawezi kuwa mafanikio matupu tu. Kwa kweli Mhe. Waziri hakutwambia matatizo yake yanayomkabili katika kipindi hiki na kipindi kijacho, ili na sisi wenziwe tukajua kwamba katika sekta hii kuna tatizo moja, mbili, tatu, pamoja na kwamba tunaelewa nadhani ni vyema angeyaeleza kimaandishi tukajua na tukaweza kushirikiana na tukasaidiana namna ya kuyatatua. Pengine mengine hayahitaji hata fedha, yanahitaji ushauri tu tukaweza kushirikiana.

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa wengi wamezungumza katika kitabu hiki lakini mimi nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa kweli amechangia vizuri amekwenda katika maeneo muhimu sana katika masuala ya elimu. Kwa upande mmoja nasema baadhi ya maeneo ametufilisi, amekwenda vizuri ameziangalia takwimu vizuri. Kwa hivyo, mimi nampongeza sana juu wa uchambuzi wake na kwa kweli maelezo yake au uchambuzi wake unahitaji kuzingatiwa kwa makini sana katika wizara hii.

Katika mafanikio Mhe. Waziri alieleza ambalo kidogo ningelihitaji jawabu wakati atakapofanya majumuisho katika hili eneo la idadi ya wanafunzi waliogharimiwa masomo kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu wa Juu Zanzibar, ambapo ametueleza kwamba kiwango kimeongezeka kulingana na takwimu za mwaka jana na mwaka huu. Sisi tuwapongeze kwa kuongeza viwango.

Lakini nikitaka kujua katika hawa ambao wamefanikiwa 1897. Je, ni wanafunzi wangapi waliomba wenye sifa, tukaweza kulinganisha kati ya

waliofanikiwa na walioomba ambao wana sifa kwa sababu tukiona takwimu ya waliomba na waliofanikiwa, basi tunaweza kuungana na Mhe. Waziri. Sasa haya ni mafanikio na ni eneo hili ambalo Waheshimiwa tulikuwa tunalipigia kelele sana na Serikali sikivu itasikia itaongeza kiwango cha fedha. Lakini hatujui wenzetu walipata kiasi gani cha fedha katika zile milioni nane ambazo tuliambiwa kwamba zitakwenda kwenye Bodi ya Mfuko wa Elimu ya Juu. Mpaka kufikia mwezi wa Machi wamepata kiasi gani kwa sababu hizi ni fedha tujue mmepata kiasi gani.

Mhe. Naibu Spika, kilichonishtua zaidi ni katika eneo hili la mpango kazi wa elimu. Mpango Kazi wa Elimu ukurasa wa 8. Katika Mpango Kazi wenzetu wametuletea Mpango Kazi wa miaka minne. Unasema kuna *bullet* moja inasema:

> "Asilimia 50 ya waombaji wa mkopo wa Elimu ya Juu waweze kupatiwa mikopo ya kusoma katika Taasisi ya Elimu ya Juu".

Mpango huo wa miaka minne bado tunazungumzia asilimia 50. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hebu Mhe. Waziri atakapokuja hapa atupe haya mafanikio aliyoweza kufanikiwa ambapo mpango kazi unaelezea kwamba baada ya miaka 4 basi angalau tufikie asilimia 50. Sasa nimekuwa na mashaka pengine hata kiwango hiki cha wanafunzi waliokuwa wameomba basi haikufikia hata hiyo asilimia 50 ambayo ni mpango kazi wa miaka ya baadae.

Jengine Mhe. Naibu Spika, kuna *bullet* ambayo imezungumzia walimu wapya 578 walioajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi, hayo ni mafanikio makubwa ya elimu. Lakini katika eneo hili Mhe. Naibu Spika, limekuwa linalalamikiwa sana, hili la ajira kwa walimu, pamoja na kwamba suala la ajira linashughulikiwa na Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, baada ya kupokea maombi kutoka kwenu. Lakini eneo hili linalalamikiwa sana na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wengi wamelizungumzia suala la ajira juu ya nafasi hizi za walimu, wengine wamesema kumekuwa na upendeleo na kumekuwa na mambo mengi tu.

Sasa suala hili Mhe. Waziri na kwa bahati nzuri na Mhe. Waziri anayeshughulikia masuala ya utumishi na yeye yupo. Hivi kweli kuna tatizo katika eneo hili lakini inaonekana tatizo kweli lipo, kama lipo basi linahitaji kufanyiwa kazi. Hatuwezi kuwaajiri watu kwa upendeleo hili litatuletea matatizo. Sisi tunataka tuwaajiri watu wale ambao wana sifa na kulingana na mahitaji yaliopo katika maeneo, tusiangalie huyu katoka Pemba, huyu katoka Kusini au huyu katoka Kaskazini, hili litatuletea matatizo kwa wananchi wetu. Tuwaangalie watu wenye sifa na mahitaji katika eneo linalohusika, eneo hili limekuwa likilalamikiwa sana Mhe. Naibu Spika.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri tunawapongeza kwa kuwaajiri walimu lakini uajiri huu kweli umekwenda kwa mujibu wa katiba, kwa sababu Katiba inaeleza wazi juu ya eneo hili la ajira kwa wananchi na vijana wengi wamesoma masomo ya *Art* wengine, lakini *Art* yao wanayosoma unakuta wamefaulu pengine Kiingereza wamefaulu vizuri, Kiswahili wamefaulu vizuri, wengine wamepasi *Geograph* ni nzuri. Lakini utawakuta mpaka leo wanasota na utawakuta wenzao wanakwenda mbele. Kwa hivyo, malalamiko yamekuwa mengi. Mhe. Naibu Spika, eneo hili linahitaji kuangaliwa kwa makini.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye mpango kazi, katika ukurasa wa 7. Mpango kazi huu ambao Mhe. Waziri ametueleza kuwa una maeneo mengi ambapo ametoa maelezo kuwa mpango huu unakusudia kunyanyua elimu. Mimi Mhe. Naibu Spika, nilipokua nikiangalia nilijiuliza huu mpango kazi umetokana na nini, lakini baadae nikaona hapa kwamba katika mpango wa mafanikio ambao Mhe. Waziri ametueleza kuna shirika hili la *Global Partnership for Education*, ambapo ina makao makuu yake Mjini Washington. Mhe. Waziri anasema limeidhinisha msaada wa dola za Kimarekani milioni 5.2 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango kazi wa elimu wa Zanzibar kwa kipindi cha miaka 3, kuanzia mwaka 2013/2014 hadi 2015/2016, kumbe ni miaka 3, alisema ni miaka 4. Fedha hizo zinatumika katika kuinua ubora wa elimu yetu katika ngazi ya maandalizi na msingi.

Mhe. Naibu Spika, tuwapongeze wenzetu kwa kutusaidia ambapo wana nia ya kuona kwamba elimu yetu inakuwa bora katika maeneo ya maandalizi na msingi, kwa sababu huu ndio msingi. Unapowaandaa vijana mapema katika mazingira mazuri basi matunda yake nayo yatakuwa mazuri katika elimu ya sekondari lakini hata elimu ya juu. Nimeona hapa juu ya hayo maeneo ambayo mpango kazi unakusudiwa kufanywa katika kipindi hiki cha miaka mitatu, ni malengo mazuri. Lakini utaona Mhe. Naibu Spika, maeneo ambayo Mhe. Waziri amelenga katika mpango kazi zaidi unalenga katika miundombinu ya kuongeza, kwa mfano uandikishaji wa wanafunzi wa maandalizi asilimia 30, uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi ya elimu ya msingi asilimia 95, idadi ya wanafunzi wa darasa ipungue hadi wanafunzi 40 ambayo ni nzuri, kuna msongamano mkubwa na mambo mengine. Lakini kubwa zaidi Mhe. Naibu Spika, umelenga katika miundombinu.

Kuna eneo moja Mhe. Naibu Spika, nadhani wenzetu wamelisahau na ni vyema nalo wakaliweka ni eneo muhimu sana, ni eneo la *quality* ya elimu kama ilivyo dhana ya fedha hizi zilivyotolewa. Wasi wasi wangu kuwa dhana inaelezea jambo hilo lakini kwenye maeneo yalivyogaiwa haikuoneshwa *quality* ya elimu ni muhimu. Mhe. Ismail Jussa kasema hapa kwamba ubora wa elimu ya Zanzibar bado ni mdogo na hata kwa Tanzania kwa ujumla.

Utafiti unaonesha kwamba katika nchi za Afrika ya Mashariki basi Tanzania ndio ya mwisho, tumeshindwa na wenzetu wa Uganda na wa Kenya. Sisi *quality* ya elimu yetu ni mbovu kabisa kuliko nchi nyengine. Kwa hivyo, eneo hili la kuboresha *quality* ya elimu ni muhimu ambalo wenzetu hawakuliweka. Sasa mimi nilikuwa na wasi wasi, hata hayo mengine ni muhimu lakini *quality* ni muhimu zaidi.

Ningemuomba sana Mhe. Waziri kwamba katika eneo hili waweke *bullet* ya kui-*review* kuipitia upya mitaala yetu, pengine hapa ndipo penye tatizo kwenye mitaala. Wenzangu wametangulia kusema hapa, sasa hivi unakuta kila mmoja anasomesha anavyopenda, katika skuli za serikali zina mpango wake, skuli za binafsi nazo zina utaratibu wake na ukija kufuata kwa wenzetu wa Tanzania Bara ambao elimu ya juu ni ya muungano na wao wana taratibu zao. Kwa hivyo, hatuna ule mfumo mmoja ambao unaofanana ulio bora. Kwa hivyo, kwa kuwa tayari nchi zilizotuzunguka wenzetu wamepiga hatua kubwa, basi nadhani kuna haja sasa ya kwenda kuona wenzetu wanafanyaje, sio vibaya, kuliko tukabakia hivi hivi tulivyo, pamoja na kwamba *quality* ya elimu inachangia na mambo mengi, lakini hili nalo ni eneo moja muhimu sana ambalo lingeweza kuwekwa hapa tukaweza kufanya mapitio juu ya mitaala yetu ili tukaona tukoje, tukae vipi au twendeje. Halafu na haya mengine nayo ambayo tumeyaainisha yataweza kusaidia katika kuifanya elimu yetu iwe bora. Kwa hivyo, eneo hilo nalo Mhe. Naibu Spika, ni muhimu.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije kwenye Idara ya Elimu ya Sekondari, wameeleza hapa majukumu yao ambapo wamesema Idara ya Elimu ya Sekondari ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa kazi za ufundishaji kwa ujumla na kufuatilia utendaji kazi wa maskulini, kupanga walimu katika skuli zote za serikali za sekondari na kuwapangia skuli wanafunzi waliofaulu na kadhalika. Mimi nakuja hapa kwenye kupanga elimu katika skuli zote za sekondari.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimekuwa na kilio cha muda mrefu juu ya skuli ya sekondari iliopo jimboni kwangu, Skuli ya Sekondari ya Nyerere hususani walimu wa sayansi. Sio Baraza hili tu, hata tokea Baraza lililopita. Skuli ile ni ya sekondari ina wanafunzi kuanzia kidato cha kwanza na kidato cha pili, inapokea wanafunzi wengi. Lakini inasikitisha sana pamoja na kelele zangu zote ninazopiga bado wizara ya elimu haijaona umuhimu wa kupeleka walimu pale wa sayansi. Sisi tunafahamu kwamba tuna uhaba wa walimu hawatoshi lakini haipendezi hata kidogo kwamba skuli kama ile ina mwalimu mmoja wa sayansi, halafu tutegemee kwamba tutazaa watoto wenye ubora wa kiwango kizuri zaidi ambao watafaulu katika masomo ya sayansi ambapo sasa hivi ndio kipaumbele ambacho tumeweka inasikitisha sana. Hili nimelisema kwa mara ya kwanza, nilisema mara ya pili na leo nasema tena kwamba bado hata

hizi skuli za ng'ambo hatuzipi kipaumbele juu ya walimu wa sayansi kwa nini Mhe. Waziri.

Sasa katika suala hili na kwa kuwa nimeshalisema sana, nataka Mhe. Waziri utakapokuja kufanya majumuisho hebu tupe takwimu za walimu wako wa sayansi, una walimu wangapi wa sayansi, una skuli ngapi ambazo zinahitaji sayansi na hawa walimu wako umewagawa vipi. Kwa sababu tunazo taarifa kwamba kuna skuli za huku mijini ambazo nyinyi ndio mnazipendelea sana, zinao walimu wa sayansi wa kutosha. Skuli moja inaweza kuwa na walimu 20 wa sayansi. Hebu na sisi wa kule ng'ambo tupunguzieni hao walimu au hawa wa ng'ambo huku hamuwataki mnataka wa mjini tu. Hapa Mhe. Waziri nahitaji maelezo ya kutosha na ya kuniridhisha, sikusudii kuondosha fungu, najua maelezo utakuwa nayo mengi ya kutosha, lugha ya matumaini utakuwa nayo kwa wanafunzi wanaosoma pale, tupate hao walimu wa sayansi ili watoto wetu na wao waweze kusoma katika masomo haya. Haipendezi hata kidogo skuli nzima ina mwalimu mmoja tu wa sayansi.

Jengine Mhe. Naibu Spika, mwaka jana nilizungumzia kuhusu posho la walimu wakuu na walimu wakuu wasaidizi na Mhe. Waziri aliniahidi, pamoja na kwamba maposho yanafanywa katika wizara ya utumishi. Mhe. Naibu Spika, nadhani sasa hivi tubadilishe utaratibu, Wizara hii ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora nayo sasa ikae mwisho kama Wizara ya Fedha, ikae karibu ya mwisho mkiani huko, sio sasa hivi inakaa mwanzo inamaliza, kuna mambo mengi ambayo yanamuhusu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora kama alivyo Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Wizara ya Fedha huwa tunaiweka mwisho kwa sababu ni wizara mama, lakini na Wizara hii ya Utumishi wa Umma nayo ni wizara mama kwa sababu inahusu mawizara yote. Tukizungumzia maposho yanahusu wizara zote, tukizungumzia ajira tunazungumzia wizara zote. Kwa hivyo anahusika na maeneo makubwa, hivyo wizara hii nayo sasa iwekwe mwisho katika kuchangia kwa sababu kuna mambo ambayo Waziri wa Utumishi wa Umma tunahitaji maelezo yake akiwa kama waziri katika bajeti yake. Kwa sababu maposho haya ya walimu wakuu tumesema haiwezekani mwalimu mkuu ana dhamana umempa skuli nzima halafu unamlipa shilingi 15,000 au shilingi 12,000 na Mhe. Waziri alituahidi hili atalishughulikia. Kwa hivyo, nataka maelezo.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho ni kuhusu msongomano wa watoto madarasani. Tuna msongomano katika skuli na moja katika skuli ambayo ina msongomano mkubwa ni ile skuli yangu ya sekondari pale, kuna wanafunzi wengi katika darasa moja haipendezi na inatokana na ufinyu wa madarasa. Sasa tumejitahidi hivi karibuni tumejenga banda moja kubwa lenye karibu madarasa sita limeshamalizika. Lakini baada ya kumaliza hilo banda sasa hivi

liko katika hatua ya kuezekwa, linahitaji kuezekwa. Wananchi wameshajenga kwa kushirikiana na viongozi wao. Sasa linataka kuezekwa na ni matumaini ya wananchi wa jimbo lile kwamba litakapomalizika basi angalau ule msongomano utapungua, kwa sababu skuli ile inasomwa na wanafunzi kutoka majimbo mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, nimejaribu kuangalia mpango wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika programu zake, nimeona hapa katika kipindi hiki cha mwaka 2013/2014 wanakusudia kujenga skuli nne nimeona humu. Sasa nimekuwa na mashaka na kwa sababu tayari kuna skuli ambazo tayari huko nyuma ziko kwenye foleni katika maeneo mbali mbali, lakini kuna skuli nne kwenye mradi huu wa uimarishaji wa elimu ya lazima. Kwa sababu nilikuwa naangalia Wizara ya Elimu fedha hizi ambazo wanamalizia mabanda ya skuli ziko wapi, nimejaribu kuziangalia na Mhe. Waziri atakapokuja atakuja kuniambia na nyengine ziko wapi. Lakini nimeangalia katika mradi wa uimarishaji wa elimu ya lazima ambayo wamesema mradi huu utatekelezwa kwa mashirikiano kati ya SMZ na Benki ya Dunia, ambapo kukamilisha ujenzi wa madarasa katika skuli nne za sekondari yaliyoanzishwa na wananchi, sasa kama kuna nyengine atakuja kuniambia kwa kupitia mradi huu.

Lakini ninachoomba Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri sana skuli ile inapokea wanafunzi wengi katika maeneo haya na msongomano upo pamoja na kwamba tayari kuna skuli nyengine zimetangulia zina mabanda, lakini tuangalie zaidi vipaumbele vya maeneo mengine. Hapa mjini kuna msongomano mkubwa na nathubutu kusema hata maeneo ya kujenga yamekuwa tatizo. Nilikuwa naangalia takwimu hapa, ukiangalia Wilaya ya Mjini mbali ya hizi skuli ambazo zinajengwa na wafadhili basi hakuna hata banda moja ambalo linajengwa sasa hivi katika Wilaya ya Mjini kwa ajili ya kuongeza idadi ya kuchukua wanafunzi.

Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba banda lile au jengo lile atukamilishie ili tupunguze msongomano na nimuombe hasa wakati atakapofanya majumuisho basi aje aseme kwamba mwaka huu tutamsaidia Mhe. Mwakilishi kumalizia jengo lile ili limalizike na watoto wetu wapate kusoma kwa nafasi, sio kusoma kwa nafasi zaidi kwa sababu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali unapoongeza madarasa basi unaongezewa kuletewa na wanafunzi, lakini pia itasaidia maana watoto wote ni wetu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri namuomba sana atakapofanya majumuisho hebu anipe moyo kwamba kwa kuwa wananchi wameshajenga banda lile basi katika mwaka huu wa fedha atusaidie ili limalizike na watoto wetu waweze kusoma katika mazingira yaliyokuwa afadhali.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, mimi naunga mkono bajeti hii ya Mhe. Waziri kwa asilimia 100 na nimuombe Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kama yupo au kaimu wake, basi wapewe hizi fedha kwa sababu wizara hii ni muhimu sana. Wizara zote ni muhimu lakini hii ni muhimu sana wapatiwe fedha kwa kadri ya zilivyoomba. Haidhuru utakuta Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imebeba eneo kubwa sana la bajeti yetu karibu bilioni 115, lakini wapatiwe zote ili waweze kutekeleza mambo haya mazuri kwa manufaa yetu. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi).*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa ili nuzungumzie maneno mawili au matatu katika hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwa kuwa bajeti hii ni muhimu sana kwa sababu ni bajeti ya elimu basi na mimi nimeona nitie baraka zangu kidogo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa namuomba nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa juhudi zake anazochukua katika kuwaendeleza vijana wetu katika suala la elimu. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri kwanza pamoja na kuwa huku nyuma wamesema kwamba Wilaya ya Micheweni wameipa kipaumbele kwa kutoa walimu wengi, lakini namuomba Mhe. Waziri aone kwamba bado skuli ya Micheweni ina matatizo ya walimu. Kwa hivyo aiangalie kwa jicho la rehema, maana walimu waliopo pale inafika muda wanahemewa na kusema sijui tusomeshe vipi. Kwa hivyo, aone kama bado skuli ya Micheweni inahitaji kuongezewa walimu.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine naomba nilaumu kidogo kwa sababu anayefanya vizuri na kulaumiwa hakosi, nimlaumu mimi. Kulianzishwa skuli ya Maziwa ya Ng'ombe anaijua Mhe. Waziri, skuli ile ilikuwa bado haijawa na walimu, kwa hivyo kulikuwa na vijana ambao walikuwa wakijitolea pale kusomasha ile skuli na walichukua juhudi kubwa ya kusomesha. Lakini kwa bahati mbaya mno, nilizungumza naye Mhe. Waziri kabla ya kutoa hizo ajira, nikamwambia Mhe. Waziri naomba sana wale vijana waliokuwa wakijitolea basi muwaangalie kwa jicho la rehema ili wapate ajira wale vijana kwa sababu wamejitolea na wamechukua muda, skuli haina walimu walichukua juhudi ya kusomesha. Kwa hivyo, muone kwamba zile nguvu na jitihada zao walizochukua basi zizae matunda, kwa bahati mbaya mno wale vijana walikuwa ni vijana watano na waliajiriwa wawili, watatu tena wanawake watupu hawakuajiriwa hata mmoja pamoja na jitihada kubwa walioichukua.

Kwa hivyo, bado namuomba Mhe. Waziri awaone wale vijana kwamba asiwavunje moyo ile jitihada yao waliyoifanya basi izae matunda, namuomba sana itakapotokea ajira basi awafikirie sana vijana wale, kwa sababu

wamechukua jitihada kubwa sana ya kuboresha ile skuli kwa kusomesha kabla hapajawa na walimu. Kwa hivyo, namkumbusha sana Mhe. Waziri kwamba jitihada yake aliyoifanya walipata ajira wawili, lakini vijana watatu bado hawajapata. Kwa hivyo na wao hawakuona vizuri hata kidogo kutokana na jitihada zao walizofanya halafu wakaachwa njiani.

Jengine ambalo nataka kulizungumza ni suala la elimu hii tunayoita elimu mjumuisho. Mhe. Naibu Spika, siku moja hapa liliulizwa swali na mimi niliuliza swali kuhusu hawa vijana wetu ambao ni walemavu. Nikauliza swali kwamba inakuaje hawa vijana kama ni walemavu lakini wakati wa kusainisha mitihani ikawa tunawaweka sawa sawa na hawa waliokuwa ni wazima. Je, hatuoni kama hawa walemavu tunawaonea. Bado narudia tena kulizungumza suala hili, kama Mhe. Waziri hawa vijana walemavu kuna walemavu wa macho, walemavu wa akili, kuna walemavu ambao kuwa ni viziwi hawasikii na kuna walemavu wa viungo, hawa walemavu wa viungo wanaona, wanasikia na wanafanya kila kitu isipokuwa tatizo lao linalowakabili ni viungo vyao. Lakini walemavu kama viziwi na wasioona Mhe. Waziri tunakwenda kusainisha mitihani halafu tunawaweka sawa sawa na wale ambao wanaona, tunawaonea. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wizara yake ione haja ya kuweka fungu la makusudi kwa hawa watu ambao wana ulemavu wa uziwi na kuona kwamba wapewe fungu maalum, mitihani yao isisainishwe sawa sawa na hawa watu waliokuwa na akili zao timamu na viungo vyao viko kamili.
Suala jengine ni kwamba Mhe. Naibu Spika, naomba hasa na kwa sababu ulituambia kwamba vitakuja vifaa vya hawa walemavu, kama sijui nukta nundu, sijui na vile vya kusomea wale waliokuwa hawana macho na vitu vya kusikilizia wale viziwi. Lakini Mhe. Naibu Spika, hasa ilivyo hawa sio kuwatenga kwa ajili ya kuwa wana ulemavu, lakini ni kuwasaidia japo kama kutakuwa kuna madarasa ya mjumuisho, lakini wangetengwa jamaa hawa wakawa wanapata elimu yao ili na mitihani yao ikawa ni ya sehemu maalum na wakapewa vipaumbele maalum, wakawekewa kiwango ambacho sio kama cha watu wa kamili. Ningeomba sana hili lifikiriwe kuwa tunawaonea jamani. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba sana wizara yako ifikirie suala la hawa watu ambao hawaoni na hawa viziwi ambao hawasikii, hilo ni jengine.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo nataka kulizungumza hili nimewahi kulizungumza katika bajeti zinafika tatu. Nilianza kwa Mhe. Haroun Ali Suleiman alipokua ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, nikaja kwa Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban alipokuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na sasa hivi liko kwako wewe Mhe. Ali Juma Shamuhuna. Mhe. Waziri kwa suala hili mara hii nitakuwa mgumu sana, sijui mtanijibu vipi mpaka niridhike ili nisiwe mgumu.

Mhe. Naibu Spika, kila siku nazungumza suala la Chuo cha Kiislamu kilichopo Kiuyu. Nazungumzia suala la kuwa na gari ambalo litawasaidia wale watoto na nazungumzia kila siku kuhusu Msikiti, nawaambia kile ni Chuo cha Kiislamu, inakuaje Chuo cha Kiislamu kisiwe na Msikiti. Leo vijana wanatumia yale madarasa yao yaani vile vyumba vya madarasa ndio wanavyovifanya Misikiti wanaswalia. Mhe. Naibu Spika, nimeomba kwa siku nyingi kwamba hawa vijana wajengewe Msikiti pale katika Chuo cha Kiislamu Kiuyu. Lakini kila siku napigwa danadana huku naelezwa mara hii tutakwenda kujenga halafu watu wanakaa kimya. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, kwa mara hii naomba suala hili nipewe jibu zuri na lenye uhakika kwamba Msikiti kama utajengwa basi kweli ujengwe na kuhusu gari, kwa sababu wale vijana pale wako mbali na hospitali na pale pana watu zaidi ya 600 wanaokaa pale. Kwa hivyo kama hapana gari ya uhakika wanapata matatizo, anapoumwa mtu inakuwa ni matatizo. Gari ya Mbunge au Mwakilishi hata ikienda kuchukuliwa iko mbali au ya hospitali hata ikenda kuchukuliwa iko mbali.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri aone kuwa suala la kuwa na gari pale katika Chuo cha Kiislamu Micheweni ni suala ambalo ni muhimu, pamoja na jitihada anayochukua ya kujenga uzio, lakini ni muhimu kuwa na usafiri pale ili watoto wetu wasipate tabu. Pale wanaanguka usiku watu wanakuwa wanapata shida sana. Naomba Mhe. Waziri kuhusu suala hili nipatiwe majibu mazuri. Mimi sina tabu naye babu yangu lakini naomba anipe majibu yaliyokuwa na uhakika kwa sababu nimeshapigwa danadana sana, mawaziri wawili waliopita hapa. Nilikuwa nazuiana nao halafu wananipa majibu kisha yanaachwa kwenye kapu, kwa mara hii nipewe jibu ambalo litakuwa na uhakika kabisa.

Suala jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo nataka nimalizie. Alizungumza hapa mwenzangu kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inatakiwa iwe na hati miliki kwa maeneo yake iliyokuwanayo, hili ni suala la msingi sana kuwa na hati miliki kwa sababu kama hamna hati miliki ya sehemu zenu basi kunazuka migogoro.

Mfano mmoja Mhe. Naibu Spika, ni huu mgogoro wa ardhi uliopo kwenye shamba ya Mzee Ayoub Suleiman. Huyu Mzee Ayoub Suleiman wa Ndagoni shamba lake limechukuliwa kwa ajili ya kujenga skuli, kwa hivyo kama limechukuliwa na wakati yeye mwenyewe ana hati miliki zake zitamsaidia. Sasa wizara nayo kama ingekuwa na hati miliki basi isingekuja hii ya kuwa ni eneo lake, lakini ni eneo lake kwa sababu yeye ana hati miliki anayomiliki kuwa ni eneo lake. Namuomba sana Mhe. Waziri wafanye jitihada ya kukutana na huyu mrithi Suleiman Ayoub huyu wa Ndagoni ili tatizo hili walimalize kwa sababu tatizo la kuwa kila siku linakuja kupigiwa kelele hapa

sio suala zuri. Namuomba Mhe. Waziri achukue jitihada waende wakakae kitako na huyo mrithi ili watatue tatizo hili na walipatie ufumbuzi ili huyu mrithi kama ni kumpa fidia ya haki yake basi apewe fidia, lakini amesharidhika na kuliko hivi kupiga kelele na ikawa yeye hajaridhika, kwa sababu eneo lake limechukuliwa na wala si haki kuchukuliwa eneo lake kama hajaridhika yeye mwenyewe. Kwa kweli itakuwa si kumtendea haki na wala sisi itakuwa hatufanyi haki.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri kwamba walione suala hili na kuweza kulimaliza tatizo hili la Ndagoni, ili iwe ni haki pamoja na halali kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kuliko kupigiwa kelele kila siku.

Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa hayo machache. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa nafasi tunampa Mhe. Mohammed Mbwana Hamad na tumalizie na Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, na mimi nachukua nafasi ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia mchana huu kuwepo hapa katika kutekeleza majukumu yetu ya kitaifa.

Pili nakupongeza wewe kwa kunipa nafasi hii angalau na mimi kuchangia mawili matatu katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ambayo ni muhimu sana juu ya hotuba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mhe. Ali Juma Shamuhuna. Kwa kweli nampongeza kwa uwasilishaji wake pamoja na kuwapongeza watendaji wake wote kuanzia Mhe. Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu na Wakurugenzi wote. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa tokea jana tunazungumzia hotuba hii basi michango yangu mimi itakuwa ni mifupi sana. Kwa hivyo, nianzie mchango kwenye ukurasa wa 5 wa kitabu hichi kuhusu mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, naipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali juu ya mafanikio makubwa waliyoyapata katika kipindi hichi cha mwaka 2012/2013. Miongoni mwa mafanikio haya nashukuru kwamba jimbo langu limeingia katika ujenzi wa skuli mpya za sekondari 13. Kutokana na hali hiyo, napongeza sana kwamba Skuli ya Ngwachani imo katika jimbo langu na hili limenipa faraja. Kwa kweli hivi karibuni tu nimetembelea pale Skuli ya Ngwachani nikenda ofisini pale na vijana wakaniambia Mheshimiwa jengo letu liko hivi tena ni zuri tu, lakini tunakuomba utusaidie mapazia ambapo

ofisi zote za Mwalimu Mkuu na sehemu nyengine na hii nauunga mkono sana. *(Makofi).*

Jambo la pili Mhe. Naibu Spika, niende katika mafanikio kuhusu ujenzi wa skuli mpya za sekondari za ghorofa katika maeneo ya Kiembesamaki, Kwamtipura, Mpendae, Kibuteni na Mkanyageni. Nataka nizungumzie kuhusu Skuli ya Mkanyageni. Mhe. Naibu Spika, kuna tetesi kwamba kuna baadhi ya majengo yatapunguzwa pale katika ujenzi wa skuli hii ya ghorofa na miongoni mwa majengo ambayo yatapunguzwa ni ujenzi wa Msikiti katika eneo lile. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika namuomba Mhe. Waziri kama hivi ni kweli basi suala hili la Msikiti liangaliwe upya kwa sababu jengo lile la ghorofa watakuwepo wanafunzi wengi kutoka maeneo mbali mbali ya Kisiwa cha Pemba na kwengineko wapi watakwenda kusali.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri kwamba suala hili aliangalie kwa makini sana jengo hili liwepo, ili kuwafanya wanafunzi wale watakaokuwepo wawe na utulivu mkubwa katika kufanya shughuli zao za ibada.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu maslahi ya walimu. Mhe. Naibu Spika, maslahi ya walimu ni kitu muhimu sana, kwa kweli walimu wengi hivi sasa hasa wa skuli za msingi wanaonekana kwamba maslahi yao ni madogo pamoja na marekebisho yanayofanywa kila baada ya kipindi, lakini inaonekana kwamba maslahi yao ni madogo.
Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri hili aliangalie kwa kina sana na ninafikiri hili litafanikiwa vizuri watakapoangalia *scheme of service*, kwani wapo walimu wetu ambao wamefanyakazi miaka mingi, lakini malipo yao ni madogo na inakuwa ni kilio cha hali ya juu kabisa.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba hili aliangalie, ili walimu wetu wajisikie, kwa sababu wapo walimu wetu wameajiriwa tokea miaka ya 1970 na mpaka leo wapo wana viwango vidogo vya elimu na wako msingi. Jambo hili kwa kweli litawapa kilio kikubwa wakati watakapostaafu wakiwa na pencheni ndogo sana. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri hili aliangalie ili walimu wetu wajisikie vya kutosha.

Vile vile katika maslahi ya walimu kwa masikitiko makubwa niseme kwamba kuna walimu hufariki, yaani wanakufa katika vipindi vya kazi. Lakini Mhe. Naibu Spika, familia za walimu hawa zinachelewa kupewa kile kiinua mgongo. Kwa mfano, kuna mwalimu katika Skuli yangu ya Chambani pale, yaani jimboni kwangu amefariki tokea mwaka jana tena mapema tu, lakini mpaka leo warithi wake wameshindwa kupata haki yao kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia

kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba hili aliangalie kwa kina sana, kwa sababu hawa watoto wanapata tabu wapate angalau kiliwazo baada ya kifo cha mzee wao.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo sasa niende kwenye ukurasa wa 15 kuhusu kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Elimu Mbadala Wingwi Mtemani. Kwanza hapa nimpongeze sana Bwana Shoka Hamad Abeid na familia yake kwa kutoa ardhi yao kujengwa skuli hii. Hata hivyo, inasikitisha sana kwamba skuli hii tokea ilipoanzwa mpaka leo imeshindwa kumalizwa. Mhe. Naibu Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri kwamba ni lini wizara yake italimaliza jengo hili ili yale malengo yaliyokusudiwa yafanikiwe. Katika ukurasa wa 20 wa kitabu hichi ambapo ni kuanzisha ujenzi wa dakhalia Skuli ya Sekondari Kengeja Ufundi. Mhe. Naibu Spika, hili ni suala zuri na kwa kweli itakapojengwa dakhalia pale itakuwa tumewapumzisha sana watoto wetu wanaosoma pale kutokana na shida na tabu ambayo wanayoipa hivi sasa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nataka nimueleze Mhe. Waziri kwamba wanafunzi wa sekondari Kengeja Ufundi hivi sasa wanalala katika vyumba vya madarasa na hili ni tatizo. Kwa hivyo, kujengwa kwa dakhalia hii, kwa kweli itapunguza kero na usumbufu wanaoupata wananfuzi wa pale, pia kutaleta amani na utulivu katika ya mchanganyiko wa wanafunzi wa kike na wa kiume. Mhe. Naibu Spika, suala la ujenzi wa dakhalia lipewe nafasi na wala lisicheleweshwa kwa muda mrefu.

Pamoja na ujenzi huo wa dakhalia lakini kuna mapungufu pale na wenzangu wengi wamechangia kuhusiana na hati miliki, lakini Skuli ya Kengeja Ufundi mpaka bado haijapatiwa hati miliki. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri ashirikiane na wizara husika kwa skuli zote pamoja na maeneo yote ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali yapate hati miliki ili muweze kujitanafasi katika shughuli zao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia katika Skuli ya Ufundi Kengeja kuna matatizo yanayowakabili walimu wetu wapya wanaokaa katika nyumba zile kuna madeni makubwa ya *bill* ya umeme. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika nimuombe Mhe. Waziri kwamba suala hili alishughulikie ipasavyo, kwani walimu wanapata usumbufu wa kukatiwa umeme mara kwa mara kutokana na deni kubwa la umeme ambalo lipo pale. *(Makofi).*

Nikiendelea katika Skuli ya Ufundi Kengeja moja katika changamoto iliopo ni ukosefu wa dereva na pale hapana dereva. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli watoto wetu wanapata tabu wakati mwengine wanaumwa usiku wanataka kupelekwa hospitali Mkoani ambako ni mbali na wala hakuna dereva,

isipokuwa kuna *bursar* ambaye anasaidia kwa sababu pia ni dereva, lakini hakuajiriwa pale kama ni dereva. Kutokana na hali hiyo, Mhe. Naibu Spika, tunaomba pale ajiriwe dereva au huyu *bursar* basi imtambue kufanya kazi ya u-*bursar* na halafu afanye kazi ya udereva impe posho ili naye ajisikie katika hali ambayo anafanyakazi hizo mbili.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nizungumzie kuhusu Vyuo vyetu vya Kiislamu. Kwa kweli Vyuo vyetu vya Kiislamu hapa ni Chuo cha Mazizini. Miongoni mwa matatizo ya Chuo cha Kiislamu Mazizini ni kuvamiwa kama walivyosema Wajumbe wenzangu kwamba maeneo mengi yanavamiwa kwa kukosekana uzio, chuo kile ni kikongwe tena ni cha muda mrefu. Kwa hivyo, tunaomba ifanywe iwezekanavyo lakini eneo lile lijengewe uzio ili lile eneo liweze kuhifadhika na wavamizi wa ardhi kila siku.

Pia tunacho Chuo cha Kiislamu Micheweni. Mhe. Naibu Spika, Chuo cha Kiislamu Micheweni, tatizo moja miongoni mwa matatizo yaliopo ni kwamba pale hapana mshauri wa wanafunzi wa kike baada ya kuondoka Mhe. Bihindi Hamad Khamis ambaye ni Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo basi hajaajiriwa tena na kama ameajiriwa jana au juzi basi *fahuwa llmudari*. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika naomba suala la *Matron* katika Chuo cha Kiislamu Micheweni liangaliwe upya ili apelekwe *Matron* na wanafunzi wa kike wapate ushauri.
Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nizungumzie kuhusu walimu waliosomea Elimu Mjumuisho. Mhe. Naibu Spika, Elimu Mjumuisho kama walivyotangulia wenzangu kusema kwamba walimu hawa wanapata tabu sana kutokana na ule mkusanyiko wa wanafunzi wenye mazingira tofauti. Lakini inasikitisha kwamba wapo walimu wamesomea Elimu Mjumuisho karibu mara mbili zilizopita, yaani mikupuo miliwi iliyopita lakini hata ule mkupuo wa kwanza hawajarekebishiwa malipo yao.

Sasa kama hivyo ndivyo basi naomba Mhe. Naibu Spika, kwamba suala hili liangaliwe ili walimu hawa na wao waondokane na ile tabu ya kutoka mwalimu ambaye amesomea apewe katika mshahara wake kwa kusomea ndani ya kodi hii ya Elimu Mjumuisho.

Mhe. Naibu Spika, niende katika Ofisi ya Mkaguzi Mkuu na hapa nataka nizungumzie kuhusu kipengele kimoja tu. Kwa kweli ukaguzi ni kitu muhimu katika elimu kwani bila ya ukaguzi basi kila siku tutakuwa tunapiga kelele tu kwamba wanafunzi wanafeli, kwa sababu usimamizi wa walimu kwa wanafunzi unakuwa ni mdogo. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba Kitengo hichi cha Ukaguzi kipewe nasafi kubwa na kama itawezekana basi wawepo wakaguzi wa elimu wa wilaya,

yaani kila wilaya iwe na mkaguzi kama vile zamani ili wazipitie skuli na kutoa ushauri wa mambo mbai mbali yanayofaa katika shughuli zao za elimu.

Mhe. Naibu Spika, suala hili la Ofisi ya Mkaguzi pale Pemba linasikitisha sana, yaani ofisi yao ni ndogo sana na wala haikidhi haja kuna changamoto tofauti ikiwemo hata gari ya kwendea katika masuala yao ya kuzizunguka skuli zetu za Pemba nzima. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika namuomba Mhe. Waziri aliangalie kwa kina na badala yake lifanyiwe ufafanuzi ili wakaguzi wetu wapate eneo zuri la kukaa pamoja na vitendea kazi ambavyo vitawafikisha kule ambako wanakwenda.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia mchango wangu kwa sababu kuna mwengine atakuja baadaye, basi naomba kuuliza tu swali kwamba walimu wa *science* kutoka Nigeria bado wapo? Kama wapo je, tumefaidika nini katika kipindi hichi ambacho wamekuwepo katika skuli zetu hizi za Unguja na Pemba?

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante kwa kujali muda. Sasa nafasi tunampa nafasi mchangiaji wa mwisho Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ndogo na mimi kujibu baadhi ya hoja ndogo ndogo za Waheshimiwa Wajumbe na pia kutoa mchango wangu kama Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kumpongeze Mhe. Waziri kwa kazi yake kubwa anayoifanya katika kuendeleza au kulielekeza jahazi hili la elimu katika kiwango kikubwa zaidi. Vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Naibu Waziri Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake wote.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja kwa kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutekeleza ahadi yake katika Jimbo langu la Mpendae. Sambamba na kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo imeahidiwa kwa imara zaidi. Mhe. Naibu Spika, inaelekea Mhe. Rais hii Ilani ya Chama cha Mapinduzi inatekelezeka. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu tu kidogo niweze kunukuu Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika ukurasa wa 188.

Ilani ya Chama cha Mapinduzi ukurasa wa 188 kifungu cha 7 kinaeleza hivi:-

> "Kutajengwa skuli mpya 21 za sekondari Unguja na Pemba. Skuli hizo zitajengwa katika vijiji vya Muwanda, Matemwe, Chaani, Dole, Uzini, Paje Mtule, Tunguu, Dimani, Kiembesamaki, Kibuteni na Mpendae na hizo kwa Unguja. Lakini kwa Pemba amezidi kuendeleza na mwenzangu aliyepita amezisoma kidogo".

Kwa hivyo, ninachotaka kusema Mhe. Naibu Spika, kwanza Ilani hii ya Chama cha Mapinduzi inatekelezeka ipasavyo, hivyo tuiamini na tumuunge mkono Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kuitekeleza Ilani hii ya Chama cha Mapinduzi. Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Jimbo la Mpendae napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Chama cha Mapinduzi pamoja na Rais wa Zanzibar kwa kutekeleza ilani hii kwa asilimia mia moja kwenye jimbo langu la uchaguzi. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, mimi labda niseme nitoe haja ya Waheshimiwa Wajumbe wengi waliosema kwamba baadhi ya vyuo vyetu vya Zanzibar viunganishwe na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*). Kwa kweli dhana ni nzuri sana Mhe. Naibu Spika, kwa sababu hiyo na kuliona hilo na serikali yetu imeliona na tayari imeanza hatua za mwanzo kwa kuweza kuviunganisha vyuo hivi na vyuo ambavyo vitaanza ni Chuo cha Afya na Chuo cha Kilimo ambavyo ndivyo vitakuwa kwa hatua ya mwanzo.

Nafikiri sote tunakumbuka kuwa madaktari wetu wanasoma chini ya ufadhili wetu au wataalamu kutoka Cuba. Sasa chuo kitaungana na wale kwa kutoa *degree* zile lakini pia kuchukua na vyuo vyengine vidogo vidogo, ili kuweza kuimarisha chuo chetu pamoja na vyuo vyengine kuonekana mustakbali wa Chuo Kikuu kuwa ni ndio Chuo Kikuu cha Taifa na kitoe sura imara ya Zanzibar yetu.

Vile vile kuna baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wamesema kwamba kuunganisha na Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka, dhamira ni nzuri. Mhe. Naibu Spika, nataka kusema kwamba Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka hakichukui mitihani yake kutoka *NACTE*, isipokuwa kimesajiliwa tu kule, kwa sababu Vyuo Vikuu unaweza kuvisajili *NACTE* au *TCU*, lakini kile kilisajiliwa kule kutokana na ule mwanzo wake ulivyokuwa na kinatoa *degree*. Hata hivyo, ushauri wao ni mzuri na utafikiriwa na serikali lakini Mhe. Waziri atakuja kueleza zaidi nadhani chuo hichi kukileta katika *SUZA*

sio kibaya kwa sababu ni fani ambayo nyengine inayotakiwa na utaratibu wa serikali hivi sasa mwingi unafuata masomo yale ambayo yanatolewa pale.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nizungumzie *Sultan Qaboos Academic Fellowship (SQAF)*. Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana ndugu yangu *Professor* Idris Ahmada Rai pamoja na Dr. Rawya Al-Busaidi Waziri wa Elimu wa Oman, kwa kubuni fikra hii na kukaa pamoja kuweza kupata angalau tukaona sasa Zanzibar tunasaidiwa mzigo mkubwa ambao umetukabili. Kwa kweli tukubali kuwa serikali haitaweza kuwasomesha wataalamu wengi nje ya nchi kwa fani kubwa, lakini kigoda hichi cha Sultan Qaboos watu wakiamini. Mhe. Naibu Spika, nataka kusema kwamba hapa haurudi Usultan, isipokuwa hichi ni kigoda ambacho kinajitegemea kwa elimu na kitatupatia wataalamu wengi ambao baadaye nafikiri serikali yetu itaringia kabisa.

Sasa kwa kuanzia hivi sasa tumepata kwa *PhD,* tumepata watu 9, *Masters* tumepata 7, *Bachelor* tunategemea kupata 4 mpaka 6, lakini mazungumzo bado yanaendelea. Mhe. Naibu Spika, watu waliomba wote wamejitokeza wengi na huu ndio muda mzuri sana kwa kuomba ambapo watu 300 wameomba hapa kuweza kupata nafasi hii.
Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kwa wananchi wa Zanzibar watumie kigoda hichi na hapa kuomba kwake ni *online*, kwa sababu imewekwa hivi hatutaki kuona kwamba watu wanachaguana kindugu au kimjomba, kishangazi wala kimadaraka, isipokuwa kila mtu atakayekuwa na uwezo basi anaweza kuchaguliwa na wala sio kisiasa na tunaomba tueleze hilo ili waweze kutufahamu zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la ufaulu wa wananchi wa mwaka 2012/2013 na wajumbe wengi wameeleza jinsi ya ufaulu ulikuwa mdogo na asilimia ya *Form IV* ilikuwa ni 14 na *Form VI* ilikuwa ni asilimia 32 ni kweli asilimia. Lakini tuangalie nani wa kulaumiwa je, tuilaumu serikali tuinyooshee kidole kimoja serikali na vidole vinne vinamuelekea nani, tuielekezee kidole kimoja Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na vidole vyengine vinamuelekea nani.

Mimi nafikiri wakati tunajenga nyumba moja basi tusigombanie fito, isipokuwa tuelekezane na tuwaelekeze wenzetu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuweza kufanya jambo ambalo linaweza kufanyika. Vile vile baadhi ya wajumbe wamesema hatukushirikishwa katika ile Tume ya Pinda. Mhe. Naibu Spika, mimi nasema sio kweli Baraza la Wawakilishi tulishirikishwa ipasavyo na Mjumbe wetu ni Mwakilishi makini wa Jimbo la Konde Mhe. Suleiman Hemed Khamis alikuwa ni Mjumbe katika tume hii. Sasa je, nani ambaye hakushirikishwa kwenye Baraza la Wawakilishi au

labda niweze kushirikishwa mimi ndio niseme tayari kuwa nimeshirikishwa au Baraza ndio limeshirikishwa. Kwa kweli wakati mwengine naomba wakati mwengine tuache siasa na twende katika ukweli na tuzungumze kitu cha ukweli na wala tusiwape *bad impression* wananchi wetu, isipokuwa tuzungumze kitu cha ukweli na serikali inafanya lile ambalo linawezekana.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye Bodi ya Mikopo. Bodi hii inajitahidi sana kutoa mikopo kwa wanafunzi wetu. Lakini tukubali kwamba umezidiwa na kuzidiwa kwenyewe ni fedha chache ambazo inazo na fedha chache inategemea na mapato yetu sisi Zanzibar nzima na wala hatuwezi wakaweza kupewa udhamini wanafunzi wote wanaomba. Hata hivyo, tunawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wachukue hatua hii madhubuti kuweza kuwaelimisha wananchi wetu majimboni, ili kujua basi huu uombaji wa Bodi za Mikopo. Kwa mfano, kuna wengine wanaomba mara mbili na wanazipa nafasi za wenzao.

Sasa ni vyema kuomba sehemu moja kwa wale wanaopata Bodi ya Mikopo ya Taifa ya Bara, basi waweze kupata na hawa wa Zanzibar pia waweze kupata, tutumie vigezo mbali mbali. Lakini unakaa muda mwingi na hata tukeshakuwagundua basi wengi wameomba huku na huku na inakuwa ni tatizo na muda umeshakwisha na matokeo yake tunalaumiana na wala hatuna kwa kwenda.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mkurugenzi wa Bodi ya Mikopo kwa hatua yake. Vile vile nataka nimshauri pamoja na wizara kwamba iweze kutafuta vyanzo vyengine vya fedha ili basi kuweze ku-*inject* katika mfuko ule ili uwe mkubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu wa China wanasema hatuwezi kufika hatua elfu moja (1,000) kabla hatujaanza hatua moja (1). Kwa hivyo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tayari imeanza hatua moja na tayari imefika 100 kuelekea elfu moja. Nataka kuwaambia Waheshimiwa Wajumbe waweze kuwashajihisha wanafunzi wote na waweze kuikubali Bodi ya Mikopo kuwa inafanyakazi imara pamoja na Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Amali na wala wasiwe na wasi wasi juu ya hilo na watatekelezwa kadri inavyowezekana.

Mhe. Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu maktaba. Kwa kweli huduma yetu ya maktaba ni nzuri sana ambayo kwa Zanzibar huduma hii tunaipongeza sana Wizara ya Elimu kwa kutuwekea maktaba ambayo iko *center* pale na ina vitabu vya kutosheleza. Lakini Mhe. Naibu Spika, huwezi kufananisha Morogoro na Dar-es-Salaam na Waheshimiwa Wajumbe wengi wamesema hapa kwamba *population* ya Zanzibar ni kubwa kutofautisha na

Pemba. Sasa tukiwa tunazungumza Waheshimiwa Wajumbe kwamba Pemba hakujajengwa maktaba kama ile au kama ile, isitoshe na mimi nitakuja kusema na mimi mbona na Donge sijajengewa maktaba kama ile, mbona Mpendae hatujajengewa maktaba kama ile. *(Makofi).*

Jambo la msingi ni kuangalia ile *center* yenyewe na vipi wananchi wameikubali pahala penyewe. Kwa hiyo, ninadhani Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwamba tuwashauri waweze kuweka maktaba ambayo kidogo inaonekana Pemba, lakini hasa iweke *center* Zanzibar kwa sababu kuna watu tofauti, makabila tofauti na wanaotoka sehemu mbali mbali ambao wanaweza kujisomea pale.

Mhe. Naibu Spika, sijawahi kuona wanafunzi wa elimu ya juu wanatoka Unguja labda wanakwenda Pemba, lakini vyuo vikuu vyote viko Unguja, sasa maktaba ile kubwa iwekwe wapi? Kwa kweli nilizungumza mapema kuwa hatuwezi kufika hatua elfu moja kabla hatujaanza hatua moja. Lakini leo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeanza na tayari imeanza kwenda hatua mia moja na mimi nadhani itafika hatua elfu moja baadae.

Mhe. Naibu Spika, ni maamuzi na Mhe. Hamza Hassan Juma alipokwenda China yeye na Mhe. Ali Salum Haji kwamba watu walikuwa wameamua kufanyakazi kwa pamoja, wameamua kutekeleza majukumu yao kwa pamoja na mimi ninawaomba Waheshimiwa Wawakilishi ambao ni wa wananchi majimboni mwao tuweze kuamua na kuchukua majukumu yetu vizuri na tumsaidie Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri katika utekelezaji yao makubwa sana.

Tunawaona na wanafanyakazi kikamilifu na Mhe. Waziri ni jembe anaweza likalimwa popote na mimi ninamuamini anapoamua, basi anafanya na anasaidiwa kwa karibu zaidi na dada yangu Mhe. Zahra Ali Hamad Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa hatua kubwa zaidi.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu ndio huo tu na niseme kwa leo nataka niseme hilo, lakini niwapongeze wote waliotayarisha hotuba hii kwa pamoja na niseme nikushukuru sana. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri, ahsante sana. Waheshimiwa Wajumbe naomba kabla sijaahirisha nitoe tangazo la Mwenyekiti wa UWAWAZA anasema kwamba wale Waheshimiwa Wanawake wote mukimaliza kikao hichi muwasubiri humu ndani kuna mambo muhimu mnataka kuelezwa.

Baada ya hayo, niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa ushirikiano wenu na tunaomba kesho tuje mapema na Mhe. Haji ataanza kujibu hoja kidogo na baadaye tumwite Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na hatimaye Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, ili tumalize hotuba hii na kesho tena tusome hotuba nyengine ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Baada ya maelezo hayo, naakhirisha kikao hichi hadi kesho siku ya Alhamis tarehe 18/07/2013 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 7:57 mchana Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 18/07/2013 saa 3:00 asubuhi))